Nipashe
Jumatano Septemba 4, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 05780014
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper


siasa
Nipashe
HABARI BORA NA KAMILIFU
Katibu Mkuu UN amaliza ziara Mashariki ya DRC
Ibrahim Mohamed Kaduma 1937-2019, mtawala, msomi na mzalendo
Wafuasi wa Trump Italia wajitoa serikalini, waingia rasmi upinzani
DC Muwango: Nachingwea ni ya maendeleo kwanza, ndipo vyama

UKURASA 13



## Pacha mmoja waliotenganishwa Saudia afariki dunia Muhimbili

UKURASA 2

# Kontena 700 ushuru kaa la moto serikalini

UKURASA 2


**YALIYOMO**

UKURASA WA 3
**MVUA KUBWA KANDA YA ZIWA YAJA**
MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), imetoa utabiri wa mvua za vuli huku wakitoa tahadhari kwa mikoa ya Kanda ya Ziwa ambayo inatarajiwa kupata mvua nyingi...

UKURASA WA 4
**AUAWA TUHUMA ZA KUIBA TOCHI**
HASSANI Mangochi mkazi wa Mtaa wa Wapiwapi Kata ya Napupa wilayani Masasi mkoani Mtwara (35)...

UKURASA WA 8
**VIJANA 400 WACHAGULIWA KUJIUNGA IDARA UHAMIAJI**
JESHI la Kujenga Taifa (JKT), limetangaza orodha ya majina ya vijana 400 wa JKT Operesheni Kikwete na Operesheni Magufuli...




Rais mstaafu Benjamin Mkapa na mkewe, Mama Anna Mkapa, wakitoa heshima za mwisho mbele ya jeneza lenye mwili wa mwanasiasa mkongwe nchini, marehemu Ibrahim Kaduma katika Kanisa la KKKT, Makongo Juu, jijini Dar es Salaam jana. Wa tatu kulia ni Askofu wa Kanisa hilo, Dayosisi ya Mashariki na Pwani, Dk. Alex Malasusa. **PICHA: JOHN BADI**

## Mkapa amsifu Kaduma uzalendo

UKURASA 3

# Ma-DC wamsindikiza mrithi wa Lissu bungeni

*WAMO wapambe 244, Chadema wasusa, Mlinga akalia kiti cha Mbowe...*Endelea ukurasa wa 2*

**MICHEZO** ZAHERA AGOMA KUIVAA MBAO, TFF YAMFUNGIA UK.32

**MAONI, KATUNI UK.6**

## Pacha mmoja waliotenganishwa Saudia afariki dunia Muhimbili

**Na Mary Geofrey**

MMOJA wa watoto pacha, waliokuwa wameungana maeneo ya kifuani hadi kwenye nyonga na kutenganishwa nchini Saudia Arabia, amefariki dunia.

Aliyefariki dunia ni Asnisia Benard, wakati akiendelea kupatiwa matibabu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) kutokana na kukutwa na tatizo kwenye utumbo.

Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Upasuaji (MNH), Dk. Sufiani Baruani, akizungumza na waandishi wa habari jana, alisema mtoto huyo alifariki dunia usiku wa kuamkia jana wakati wa kuendelea kupatiwa matibabu.

Asnisia na Melnes Benard, walizaliwa Januari 28, mwaka jana na kufanikiwa kupelekwa Saudi Arabia kutengenishwa na kufanikiwa kurejeshwa nchini Ijumaa ya wiki iliyopita.

**MAISHA YA ASNISIA MNH**

Daktari Bingwa Mshauri Mwelekezi wa Upasuaji wa Watoto MNH, aliyekuwa akiwahudumia watoto hao, baada ya kurejea nchini, Dk. Petronila Ngiloi, alisema chanzo cha pacha huyo kupoteza maisha ni baada ya kutapika kwa muda mrefu na matatizo kwenye utumbo.

"Tangu walivyotoka safarini mmoja alionekana hakuwa na hali nzuri mmoja alikuwa akilia lakini mwingine alikuwa tu kimya na niliambiwa alianza kutapika akiwa kwenye ndege na tulivyotoka uwanja wa ndege tulikwenda moja kwa moja hospitali kumfanyia uchunguzi kwanza," Dk. Ngiloi alisema.

Alisema kuwa wakati wakiendelea na uchunguzi alianza kutapika na kupandisha homa hali iliyomfanya apoteze maji na madini hivyo walilazimika kumuwekea dripu za maji.

"Baada ya vipimo kutoka vilionyesha kulikuwa na hitilafu kwenye utumbo ulikuwa umejikunja, tulimfanyia upasuaji lakini hali iliendelea kuwa mbaya na baadaye kupoteza maisha akiwa chumba cha uangalizi maalum (ICU)," Dk. Ngiloi alisema.

Dk. Ngiloi alisema pacha mwingine hali yake inaendelea vizuri na hana tatizo lolote.

Alisema walipanga kuwasafirisha kuwarudisha mkoani Kagera Septemba 6, mwaka huu lakini wanatarajia kuwasifirisha kesho ili kuwahi kumzika mtoto huyo nyumbani kwao. Pacha hao Anisia na Melnes, walizaliwa wilayani Misenyi mkoani Kagera na kupelekwa nchini Saudi Arabia kwa ajili ya kutenganishwa kazi iliyofanikiwa na kurudishwa nchini.

Kutokana na kufanyiwa upasuaji huo, waliondolewa mguu mmoja ambao ulikuwa wanawafanya wawe na mitatu na kuwaacha na mguu mmoja kila mmoja.

# Kontena 700 zilizokwepa ushuru kaa la moto serikalini

**Na Romana Mallya**

KONTENA 700 zinazodaiwa kuingizwa nchini bila kulipiwa kodi, zimekuwa kama kaa la moto kutokana na mamlaka mbalimbali za serikali kujiweka kando kuliweka wazi.

Kila mamlaka ilipoulizwa na Nipashe kuombwa ufafanuzi kuhusiana na kontena hizo zinazodaiwa kuingizwa na kiongozi mwandamizi nchini haikuwa tayari kutoa maelezo.

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), imesema madai yaliyoibuliwa na Katibu wa Itikadi na Uenezi Chama Cha Mapinduzi (CCM), Humphrey Polepole, kuhusu kiongozi huyo mkubwa nchini kukwepa kodi baada ya kuingiza mzigo wa kontena hizo bandarini wao hawawezi kuyazungumzia.

Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipakodi TRA, Richard Kayombo, alipoulizwa jana na Nipashe kwa njia ya simu kuhusu kontena hizo, alisema mamlaka haiwezi kuyazungumzia kwa sababu yawezekana ni taarifa za ndani.

"Yawezekana hizi ni taarifa za ndani ndiyo maana Polepole hakutaja jina wala kampuni husika. Kwa sasa hatuwezi kuzungumzia chochote kuhusu hizo kontena na sisi tumeona taarifa kwenye gazeti," alisema.

Juzi, Nipashe ilichapisha habari ambayo Polepole Jumamosi iliyopita akiwa kwenye kongamano la umuhimu wa amani na mapambano dhidi ya rushwa kuelekea Uchaguzi Mkuu, alisema kiongozi huyo (jina hakulitaja) alikuwa na kontena 700 bandarini amekwepa kodi.

Akizungumza kwenye kongamano hilo, Polepole alisema "Yupo kiongozi mmoja mkubwa sana Tanzania sitamsema hata Takukuru wanamfahamu, ila mniwie radhi sitamtaja jina, alikuwa na kontena 700 bandarini amekwepa kodi.

"Kila kontena moja lilikuwa na futi 40, huyu kiongozi alitaka Rais amsaidie, lakini Rais Magufuli alimwambia lipa kodi uende zako. Huyu kiongozi mpaka sasa amenuna," alidai.

"Hivi ninavyoonea mpaka sasa amenuna. Rais Magufuli kazi yake ni kushughulika na watu walionuna. Siku zote ukisimamia haki hupendwi. Mtume alisimamia haki hakupendwa, Yesu alisimamia haki Wayahudi wakamuua, Ayubu alisimamia akapoteza kila kitu hadi familia yake."

Polepole alidai hakuna mtu anayesimamia haki ambaye ameishi maisha ya starehe bali huishi kwa imani.

Kongamano hilo liliandaliwa na Jumuiya ya Waislamu wa Shia Tanzania na kuhudhuriwa na viongozi wa vyama vya siasa, chama tawala na vyama vya upinzani, viongozi wa dini na wadau wengine.

Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwelwe, alipotafutwa kuzungumzia suala hilo la kontena 700 kama wizara yake inafahamu alisema ndio kwanza analisikia kutoka kwa mwandishi na kuomba aulizwe Waziri wa Wizara ya Fedha na Mipango ili kujua ni la kweli au la na kama alilipa kodi.

Gazeti hili lilimtafuta Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano serikalini, Wizara ya Fedha na Mipango ambaye pia ni Msemaji wa wizara hiyo, Benny Mwaipaja, ambaye alisema suala hilo halipo wizarani hapo.

"Suala hili halipo wizarani, ni la TRA labda ujaribu huko kutafuta majibu," alisema.



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda (kulia), akimkabidhi Waziri wa Katiba na Sheria, Balozi Dk. Augustino Mahiga, maombi ya mabadiliko ya Sheria ya Ndoa na Mirathi, jijini Dodoma jana, yaliyotolewa na wajane wa mkoa huo. Katikati ni Mwenyekiti wa Chama cha Wajane Tanzania (TAWIA), Rose Sarwatt. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Ma-DC watatu wamsindikiza mrithi Tundu Lissu bungeni

**Na Sanula Athanas, DODOMA**

MIRAJI Mtaturu ameapishwa kuwa Mbunge wa Singida Mashariki (CCM), ikiwa ni takribani saa 12 tangu Mahakama Kuu ibariki kuapishwa, huku wabunge wa Chadema wakisusa kushiriki kiapo chake.

Mtaturu aliwasili bungeni jijini Dodoma jana, asubuhi, akisindikizwa na wapambe 244 kutoka jimboni, ikiwamo Kamati ya Siasa ya Mkoa wa Singida na Wakuu wa Wilaya za Ikungi, Manyoni na Singida Mjini.

Mbunge huyo mpya aliingia kwenye ukumbi wa Bunge majira ya saa 3:05 asubuhi mara tu baada ya wimbo wa Taifa kuashiria kuanza kwa mkutano wa 16 wa Bunge la 11, akisindikizwa na baadhi ya wabunge wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kisha kula kiapo cha uaminifu mbele ya Spika Job Ndugai.

Wakati mbunge huyo akiingia ukumbini, wabunge wote wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), hawakuwamo ukumbini, ikiwa ni ishara ya kususa kushiriki kiapo cha mbunge huyo. Kulikuwa na wabunge wachache wa Chama cha Wananchi (CUF) wakati wa kiapo hicho.

Mtaturu alitangazwa mshindi wa kiti cha ubunge wa Singida Mashariki (CCM) baada ya wagombea kutoka vyama vya upinzani kutorudisha fomu za kuwania ubunge wakati wa mchakato wa uchaguzi mdogo wa jimbo hilo.

Kiti cha ubunge wa jimbo hilo, kilitangazwa kuwa wazi na Spika Ndugai Juni 28, mwaka huu, akieleza kuwa aliyekuwa Mbunge wa jimbo hilo, Tundu Lissu (Chadema), amepoteza nafasi ya kuendelea kuwa mbunge kutokana na utoro bungeni na kushindwa kujaza fomu za tamko la mali na madeni.

Hata hivyo, Lissu kupitia kaka yake, Alute Mughwai, alifungua kesi Mahakama Kuu kupinga uamuzi huo. Katika kesi hiyo, Lissu aliiomba mahakama kuzuia Mtaturu kuapishwa bungeni na kubatilisha uamuzi wa kuvuliwa ubunge.

Juzi usiku, Mahakama Kuu iliruhusu Mtaturu kula kiapo bungeni huku ikitarajia kutoa uamuzi wake kuhusu maombi ya Lissu, Agosti 9, mwaka huu.

Lissu yuko Ubelgiji akiendelea na matibabu ya kibingwa baada ya kushambuliwa kwa kupigwa risasi na watu wasiojulikana wakati akijiandaa kushuka kwenye gari nyumbani kwake Area D mjini Dodoma Septemba 7, 2017.

**AULIZA SWALI**

Mtaturu alipata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza wakati wa kipindi cha 'Maswali', akihoji sababu za serikali kutotoa Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya mradi wa kuchimba visima na kama serikali iko tayari kutoa Sh. bilioni mbili ili kutengeneza miundombinu ya jimbo lake kwa kuwa tathmini ilishafanyika.

Kutokana na swali hilo, Spika Ndugai aliitaka Wizara ya Maji kuhakikisha tatizo la maji katika Jimbo la Singida Mashariki linatatuliwa.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, alisema: "Kwa kuwa Mtaturu ni jembe, wembe kutokana na kazi kubwa alizofanya, wananchi wa Jimbo la Singida Mashariki, wamtumie vizuri. Serikali itatua tatizo hilo."

Katika swali la msingi, Mbunge wa Mikumi, Joseph Haule 'Prof. Jay' (Chadema), aliitaka serikali kulieleza Bunge hatua inazochukua kuhakikisha inatatua changamoto ya upatikanaji wa maji jimboni kwake.

## HABARI KITAIFA

# Mkapa amsifu Kaduma kwa uzalendo, uadilifu

**Na Waandishi Wetu**

RAIS wa Awamu ya Tatu, Benjamin Mkapa, ameelezea kushtushwa na kifo cha mwanasiasa mkongwe Ibrahim Kaduma, huku akimmwagia sifa kuwa alikuwa mpenda haki na mzalendo wa kweli.

Akizungumza jana wakati wa ibada ya kuuaga mwili wa mwanasiasa huyo uliyofanyika katika Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Usharika wa Makongo jijini Dar es Salaam, Mkapa alisema hakupata taarifa juu ya ugonjwa wa Kaduma bali alipata habari kuwa amefariki dunia.

"Sikujua kama Kaduma alikwenda India kwa matibabu bali nilishtushwa na taarifa za kifo chake. Pamoja na hayo niseme taifa limepoteza hazina muhimu kwani alijitoa kwa moyo wake katika utumishi wake na kila nafasi aliyopewa kuiongoza.

"Nilimfahamu Kaduma tangu alipokuwa Hazina akiwa Mkurugenzi wa Fedha za Nje kwani tulikuwa tunaonana katika masuala ya kazi. Lakini sifa kubwa aliyokuwa nayo ni uaminifu, upendo na uzalendo. Aliwapenda watu wote na alitenda haki bila kujali dini, rangi wala kabila," alisema.

Mbali na sifa hizo, Mkapa alisema Kaduma alikuwa mkweli na mtu mwenye kusimamia kile anachokiamini na alipenda kujifunza kutoka kwa watu na hiyo ilimsaidia kuyafahamu mambo mengi.

Pia alisema mwanasiasa huyo ambaye aliwahi kuwa Waziri katika serikali ya awamu ya kwanza chini ya Mwalimu Julius Nyerere, alikuwa mkweli kwa wakubwa na wadogo na hata alipohojiwa hakuona shida kusimamia ukweli hata kama hautamfurahisha mtu mwingine.

"Alikuwa mtu mwadilifu ndiyo maana hata katika utumishi kwenye nafasi mbalimbali na hata taasisi alizoziongoza, alifanya mambo kwa uadilifu na kutenda haki bila kumwonea mtu yeyote," alisema.

Naye Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Prof. William Anangisye, alisema Kaduma atakumbukwa kwa mambo mengi na jumuiya ya chuo hicho kutokana na mchango wake alioutoa.

Alisema miongoni mwa mambo aliyoyafanya ambayo yatamfanya akumbukwe ni kuanzisha Taasisi ya Taaluma za Maendeleo (IDS) ambayo alikuwa mkurugenzi wa kwanza na baadaye Makamu Mkuu wa UDSM mwaka 1977 hadi 1980.

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mzumbe, Prof. Lughano Kusiluka, alisema enzi za uhai wake akiwa Mkuu wa Chuo hicho, Balozi Kaduma alianzisha kampasi mbili za chuo hicho za Mbeya na Dar es Salaam ambazo zimekuwa zikitoa kozi mbalimbali kama zile zinazotolewa katika kampasi Kuu ya Chuo hicho mkoani Morogoro.

Akihubiri katika ibada hiyo, Askofu Charles Salala wa Kanisa la Africa Inland Church (AICT) Dayosisi ya Dar es Salaam na Pwani, alisema wanadamu wanapaswa kutenda haki na kumpendeza Mwenyezi Mungu katika maisha yao kama alivyofanya Kaduma.

Ibada ya kuuaga mwili wa Kaduma, iliyoongozwa na Askofu wa KKKT Dayosisi ya Mashariki na Pwani, Dk. Alex Malasusa, ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali akiwamo Waziri Mkuu mstaafu, Edward Lowassa.

Balozi Ibrahimu Kaduma alifariki Agosti 31, mwaka huu, nchini India, na anatarajiwa kuzikwa mkoani Njombe Septemba kesho.

## TMA yatahadharisha mvua kubwa kwa Kanda ya Ziwa

**Faustine Feliciane na Mariam Magili**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), imetoa utabiri wa mvua za vuli huku wakitoa tahadhari kwa Mikoa ya Kanda ya Ziwa ambayo inatarajiwa kupata mvua nyingi.

Mkurugenzi Mkuu wa (TMA), Dk. Agnes Kijazi, alisema mikoa ya Kaskazini mwa Tanzania (Arusha, Kilimanjaro na Manyara) ambazo mvua zake zinatarajiwa kuanza mwishoni mwa mwezi wa Oktoba, itarajiwa kuwa na mvua kidogo (chini ya wastani) sawa na ukanda wa Pwani ya Kaskazini mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Tanga, Pemba na Unguja na sehemu ya mkoa wa Morogoro ambayo itakuwa na uhaba wa mvua.

Kwa Kanda ya Ziwa, kunakotarajiwa kuwa na mvua kubwa, mvua hizo zitaanza wiki ya pili ya Oktoba ingawa kwa baadhi ya mkoa wa Kagera mvua zimeanza kunyesha mwezi huu.

"Sasa katika Mikoa ile itakayopata mvua za wastani na chini ya wastani kwa maana ya mvua ndogo kutakuwa na upungufu wa unyevunyevu kwenye ardhi, hivyo kupelekea kuwa na upungufu wa maji na malisho ya mifugo, na huenda kukatokea na migogori kati ya wafugaji na wakulima," alisema.

Dk. Kijazi alisema kwa upande wa sekta ya uvuvi katika maeneo hayo inaweza kuathiriwa kutokana na upungufu wa maji katika mabwawa ya samaki, hivyo wafugaji wanashauriwa kuimarisha miundombinu ya ufugaji na kuzingatia matumizi sahihi ya maji.

"Kwa maeneo ambayo yatapata mvua za wastani mpaka juu ya wastani katika mikoa ya Kanda ya Ziwa, shughuli za kawaida za kilimo zinatarajiwa, malisho na maji ya kutosha kwa ajili ya mifugo na wanyamapori yanatarajiwa," alisema Kijazi.

TMA imtoa tahadhari ya kuwapo magonjwa ya mlipuko kwa mikoa ya Kanda ya Ziwa kutokana na mvua nyingi zitakazonyesha na pia huduma za majisafi na majitaka zitaathirika, hivyo kuzitaka mamlaka husika kuchukua tahadhari na kuimarisha miundombinu.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA
TASAC

TANGAZO

UTARATIBU WA WATEJA KUTOA MAONI USHAURI AU MALALAMIKO KWA HUDUMA ZINAZOTOLEWA NA SHIRIKA

SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA (TASAC) LILIANZISHWA KWA MUJIBU WA SHERIA YA UWAKALA WA MELI TANZANIA NA. 14 YA MWAKA 2017 NA KUANZA KUTEKELEZA MAJUKUMU YAKE KUANZIA TAREHE 23 FEBRUARI, 2018. SHIRIKA LIMEKUWA LIKITOA HUDUMA YA KUSIMAMIA BIASHARA YA HUDUMA ZA MELI, UHAKIKI WA SHEHENA, UONDOSHAJI WA SHEHENA NA MIZIGO BANDARINI. SHIRIKA LINASIMAMIA PIA UTEKELEZAJI WA MIKATABA YA KIMATAIFA YA SHIRIKA LA BAHARI DUNIANI "INTERNATIONAL MARITIME ORGANIZATION" (IMO) ILIYORIDHIWA NA SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.

SHIRIKA LINAPENDA KUWATANGAZIA WATEJA WAKE WOTE KUTOA MAONI, USHAURI AU MALALAMIKO KUPITIA TOVUTI YA SHIRIKA www.tasac.go.tz , BARUA PEPE info@tasac.go.tz NA customerservices@tasac.go.tz AU PIGA SIMU YA BURE, NAMBA 0800 110 101/0800 110 107 NA KUPITIA MASANDUKU YA MAONI YALIYO KATIKA OFISI ZA TASAC MAKAO MAKUU NA MIKOANI.

IMETOLEWA NA:

MKURUGENZI MKUU

SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA (TASAC)

215401802

# Sababu 8 Bunge kumpongeza JPM

**Na Sanula Athanas, DODOMA**

BUNGE limepitisha azimio la kumpongeza Rais John Magufuli kwa kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), huku likitaja sababu nane za kumpongeza.

Akisoma azimio hilo bungeni jijini Dodoma jana, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mussa Zungu, alisema limetolewa chini ya Kanuni ya 54 ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari 2016.

Zungu alisema kuwa tangu Rais Magufuli aingie madarakani, mataifa mengi yamekuwa yakipendezwa na uongozi wake na viongozi wa nchi za SADC wanatambua na kuthamini uongozi wake bora.

Alisema kwa kutambua hilo, Bunge la 11 katika mkutano wake ulioanza jana, linaazimia kumpongeza Rais Magufuli kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa SADC. Alisema chombo hicho cha kutunga sheria pia kinampongeza Rais Magufuli kwa kuwashawishi marais wote wa nchi 16 zinazounda SADC kukubali Kiswahili kiwe moja ya lugha rasmi zitakazotumika katika shughuli mbalimbali za jumuiya hiyo.

Zungu alisema Bunge pia linampongeza kwa dhati Rais Magufuli kwa kusimamia maandalizi mazuri yaliyofanikisha kwa ufanisi mkubwa uendeshaji wa mkutano wa 39 wa SADC. Alisema maandalizi hayo yalihusisha usafiri wa ndani, malazi na usalama wa wageni wote hususan marais wa nchi za jumuiya hiyo.

Mbunge huyo wa Ilala (CCM) pia alisema Bunge linampongeza kwa dhati Rais Magufuli kwa kusimamia uratibu na kuendesha vyema vikao vyote katika Mkutano wa Marais wa nchi za SADC.

Alisema Bunge pia linampongeza Rais Magufuli kwa kuwezesha na kuratibu utiaji saini wa itifaki zenye maslahi kwa nchi za SADC.

Zungu alisema Bunge linampongeza Rais Magufuli kwa kutoa wito kwa nchi wanachama kuimarisha viwanda vyake ili kuzalisha bidhaa ambazo watashirikiana katika kununua na kuuza ndani ya nchi za SADC badala ya kuagiza kutoka nje.

Alisema Bunge pia linampongeza Rais Magufuli kwa kuitaka serikali kuweka mazingira ili Watanzania wengi waweze kutumia fursa zinazoweza kupatikana kutoka nchi za SADC.

"Bunge pia linampongeza kwa dhati Rais Magufuli kwa kuitaka serikali kuanzisha kitengo maalum kitakachokuwa kinatoa taarifa za mara kwa mara kuhusu fursa zinazopatikana katika nchi za SADC," Zungu alisema.



Takataka zikiwa zimetelekezwa bila kuzolewa kwa muda mrefu katika kituo cha daladala cha Mwenge, jijini Dar es Salaam jana na kusababisha usumbufu pia kuhatarisha afya za abiria kituoni hapo. **PICHA: MIRAJI MSALA**






# Auawa tuhuma za kuiba tochi

**Na Hamisi Nasiri, MASASI**

HASSANI Mangochi mkazi wa Mtaa wa Wapiwapi Kata ya Napupa wilayani Masasi mkoani Mtwara (35), ameuawa na wananchi wenye hasira kali kwa kupigwa kwa mapanga, marungu na mawe kwa tuhuma za kuiba tochi.

Tochi hiyo inadaiwa ni ya kutumia umeme wa jua (solar) yenye thamani ya Sh. 49,000.

Mmoja wa ofisa wa Jeshi la Polisi mkoani Mtwara ambaye hata hivyo hakutaka jina lake liandikwe gazetini kwa kuwa sio msemaji wa suala hilo, alisema tukio hilo lilitokea juzi saa 5:30 asubuhi katika kijiji cha Mwenge Mtapika Kata ya Mwenge Mtapika mjini Masasi.

Alisema Mangichi alikutwa na mauti baada ya kufika katika kijiji hicho na kudaiwa kutaka kuiba tochi ambayo inatumia umeme wa jua mali ya Asha Selemani, mkazi wa Mwenge, na kwamba tochi hiyo ilikuwa imeanikwa nje ya nyumba ya mama huyo.

Alisema marehemu wakati akijaribu kufanya kitendo hicho cha wizi ndipo baadhi ya wananchi walipomgundua, kisha wananchi wenye hasira kali walipomkamata na kuanza kumpiga kwa kutumia silaha hizo na kumsababishia majeraha makubwa sehemu mbalimbali za mwili wake.

Aliongeza kuwa baada ya kupata majeraha hayo yaliyotokana na kipigo hicho kutoka kwa wananchi, alitokwa na damu nyingi mwilini na baadaye alifariki dunia.

Alisema mwili wake umeshachukuliwa na ndugu zake kwa ajili ya kwenda kufanya taratibu za maziko.

"Jeshi la Polisi mkoani Mtwara tunatoa wito kwa wananchi kuacha kuchukua sheria mkononi badala yake wafuate kanuni na sheria za nchi na kwamba tutawasaka wote waliohusika na kitendo hiki cha kuchukua sheria mkononi na kisha tutawafikisha kwenye mkondo wa sheria," alisema ofisa huyo.

Menyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Mwenge, Yohana Omari, alisema alipata taarifa ya kukamatwa mtu huyo na kwamba wananchi walimvamia na kuanza kumpiga.

Alisema kabla ya wananchi hao kumuua walianza kumvunja miguu yote kwa kutumia silaha hizo na kumsababishia majeraha hayo ambayo yalimpelekea kifo chake.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mtwara, Blasius Chatanda, alipotafutwa na gazeti hili kuelezea tikio hilo pamoja na watu waliokamatwa, simu yake ilikuwa ikiita bila majibu.

# Hukumu rufani diwani aliyepiga trafiki yaiva

**Na Joctan Ngelly, KIGOMA**

MAHAKAMA ya Wilaya Mkoa wa Kigoma inatarajia kutoa hukumu ya rufani ya kesi inayomkabili Diwani wa Kata ya Mwanga Kaskazini, kupitia Chama cha ACT-Wazalendo, Clayton Revocatus (34), anayepinga hukumu ya kifungo cha miaka mitano iliyotolewa na Mahakama ya Mwanza Mwandiga, ya kosa la kumshambulia kwa kumpiga askari polisi wa kikosi cha usalama barabarani.

Hukumu hiyo inatarajiwa kutolewa Septemba 10, mwaka huu.

Mshtakiwa huyo alipandishwa kizimbani jana mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Eva Mushi, baada ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Kenneth Mtembei, ambaye anasikiliza kesi hiyo kutokuwapo mahakamani.

Upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Shabani Masanja, ulidai kuwa upande wa utetezi wa mshtakiwa huyo ulipeleka mahakamani sababu tano za rufani hiyo.

Ulitaja sababu ya kwanza kuwa ni kesi haikuthibitika kwa kiwango cha sheria, sababu ya pili Mahakama ya Mwanzo Mwandiga ilikosea kuwaruhusu washauri wa mahakama hiyo kuuliza maswali ya kuwachanganya mashahidi, sababu ya tatu ni Mahakama ya Mwanzo Mwandiga kumwingilia mshtakiwa wakati wa utetezi wake, sababu ya nne Mahakama ya Mwanzo Mwandiga kutokuwa na mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo na sababu ya tano ni mahakama hiyo kushindwa kuandika maoni ya washauri wa mahakama hiyo katika mwenendo mzima wa kesi.

Upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali Masanja, ukijibu hoja tano za rufani hiyo, ulidai sababu zao zote zilizozitolewa mahakamani hazina ukweli.

Baada ya pande zote kutoa hoja zao, Hakimu Mushi alimuuliza wakili wa kujitegemea Eliutha Kivyino, ambaye anamtetea mshtakiwa huyo kama kuna jambo la kuongeza tofauti na sababu tano alizopeleka mahakamani na wakili huyo alijibu kuwa hana jambo lingine la kuongeza na kuomba tarehe nyingine ya kutoa hukumu dhidi ya mteja wake.

Hakimu Mushi aliahirisha kesi hiyo hadi Septemba 10, mwaka huu, kwa ajili ya kutoa hukumu ya rufani hiyo.

Awali Mahakama ya Mwanzo Mwandiga, ilimhukumu Diwani Revocatus, maarufu Baba Revo kutumikia kifungo cha miezi mitano jela kwa kosa la kushambulia kwa kumpiga Askari Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani ngumi na makofi sehemu mbalimbali za mwili wake.

HABARI KITAIFA

## Malinzi: Fedha zote nilizozikopesha TFF nililipwa kihalali

**Na Hellen Mwango**



IKIWA ni siku ya nne ya utetezi wa Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), Jamal Malinzi, anayekabiliwa na kesi ya kughushi na kutakatisha fedha, amedai mahakamani kwamba fedha zote anazotuhumiwa kuzitakatisha alilikopesha shirikisho hilo na alilipwa kihalali.

Shahidi huyo wa kwanza wa utetezi alitoa utetezi huo juzi katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi, Maira Kasonde.

Akiongozwa na Wakili wa Utetezi, Richard Rweyongeza, Malinzi alidai kuwa Dola za Marekani 2400 alizolipwa na TFF ilikuwa ni malipo baada ya kuhudhuria mkutano wa FIFA nchini Mexico, Mei 16, 2016, kwamba wakati anakwenda katika mkutano huo alitumia fedha zake binafsi hivyo aliporudi nchini alilipwa fedha hizo na shirikisho hilo.

Kadhalika alidai kuwa Dola za Marekani 7,000 anazodaiwa kujipatia kwa njia ya udanganyifu, alilipwa kihalali na TFF, baada ya kuchukua fedha yake binafsi kumlipa kocha wa Timu ya Taifa ya Vijana maarufu kama Serengeti Boys.

Akifafanua katika ushahidi wake, Malinzi alidai hata Dola za Marekani 10,000 alizolipwa na TFF, alilipwa kihalali kwa sababu alilikopesha shirikisho hilo kuilipia Timu ya Taifa ya Vijana chini ya miaka 17 walikuwa wanacheza na timu ya vijana ya Misri na hiyo ilikuwa Juni 16, 2016.

"Nilikuwa natoa fedha zangu mfukoni kuwalipita wachezaji halafu baadaye fedha zikipatikana TFF inanilipa, hivyo niseme tu fedha hizo nilipewa kihalali na TFF na wala sikujipatia kwa njia ya udanganyifu kama jinsi shtaka la 26 linavyoeleza kuwa nilijipatia fedha hizo kwa njia ya udanganyifu," alidai.

Mshtakiwa huyo aliendelea kujitetea kuwa kuanzia mwaka 2014 hadi 2016, alikopesha TFF jumla ya Sh. milioni 320 kama sehemu ya familia ya shirikisho hilo.

"Mheshimiwa hakimu katika kipindi changu, walikuwapo watu mbalimbali ambao walikuwa wakiikopesha TFF, lakini mimi ndio rais wa kwanza ambaye nilikamatwa na kufikishwa mahakamani," alidai Malinzi.

Mbali na Malinzi washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Katibu Mkuu wa zamani, Selestine Mwesigwa, Mhasibu Nsiande Mwanga na Karani Flora Rauya.

Kesi ya msingi namba 213/ 2017 washtakiwa hao wanakabiliwa na mashtaka 20 yakiwamo ya kula njama, kughushi, kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na kutakatisha fedha Dola za Marekani 173,335.

# Mawakala ATCL wahukumiwa jela miaka 20

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, imewahukumu mawakala 12 wa Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) kulipa faini ya Sh. milioni moja kila mmoja au kwenda jela kutumikia kifungo cha miaka 20 baada ya kukiri kosa la kulisababishia shirika hilo hasara ya zaidi ya Sh. milioni 10.8.

Kadhalika, mahakama hiyo imewaamuru washtakiwa wote kulipa fidia ya Sh. 10,874,280 na mali zote walizozitumia katika kutekeleza tuhuma za kusababisha hasara hiyo ikiwamo simu 13 na kompyuta mpakato sita, zitaifishwe na kuwa mali ya serikali.

Hata hivyo, hadi Nipashe inaondoka mahakamani hapo juzi jioni, washtakiwa hao, walikuwa hawajalipa faini hiyo.

Hukumu hiyo ilisomwa juzi na Hakimu Mkazi Mwandamizi, Salum Ally, aliyepangiwa kusikiliza kesi hiyo.

Alisema baada ya washtakiwa kukiri makosa yao, mahakama yake imezingatia hoja zilizotolewa na pande zote mbili.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, aliwataja washtakiwa hao kuwa ni, Fabian Ishengoma, Adamu Kamara, Marlon Masubo, Alexander Malongo, Tunu Kiluvya, Jobu Mkumbwa, Mohamed Issa, Godfrey Mgomela, Absalom Nyusi, Janeth Lubega, Mary Semakweli na Janet Lubega.

Awali, kabla ya hukumu hiyo, Wankyo aliiomba mahakama itoe adhabu kali kwa washtakiwa ili iwe fundisho kwao na kwa wengine wenye tabia kama hiyo. Pia, aliiomba mahakama iamuru kampyuta mpakato na simu za mkononi zilizotumika katika kuisababishia serikali hasara zitaifishwe na serikali.

"Mheshimiwa hakimu pia naiomba mahakama hii kuwaamuru washtakiwa kulipa fidia ya hasara wanayotuhumiwa kuisababishia ATCL.

**"Mheshimiwa hakimu pia naiomba mahakama hii kuwaamuru washtakiwa kulipa fidia ya hasara wanayotuhumiwa kuisababishia ATCL.**

Katika utetezi kwa niaba ya washtakiwa, Wakili Benedict Inshabakaki, amedai washtakiwa hao ni wakosaji wa kwanza na kwa kuwa wamekiri mashtaka yao wenyewe wanaomba wapunguziwe adhabu kwa kuwa hawajaisumbua mahakama na vile vile ni vijana wadogo ambao wanafamilia zinazowategemea na pia ni nguvu kazi ya kesho.

Wakili Inshababakaki ameendelea kudai kuwa, wateja wake hao wamekaa ndani kwa zaidi zaidi ya miezi minane, hivyo watakuwa wamejifunza na wanajutia hivyo, tunaomba walipe faini na siyo kifungo gerezani.

Hakimu alisema mahakama yake imesikiliza hoja za pande zote mbili bila kuacha shaka na kuwatia hatiani kwa tuhuma zinazowakabili.

"Baada ya washtakiwa kukiri tuhuma zao ni wazi kwamba wameonyesha kujutia kitendo hicho cha kuisababishia hasara ATCL, mahakama yangu inamhukumu kila mshtakiwa kulipa faini ya Sh. milioni moja, mkishindwa mtakwenda jela miaka 20," alisema.

"Pia washtakiwa wote mnatakiwa kulipa fidia ya hasara hiyo kwa ATCL mahakama pia inaamuru zana zilizotumika katika kusababisha hasara ambazo ni, simu 13 na Laptop sita zitaifishwe kuwa mali ya serikali na kama washtakiwa hamjaridhika, rufani iko wazi," alisema Hakimu Ally.

Katika kesi hiyo washtakiwa hao walikuwa wanakabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi ikiwamo kuisababishia serikali hasara ya Sh. 10,874,280.

# Chuma chakavu kujadiliwa tena

**Na Jovin Lamwel, TUDARCO**

MIEZI mitano baada ya aliyekuwa Waziri Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), January Makamba, kuongoza kikao cha kukusanya maoni na matumizi ya taka hatarishi aina ya chuma chakavu na kutoa uamuzi wa kuruhusu biashara ya vyuma chakavu iliyokuwa imepigwa marufuku, kikao kingine kimeitishwa.

Katika kikao cha awali wadau walitoa maoni na kisha kuruhusiwa kuendelea na biashara hiyo wakati hatua za kutunga kanuni zikiendelea, hiyo ikitokana na malalamiko ya wadau kuzuiwa kuendelea na biashara hiyo kupata hasara.

Kwa mujibu wa tangazo lililotolewa na Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), wadau wa biashara hiyo wametakiwa kukutana leo jijini Dar es Salaam kujadili na kutafuta ufumbuzi wa changamoto ambazo zimeendelea kujitokezaa kwenye mfumo wa usimamizi na udhibiti wa taka hatarishi.

Tangazo hilo lilibainisha kuwa katika mkutano huo majadiliano yatajikita kwenye uhifadhi na utunzaji, ukusanyaji, usafirishaji, urejeeshi na uteketezaji wa taka hatarishi kwa mujibu wa rasimu hiyo kanuni na tozo na ada za mazingira za 2018.

Mkutano huo utaongozwa na Waziri wa Wizara hiyo, George Simbachawene, na kuwaleta pamoja wadau mbalimbali wa biashara hiyo.

Aprili, mwaka huu, Nemc ilitangaza kikao cha wadau ambacho baada ya kupokea maoni yao, aliyekuwa waziri alitoa uamuzi wa kuruhusu biashara ya vyuma chakavu wakati wakisubiri utengenezaji wa kanuni za sheria.

Katika kikao hicho, Makamba alisema serikali imesikia maoni ya wadau na katika kanuni zijazo watatenganisha ada za wakusanyaji, wasafirishaji, wauzaji na wenye viwanda kwa kuzingatia mporomoko wa bei za bidhaa mbalimbali.

Alisema katika kipindi cha mpito tutazunguka kuongea na watu mahusus wataangalia vibali na iwapo itabainika mtu hajakaguliwa na kupewa cheti cha tathimini ya mazingira (EAA) atafungiwa kufanya biashara hiyo na kutoruhusiwa kuomba leseni baada ya kanuni mpya.


SOMA GAZETI LAKO LA THE GUARDIAN NA NIPASHE POPOTE ULIPO KUPITIA

epaper.ippmedia.com

UTAPATA GAZETI LA THE GUARDIAN NA NIPASHE KWA URAHISI ZAIDI
UTAPATA HABARI MPYA KILA SIKU
UTAPATA TAARIFA ZA ZABUNI (TENDER) NA NAFASI ZA KAZI



Ingia kwenye GooglePlay au ios (Apple Store) kisha tafuta **The Guardian-IPP Media**

Superbrands · The Guardian · Google Play · App Store · Nipashe

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hili la moto mwendokasi ni changamoto uokoaji

**KUUNGUA** kwa basi la mwendo kasi juzi jijini Dar es Salaam kumeongeza hofu ya usalama ndani ya vyombo vya usafiri vya umma.

Woga unatokea kwa sababu hakuna usalama wa kutosha ndani ya vyombo vya usafiri wa umma licha ya kwamba ni muhimu kuliko chochote kile kwa vile usafiri huo hubeba idadi kubwa au abiria wengi kupindukia.

Hali inakuwa mbaya zaidi kwenye magari ya mwendo kasi ambayo licha ya kuwa na abiria wengi sana hakuna mifumo madhubuti ya kuwahakikishia usalama na hata ya kufanikisha uokoaji pale tatizo linapotokea.

Changamoto kubwa ni kwamba watu wengi hawafahamu jinsi ya kujiokoa iwapo ajali itatokea mbali na kufikiria kuwa wanaweza kuruka dirishani.

Pamoja na kukosa ufahamu wa jinsi ya kujiokoa abiria wengi hawana wazo kuhusu usalama wao na wengi hupanda kwenye magari bila kujali kuwa chochote kinaweza kutokea hasa gari kuwaka moto nao wakashindwa kuokoka.

Watanzania wengi hawajali wala kuwaza iwapo ajali itatokea watajiokoaje? Ndiyo maana wanapoingia kwenye gari hakuna anayejishughulisha kutafuta jinsi ya kujiokoa kama ajali inatokea.

Hata hivyo, tusilaumiane bali kuanzia sasa serikali na mamlaka ziimarishe miundombinu na mifumo ya kujiokoa ndani ya mabasi ya umma.

Tukiwageukia wasafirishaji wa mwendokasi, pengine tuwahoji hivi wana utaratibu gani wa kujiokoa?

Kubwa ni kwamba milango ya gari za mwendokasi hufunguliwa kwa mfumo wa umeme kazi inayofanywa na injini, hivyo iwapo ajali itatokea kwa sababu za hitilafu kwenye injini itakuwa vigumu kufungua milango hiyo.

Na kama kuna ajali iliyokwamisha injini inamaanisha kuwa uwezekano wa milango kufunguka ni mdogo hivyo majeruhi na vifo vinaweza kuwa vingi sana.

Kwa hiyo kazi ya kwanza ambayo magari ya mwendokasi yanatakiwa kuipatia majibu ni hiyo ya milango ya kujiokolea.

Suala jingine ni jinsi ya kushuka kwenye magari hayo ambayo mara nyingi yanategemea ukingo wa barabara za ndani ya vituo ili abiria kupanda na kutoka.

Swali letu ni hili , hivi iwapo tatizo litatokea nje ya kituo itakuwaje? Jambo hili nalo walitafakari itakuwaje kama gari litapata hitilafu ya moto njiani na wala si ndani ya kituo?

Je inawezekana kwa mabasi ya mwendokasi kuwa na milango ya kuokolewa watu ambayo itafunguliwa kwa nguvu za binadamu badala ya hiyo inayojiendesha yenyewe?

Vipi magari haya yana ngazi za kuokolewa watu iwapo ajali itatokea katika eneo ambalo si kituoni?

Ni vyema kufikiria suala hilo kwani milango ya magari hayo hata kama inafunguka iko juu kiasi kwamba ni vigumu abiria kushuka chini kwa haraka ili kujiokoa ajali inapotokea.

Ni eneo la kuchukua tahadhari kwa kuwa abiria wanaweza kukanyagana na kuumizana iwapo hakutakuwa na udhibiti kwenye eneo la kutoka mlangoni.


Tatizo jingine la magari haya ni kukosa madirisha makubwa yanayowezesha watu kujiokoa. Suala hilo nalo mamlaka ilitazame. Jambo jingine muhimu kwa magari haya ya mwendokasi ni kudhibiti idadi ya abiria.

Yanabeba watu wengi mno na ajali inapotokea inakuwa vigumu kuwaokoa hilo nalo ni jambo la kutafakari kuhusu idadi ya abiria wanaobanana kupindukia ndani ya magari hayo. Kwa hiyo tunachotaka kusema ni hiki, kampuni hii kwa kuzingatia kilichotokea Jumapili, itafakari upya mikakati na mifumo ya kuwaokoa abiria kwani si salama kuacha hali ikabaki kama ilivyo sasa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge

# Miji inaweza kutunza mazingira, wenzetu wameliweza kimsingi

Na Salome Kitomari

**MOJA** ya mambo ya kujifunza kutoka kwa wengine ni utunzaji wa mazingira katikati ya miji sambamba na maendeleo ya miundombinu.

Muungwana alipata fursa ya kutembelea Thailand hivi karibuni, nchi ambayo imepiga hatua kubwa kwenye miundombinu ya kisasa.

Ina mtandao wa barabara za kawaida, kulipia, treni za umeme na maeneo mengine ya watembea kwa miguu.

Licha ya kuwa na barabara kubwa zilizojengwa juu zenye kupitisha magari 16 kwa wakati mmoja yanayokwenda na kurudi, lakini utunzaji wa mazingira umepewa kipaumbele.

Lengo ni kuhakikisha kuna hifadhi ya mazingira inanyonya hewa chafu na kutoa hewa safi.

Katika Jiji la Bangkok, kuna makutano ya barabara yasiyohesabika yenye maumbo ya kila aina, yakiwa na barabara zilizojengwa juu ya ardhi, kila moja likiwa na kipaumbele cha utunzaji wa mazingira.

Thailand ni nchi iliyoendelea ikiwa na viwanda vingi na uchumi wake unategemea pia shughuli za kilimo na biashara, bila kusahau usafirishaji. Ni kitovu cha usafiri wa anga, barabara na maji.

Kwa uwekezaji wa miundombinu na majengo mengine mengi, ilikuwa ni vigumu sana kuona misitu au eneo lililohifadhiwa vizuri ili kuleta hali ya ukijani wa kutosha kwenye jiji la Bangkok, lakini imewezekana kutokana na kuwekwa kwenye vipaumbele vyao.

Muungwana alikaa katika jiji la Bangkok kwa siku nane na siku mbili katika eneo la Prachuap Khiri Khan, mwendo wa saa nne kutoka jijini Bangkok.

Kote huko alishuhudia jitihada za utunzaji mazingira kwa kuhakikisha uwekezaji wa miundombinu unakwenda sambamba na upandaji wa miti na utunzaji wa maeneo ya misitu midogo ndani ya miji hiyo.

Utunzaji wa mazingira ni muhimu kwa nyakati hizi ambazo kuna changamoto ya mabadiliko ya tabianchi.

Ni kwa mantiki hiyo Muungwana anaasa kwamba kasi ya ujenzi wa miundombinu inayoendelea jijini Dar es Salaam na maeneo mengine ya nchi, inapaswa kuhakikisha miti inayokatwa kupisha ujenzi inapandwa upya kwa ajili ya kutunza mwonekano maridhawa na mvuto kwa jiji na miji mingine.

Jiji la Dar es Salaam halina maeneo ya misitu na miti ya kutosha kwa ajili ya kunyonya hewa ukaa inayozalishwa na shughuli za kibinadamu, badala yake linategemea misitu ya Kisarawe ambayo nayo inavamiwa na shughuli za kibinadamu.

Kama wengine walivyoweza kutunza mazingira kadri maendeleo yanavyozidi kusonga mbele, ndivyo inavyopaswa Watanzania wafanye wakitambua umuhimu wa mazingira kwa afya zao na viumbe vingine kwa ujumla.

Unapotembelea Bangkok utaona maghorofa mengi yenye urefu tofauti lakini hatua chache utaona miti mingi ambayo inasaidia kutunza mazingira na wakati huo huo inaweka madhari nzuri.

Zipo bustani nyingi za kila aina kwenye barabara zote, hakuna barabara iliyojengwa bila kuwekwa bustani, na barabara za kwenda nje ya jiji katikati kuna miti mingi ambayo inasaidia kunyonya hewa ya ukaa inayotolewa na magari.

Ni la kuiga hata kwetu kwa mfano katika eneo la Kariakoo lililomea maghorofa mengi bila ya miti, hata kama kuna eneo linaloweza kupandwa mti husika.

Kuna maeneo kwa mfano katika jiji la Bangkok yaliyo na ardhi oevu lakini yametunzwa vyema, tofauti na maeneo yetu ambayo yamevamiwa na watu wamejenga kama ilivyo eneo la Jangwani, Kinondoni, Msasani na kwingine.

Inawezekana maeneo hayo kutunzwa kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho, kwa kuhimiza jamii husika kupanda miti.

Aidha, wenye maghorofa walazimishwe kupanda miti mingi nje ya maeneo yao, huku wasimamizi wa mazingira wakihakikisha hakuna uvamizi wa maeneo yanayohitaji kutunzwa kwa manufaa ya wote.

Uharibifu wa mazingira unaweza kufanywa na wachache, lakini madhara yake ni kwa jamii nzima na ndiyo maana ya mabadiliko ya tabianchi tunayoshuhudia, yaani ukosefu wa mvua, mafuriko, vimbunga na mengineyo.

## HABARI KITAIFA



Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Moshi (MUWSA), Joyce Msiru (kushoto) na watendaji wa MUWSA, wakipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi wa Uzalishaji na Usambazaji Maji (DAWASA), Mhandisi Aron Joseph (kulia), kuhusu namna maabara ya kupima na kusafisha maji inavyofanya kazi, wakati wa ziara kwenye mamlaka hiyo hivi karibuni. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Mchungaji, wake zake wapandishwa kizimbani

**Na Hellen Mwango**

MCHUNGAJI wa Kanisa la The Early Church of Lord Yeshwah, David Chirhuza (33) na wake zake wawili, wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam wakikabiliwa na tuhuma za kufanya kazi za kanisa bila kibali.

Mbali na Chirhuza washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Eather Sebuyange (27), Kendewa Ruth (26) ambao ni wake wa mchungaji huyo na Samwel Samy (22).

Mchunga kondoo huyo na wenzake walisomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Agustino Mbando.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na Waendesha Mashtaka wa Idara ya Uhamiaji, Godfley Ngwijo na Sita Shija.

Ngwijo alidai kuwa Septemba 2, mwaka huu eneo la Salasala Kilimahewa, jijini Dar es Salaam, mchungaji huyo na wenzake walikutwa wakiishi nchini bila kibali.

Katika shtaka la pili, ilidaiwa kuwa mchungaji huyo pekee alikutwa akijihusisha na kazi za kanisa akiwa hana kibali cha kuishi nchini.

Baada ya kusomewa mashtaka hayo, mchungaji David alikana shtaka la kwanza na kukiri shtaka la pili.

Pia washtakiwa wenzake wamekiri mashtaka ya kuingia nchini bila kibali.

Washtakiwa wote walirudishwa baada ya kushindwa kutimiza masharti ya dhamana likiwamo la kuwa na wadhamini wawili ambao ni watumishi wa serikali.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi Septemba 9, mwaka huu kwa ajili ya kutajwa.

# Watumiaji kuni watahadharishwa afya

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

NAIBU Waziri wa Nishati, Subira Mgalu amesema matumizi ya tungamotaka ikiwamo mafiga matatu husababisha madhara ya kiafya kutokana na kuvuta hewa chafu inayotokana na kuni na mkaa kwa watumiaji.

Mgalu alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti maalum (CCM), Shally Raymond.

Katika swali lake, Mbunge huyo alisema afya za wanawake wengi vijijini zinaathiriwa na moshi wa kuni wanapopika kwenye majiko ya mafiga matatu ambayo yanatumia kuni nyingi na hivyo kuchochea kasi ya ukataji miti.

"Serikali ina mpango gani wa kuondoa matumizi ya majiko ya mafiga matatu kote nchini?, Je, serikali ina mkakati gani wa haraka wa kuondoa majiko hayo kwenye shule zote za msingi na sekondari?" Alihoji.

Mgalu akijibu alisema matumizi ya tungamotaka husussan kuni na mkaa kama chanzo cha nishati ya kupikia hapa nchini yanakadiriwa kufikia asilimia 85.

Alisema kuwa pamoja na kuwa na madhara kiafya pia inasababisha uharibifu wa mazingira kutokana na ukataji wa miti.

Hata hivyo, alisema kupitia Sera ya Taifa ya Nishati ya mwaka 2015, serikali inahamasiha matumizi bora ya nishati ikiwamo teknolojia zinazopunguza gesi ya ukaa na matumizi makubwa ya kuni na mkaa kwa kutumia majiko banifu.

Alisema serikali imekuwa ikihamasisha kuacha matumizi ya nishati mbadala wa kuni na mkaa katika kupikia na gesi za mitungi, bayogesi, vitofali vya mabaki ya tungamotaka na majiko ya nishati jua.

Aliongeza kuwa Wakala wa Nishati Vijijini(REA) kupitia mfuko wa nishati vijijini pamoja na jukumu la usambazaji wa umeme vijijini inasaidia usambazaji wa teknolojia bora za kupikia husussan katika taasisi za umma nchi nzima zikiwamo shule, magereza, kambi za wakimbizi na zahanati.

# Waziri Mkuu aiomba Japan mafunzo madaktari bingwa

**Na Mwandishi Wetu**



WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameiomba Serikali ya Japan ikubali kutoa mafunzo zaidi kwa madaktari bingwa wa upasuaji na madaktari bingwa wa magonjwa ya figo na moyo kutoka Tanzania ili kukidhi mahitaji makubwa ya madaktari hao nchini.

Waziri Mkuu aliwasilisha ombi hilo juzi alipozungumza na Mshauri Maalum wa Masuala ya Afya wa Taasisi ya Tokushukai General Incorporated Association iliyo chini ya Serikali ya Japan, Akio Egawa, kwenye uwanja wa ndege wa Narita nchini Japan akiwa njiani kurejea nyumbani.

Waziri Mkuu alisema hivi sasa Tanzania ni kimbilio kwa nchi jirani katika tiba ya moyo na figo, hivyo madaktari bingwa wa upasuaji na madaktari bingwa wa magonjwa hayo wanahitajika sana.

Alisema baada ya hospitali ya Benjamini Mkapa ya Chuo Kikuu cha Dodoma kufanikiwa kupandikiza figo kwa wagonjwa saba chini ya ufadhili wa Taasisi hiyo, nchi jirani pia zinategemea kupata huduma hiyo nchini Tanzania, hivyo madaktari na vifaa tiba zaidi vinahitajika Ili kujenga uwezo wa kuwahudumia wagonjwa wa ndani na nje.

Majaliwa liishukuru Serikali ya Japan kupitia Taasisi hiyo kwa misaada yake ambayo kwa kiwango kikubwa imefanikisha kuanzishwa kwa tiba ya upandikizaji figo katika hospitali ya Benjamin Mkapa ya Chuo Kikuu cha Dodoma.

"Nashauri uandaliwe utaratibu wa kubadilishana watalaam ili Watanzania waende Japan kutibu wagonjwa na Wajapan waje nchini kufanya kazi kwenye hospitali zetu lengo likiwa ni kubadilishana ujuzi na kuongeza uzoefu."

Pia alimkaribisha nchini Egawa ili aweze kuona mwenyewe maeneo mengine ambayo Taasisi anayoiongoza inaweza kusaidia ili kuifanya nchi yetu kuwa na uwezo mkubwa katika tiba ya uapandikizaji wa figo Barani Afrika.

Kwa upande wake, Egawa alimwahidi Majaliwa kuwa Taasisi yake iko tayari kuunga mkono juhudi za Serikali ya Tanzania kwa kuendelea kusaidia hospitali ya Benjamin Mkapa ili kuiimarisha na kuiwezesha kufanya vizuri zaidi katika huduma ya tiba ya figo na moyo. Alisema taasisi yake iko tayari kuendelea kutoa ushirikiano na Serikali ya Tanzania.


## NOTISI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Sisi Adili Auction Mart Ltd Kwa idhini tuliyopewa na AMANA BANK LTD na mamlaka tulionayo kisheria tunatoa notisi ya siku 14 kuanzia siku ya tangazo hili kwa wadaiwa wote na wadhamini mlipe madeni yenu yote kinyume cha hapo tutauza kwa mnada wa hadhara dhamana ya mdaiwa wake. Mnada utafanyika mahali ilipo dhamana.

**MCHANGANUO WA DHAMANA ITAKAYOUZWA NA MAHALI ILIPO**

| NA | JINA LA MDAIWA/MDHAMINI | JINA LA MMILIKI | DHAMANA INAYOUZWA | MAHALI DHAMANA ILIKO | TAREHE YA MNADA NA MUDA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Z AND M (T) GENERAL TRADERS | ZAHRA SAID MWEMA | C.T No. 118524/13, L.O No. 455451 | Plot No. 192, Jangwani Beach Area Kinondoni Municipality | Tarehe 21.09.2019 Saa Nne (10:00 A.M) asubuhi na kuendelea |
| 2 | SAADA DAUD MTULUKU | SAADA BAKARI MTULUKU | C.T No. 481153, L.O No. 170792 | Plot No 1053, Block 'E' Buhongwa Area Mwanza City | Tarehe 21.09.2019 Saa Nne (10:00 A.M) asubuhi na kuendelea |

Adili Auction Mart Ltd Mawasiliano simu No 0687 571 118/0767 873 988

**MASHARTI YA MNADA**

1) Mnunuzi anatakiwa kulipia 25% ya bei ya mnada siku ya mnada na kiasi cha pesa kilichobaki atakilipa ndani ya siku 14, kinyume cha hapo kiasi kilichotolewa awali hakitarudishwa na mnada utarudiwa tena.
2) Ukaguzi wa dhamana utafanyika siku nne kabla ya mnada kuanzia saa Nne(10:00 A.M) asubuhi hadi saa Nane (02:00 P.M) mchana.
3) Gharama za kubadilisha hati miliki (transfer of ownership) na gharama nyingine zikiwemo usafiri ni za mnunuzi.
4) Dhamana itauzwa "kama ilivyo"



Meneja wa benki ya NMB Kanda ya Magharibi, Sospeter Magesse akizungumza wakati wa kongamano la wafanyabiashara wanachama wa klabu ya benki hiyo, mkoa wa Kigoma wikiendi, lililolenga kuwapa mafunzo na nidhamu ya biashara, lililofanyika Kasulu mjini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vijana 400 wachaguliwa kujiunga idara Uhamiaji

**Na Mwandishi Wetu**

JESHI la Kujenga Taifa (JKT), limetangaza orodha ya majina ya vijana 400 wa JKT Operesheni Kikwete na Operesheni Magufuli waliochaguliwa kujiunga na mafunzo ya Idara ya Uhamiaji.Taarifa iliyotolewa na JKT jana ilisema vijana hao wanatakiwa kuripoti katika Chuo cha Uongozi JKT kilichopo Kimbiji, jijini Dar es Salaam kuanzia Septemba 14 hadi Septemba 15, mwaka huu kwa kuanza mafunzo hayo. Taarifa hiyo ilisema uteuzi huo unafuatia usaili uliofanywa na Idara ya Uhamiaji mwezi Agosti, mwaka huu kwenye Kambi ya Mgulani JKT, jijini Dar es Salaam."Orodha kamili ya majina ya vijana waliochaguliwa na aina ya vifaa wanavyotakiwa kwenda navyo, inapatikana kwenye tovuti ya JKT ambayo ni www.jkt.go.tz." ilisema taarifa hiyo.

## Timu kuchunguza basi mwendokasi

**Na Gwamaka Alipipi**

SIKU mbili baada ya basi moja la mwendokasi kuwaka moto, timu ya uchunguzi kubaini chanzo cha ajali hiyo imeundwa.

Tukio la kuungua kwa gari hilo lilitokea Septemba Mosi usiku eneo la kituo kikuu Kimara Mwisho, lakini halikuleta madhara yoyote kwa abiria wala dereva.

Akizungumza na Nipashe, Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (Dart), Ronald Lwakatare, alisema kuna timu ya uchunguzi ambayo imeundwa kubaini chanzo cha tukio hilo.

"Linafanyiwa uchunguzi, siwezi kulitolea majibu ya moja kwa moja, ni timu ya wataalamu, imeundwa ikiwajumuisha LATRA na imeshaanza kazi," alisema Lwakatare.

Lwakatare alisema timu hiyo itakapokamilisha itatoa taarifa na wananchi wataweza kufahamu nini kilichosababisha gari hilo kuwaka moto.

Juzi Kamanda wa Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji Kinondoni, Jenifer Shirima, alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo akibainisha kuwa ni jambo la kushukuru kuwa hakukuwa na binadamu aliyejeruhiwa ama kusababishiwa kifo na moto huo.

Alieleza kuwa walipokea taarifa ya kuzuka kwa moto huo saa 2:02 usiku, na kwamba mtambo wao uliwasili eneo la tukio saa 2:15 ukiwa na maji lita 8,000 na kufanikiwa kuuzima.






# Kamwelwe aelezea changamoto sekta anga

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwelwe, amesema nchi nyingi barani Afrika ikiwamo Tanzania hazifanyi vizuri katika sekta ya usafiri wa anga.

Waziri Kamwelwe aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akifungua mkutano wa kimataifa wa Shirikisho la Huduma za Anga na Uongozaji Ndege (CANSO).

"CANSO kama sauti ya pamoja ya idara za uongozaji ndege duniani inatakiwa kuongeza usimamizi na ushirikiano kwa nchi wanachama katika kushughulikia changamoto zilizopo na zinazojitokeza," alisema.

Alisema Tanzania shughuli za udhibiti na uongozaji ndege zinafanyika kwa ufanisi mkubwa licha ya changamoto kadhaa, ikiwa ni pamoja na uhaba wa wataalamu, uchakavu miundombinu ya usafiri wa anga, udukuzi wa mifumo na mawasiliano ya anga, uhaba wa fedha na mabadiliko ya mara kwa mara ya teknolojia.

Alisema pamoja na changamoto hizo amepata taarifa kuwa kazi kubwa inafanyika na ufanisi uko bayana.

Alisema mafanikio ya CANSO yanadhihirishwa na uchache wa matukio ya ajali au matukio hatarishi ikiwamo ndege kupishana katika mazingira yasiyo salama.

"Kukua kwa mashirika ya ndege na ongezeko la abiria ni ishara tosha kuwa usafiri wa anga ni salama na unakua kwa kasi na hivyo kuongeza pato la taifa," alisema.

Pia, alisema takwimu zinaonyesha, usafiri wa anga ni moja ya sekta zinazokua kwa haraka sana duniani na hasa barani Afrika.

"Kwa mujibu wa takwimu hizo, idadi ya safari za ndege zinatarajia kuongezeka mara mbili, katika muda wa miaka kumi.

Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), Hamza Johari, alisema wanachokitaka ni upatikanaji wa mfumo mmoja ambao unatoa huduma bora na sio kila nchi kuwa na teknolojia yake katika masula ya usafiri wa anga.

**"CANSO kama sauti ya pamoja ya idara za uongozaji ndege duniani inatakiwa kuongeza usimamizi na ushirikiano kwa nchi wanachama katika kushughulikia changamoto zilizopo na zinazojitokeza," alisema.**

## HABARI MIKOANI

# Mwanza kujenga hospitali 2 za wilaya

**Na Anthony Gervas,** MWANZA

SERIKALI mkoani Mwanza inajenga hospitali mbili katika wilaya za Buchosa na Ilemela mkoani humo, zitakazogharimu Sh. bilioni tisa.

Akizungumza hivi karibuni katika hafla ya uzinduzi wa wodi za wagonjwa mashuhuri (Vip) na binafsi katika Hospitali ya Rufani Bugando, jijini Mwanza, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, alisema kuwa serikali mkoani Mwanza itaendelea kuunga mkono juhudi za uboreshaji wa huduma za afya nchini.

"Serikali mkoani Mwanza tunawajibika kuunga mkono juhudi za kuboresha huduma za afya nchini, sisi tunajenga hospitali mbili za wilaya, moja inajengwa Buchosa na nyingine inajengwa Ilemela ambazo zitakuwa mkombozi wa wananchi kupata huduma hiyo, alisema Mongella.

Aliwataka wananchi mkoani Mwanza, kujiunga na huduma ya bima ya afya ambayo itakuwa njia pekee na mkombozi kwao hasa wasiojiweza wakati wa kupata huduma za matibabu katika hospitali mbalimbali za serikali na binafsi.

Alisema uchumi wa Mkoa wa Mwanza umekuwa mkubwa, hivyo kuna haja ya kuimarisha sekta za afya, huku akisema asilimia 96 ya Hospitali ya Bugando ndiyo imekuwa mkombozi mkubwa wa huduma za afya kwa wananchi katika kanda hiyo kuliko taasisi zingine.

Alisema anataka Mkoa wa Mwanza uwe kitovu cha kimataifa cha utoaji wa huduma za afya yakiwa ni malengo ya serikali.



Dereva wa gari lenye namba za usajili T268 CAJ, akivunja sheria za usalama barabarani kwa kukatisha juu ya barabara ya mwendokasi na kugeuza alikotoka 'U-Turn', katika Mtaa wa Msimbazi, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JOHN BADI**

# Mkurugenzi OBC afutiwa kesi, ashtakiwa tena

**Na Mwandishi Wetu**

WALIMU wametakiwa kujifunza elimu ya kibenki ikiwamo mikopo, amana na huduma zingine zinazotolewa na benki mbalimbali ili iwasaidie kupania uwezo wao kiuchumi na kujenga tabia ya kujiwekea akiba.

Rai hiyo ilitolewa jana na Kaimu Katibu wa Chama cha walimu (CWT) mkoa wa Rukwa, Aurelia Mwanakulya, ambaye alikuwa mgeni rasmi alipokuwa akifungua warsha ya Siku ya Walimu ilioandaliwa na Benki ya NMB katika Mji wa Sumbawanga, mkoa wa Rukwa nakuhudhuriwa walimu wapatao 300.

"Mkijijengea tabia ya kujiwekea akiba na kutumia mikopo kwa busara hakika mtaweza kukidhi mahitaji yenu mbalimbali pindi yanapojitokeza," alisisitiza.

Kwa upande wa Benki ya NMB aliitaka taasisi hiyo ya kibenki kuzidi kubuni bidhaa zaidi, lakini pia kuhakikisha kuwa huduma hizo zinapatikana kwa unafuu, uharaka na ufanisi mkubwa.

"Ni lazima NMB ijue kuwa ushindani ni mkubwa katika sekta ya kifedha na ni wale tu watakaoweza kushindana na ubora unafuu na ufanisi ndio watakaodumu kwenye soko," alibainisha.

Kwa upande wake Meneja Mwandamizi NMB wa Amana za Wateja na Bima, Issac Mgawasa, alisema kwa sasa taasisi hiyo ya kifedha ina wateja zaidi ya milioni 3.2 kati ya hao milioni 2.5 wanatumia simu za mikononi kufanya miamala mbalimbali.

"Tuna imani kuwa miaka michache ijayo tutakuwa tunakuwa na jamii isiyotegemea matumizi ya fedha halisi," alisisitiza.

Nae Meneja NMB wa Biashara Kanda za Nyanda za Juu Kusini, Humphrey Kaaya, alisema kuwa taasisi hiyo itaanzisha programu ya matumizi bora ya mikopo kwa wateja wake.

Akifafanua, alisema kuwa programu hiyo itawanufaisha wateja wa NMB katika mikoa ya Rukwa, Mbeya, Iringa na Katavi.

Meneja wa NMB Tawi la Sumbawanga, Happiness Pimma, alisema kuwa benki hiyo ni ya pekee inayotoa mikopo mingi kwa watumishi wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa ambapo wengi wao ni walimu wakiwa pia wamefaidika na mikopo .

Wakichangia walimu kwa nyakati tofauti waliishukuru kutoa mikopo bila urasimu, huku wakiitaka ianze kutoa elimu ya ujasiriamali ili waweze kunufaika na mikopo hiyo, huku wakisisitiza kuwa wengi wao hawana elimu hiyo.

## Machifu waombwa kuachana na siasa

**Na Gurian Adolf, SUMBAWANGA**

KATIBU wa baraza la watemi wa makabila ya Wafipa mkoani Rukwa, Chelenganya Sikulumbwe, amewashauri machifu hao kutojihusisha na chama chochote cha siasa,badala yake wawe washauri wa wananchi katika changamoto zinazowakabili.

Ushauri huo aliutoa kwa watemi hao waliokutana wilayani Kalambo wakati wa sherehe za kumsimika mtemi Sapwe Nkongasimfukwe wa himaya ya Mambwe Nkoswe, zilizofanyika katika Kijiji cha Kalembe.

Alisema hivi karibuni utafanyika uchaguzi wa kuwapata viongozi wa serikali za mitaa, hivyo ni vvema viongozi wa kimila wasijihusishe na chama chochote cha kisiasa ili waendelee kuaminika na kuheshimika.

''Ninawaomba sana watemi wa makabila ya Wafipa kutojihusisha na chama chochote cha kisiasa kwani ninyi ni viongozi wa watu wote bila kujali itikadi ya kidini wala ya kisiasa kwa kufanya hivyo mtaendelea kulinda hadhi yenu na kuheshimika, lakini tofauti na hivyo hamtaaminika tena," alisema.

## Wanafunzi, mwalimu, mlinzi kortini tuhuma mauaji

**Na Lilian Lugakingira, BUKOBA**

WANAFUNZI wanne, mwalimu na mlinzi mmoja wa Shule ya Sekondari Katoro Islamic katika Wilaya ya Bukoba mkoani Kagera, wamefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Bukoba, wakikabiliwa na shtaka la kumuua Mud Muswadiku, aliyekuwa akisoma kidato cha nne katika shule hiyo.

Washtakiwa hao walifikishwa mbele ya hakimu wa mahakama hiyo Flora Kaijage Septemba 2, mwaka huu na hawakutakiwa kujibu chochote kutokana na mahakama hiyo kutokuwa na mamlaka ya kusikiliza kesi za mauaji.

Waliofikishwa mahakamani ni Badru Issa Tibagililwage (27) mlinzi, Majaliwa Abdul (35) mwalimu, na wanafunzi ni Husama Ramadhan (17), Sharif Huled (19), Hussein Mussa (20) na Abdalah Juma (19).

Mwendesha mashtaka wa serikali, Chema Maswi, alidai kuwa mauaji hayo yalitokea Aprili 14, mwaka huu na kuwa upelelezi unaendelea.

"Tumewasilisha mahakamani kesi namba 18 ya mwaka 2019 inayohusiana na mauaji ya mwanafunzi Mud Muswadiku, washtakiwa wako sita, lakini tunaendelea na upelelezi wa kesi ili kuhakikisha taarifa za kina zinapatikana," aliieleza mahakama.

# Madaktari bingwa wapya 365 kusambazwa kwenye uhaba

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

BUNGE limeelezwa kuwa jumla ya madaktari bingwa 365 wanaotarajiwa kuhitimu mafunzo yao kuanzia mwaka wa fedha 2019/20, 2020/21 na 2021/22 watasambazwa kwenye hospitali mbalimbali hususani maeneo yenye uhaba mkubwa.

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Sonia Magogo (CUF), ambaye alihoji serikali ina mkakati gani wa kuongeza madaktari bingwa nchini.

Akijibu, Dk. Ndugulile alisema katika mwaka 2017/18 wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo ilitenga kiasi cha Sh. bilioni mbili zilizotumika kwa ajili ya kusomesha madaktari bingwa 125 wa fani za kipaumbele katika chuo cha MUHAS ambao wanatarajiwa kumaliza 2020/21.

"Katika mwaka wa fedha 2018/19 serikali ilitenga kiasi cha Sh. milioni 1.8 ili kuendelea kugharamia mafunzo ya ngazi ya kibingwa katika kada mbalimbali za afya 127 katika chuo cha MUHAS," alisema.

Aidha, alisema hadi kufikia Juni mwaka 2019 jumla ya watumishi wa sekta ya afya 458 walikuwa wanaendelea na masomo katika ngazi mbalimbali za taaluma.

Hata hivyo, alisema katika idadi hiyo 435 wanaendelea na masomo yao ndani ya nchi na 23 nje ya nchi kwa ufadhili wa serikali na pia jumla ya madaktari bingwa 365 wanatarajiwa kuhitimu mafunzo yao kuanzia mwaka wa masomo 2019/20, 2020/21 na 2021/22.

Alisema wataalamu hao watasambazwa kwenye hospitali kulingana na uwiano wa wataalamu waliopo pamoja na kuzingatia maeneo yenye uhaba mkubwa.

"Katika mwaka 2019/20 wizara imetenga jumla ya Sh. bilioni 1.8 kwa ajili ya kugharamia mafunzo ya wataalamu bingwa katika fani za vipaumbele na kutokana na uhaba uliopo kwenye hospitali za rufani za mikoa, wizara itahakikisha fedha hiyo inatumika vyema katika kusomesha wataalamu wanaotoka kwenye maeneo yenye uhaba mkubwa," alisema.

Kadhalika, alisema wizara kupitia hospitali za rufani ngazi ya Taifa na taasisi za nje zitaendelea kuendesha kambi za udaktari bingwa hapa nchini kwa lengo la kusogeza huduma za kibingwa na kujenga uwezo wa wataalamu hao.



Katibu Msaidizi wa Chama cha Mabunge Jumuiya ya Madola (CPA), Kanda ya Afrika, Said Yakubu (kulia), akizungumza na Mwakilishi Maalum wa Spika wa Pakistan, Shandana Gulzar Khan, ambaye ni mgombea wa nafasi ya Uenyekiti wa Dunia wa Wabunge Wanawake wa Jumuiya ya Madola katika Mkutano wa Chama cha Mabunge Jumuiya ya Madola unaoendelea mjini Zanzibar jana. Shandana Gulzar Khan ni mmoja kati ya wageni maalum waalikwa katika mkutano huo. **PICHA: BUNGE**

# Busisi-Nyang'holongo kujengwa kwa awamu

SERIKALI imesema ahadi za viongozi wa nchi ikiwamo ahadi ya ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya kutoka Busisi hadi Nyang'holongo kuelekeza Kahama mjini itatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Hayo yalielezwa jana bungeni na Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Elias Kwandikwa, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Nyang'hwale(CCM), Hussein Amar.

Katika swali la mbunge huyo, alisema Rais wa awamu ya nne Jakaya Kikwete katika ziara yake wilayani Nyang'hwale akipoongozana na aliyekuwa Waziri wa Ujenzi, John Magufuli na Kassim Majaliwa alihidi wananchi ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami pamoja na kuondoa tatizo la mawasiliano ya simu.

"Je, ni lini ahadi hiyo ya viongozi wakuu wa nchi itatekelezwa kwa kujengwa barabara hiyo kwa kiwango cha lami,"alihoji.

Alihoji pia ni lini serikali itatimiza ahadi hizo kwa kujenga minara ya mawasiliano ya simu ili maeneo mengine ya Nyamtukuza, Kanegere, Nyugwa na maeneo mengine ili yaweze kusikika na kuchochea maendeleo ya nchi. Naibu Waziri Kwandikwa alisema wakati serikali ikiendelea kutafuta fedha, barabara hiyo itaendelea kufanyiwa matengenezo mbalimbali ili iweze kupitika majira yote ya mwaka.

"Kufuatia ahadi iliyotolewa na Rais wa awamu ya nne na utekelezaji wa sera za serikali, serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa wote iliainisha uhitaji wa mawasiliano katika Wilaya ya Nyan'hwale yakiwamo maeneo yaliyoahidiwa ili kutambua maeneo yote yenye uhitaji wa mawasiliano kwa ajili ya ufikishaji wa huduma hiyo," alisema.

Alisema kabla ya tathmini hiyo serikali ilikuwa imejenga mnara wa mawasiliano katika kata ya Shabaka mwaka 2013 yenye wakazi takribani 12,072 katika mradi uliotekelezwa na kampuni ya Vodacom.

## Mnada wa chai wanukia

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, amesema maandalizi ya mnada wa chai yanatarajiwa kukamilika Septemba 2019 ili kuwe na mnada utakaosaidia kupunguza gharama za usafirishaji wa chai nje ya nchi.

Bashungwa alitoa kauli hiyo alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Busekelo (CCM), Fredy Mwakibete, ambaye katika swlai lake alisema wananchi wa kata za Mpombo, Kandete, Isange na Luteba pamoja na kata za Kabula, Lwanga na Lupato wanalima zao la chai kwa wingi lakini bei ya zao iko chini.

"Je,ni lini serikali itatafuta soko la uhakika la zao la chai ambalo litasababisha kupanda kwa bei kuliko bei ya sasa ya Sh. 315 kwa kilo?" Alihoji.

Akijibu, Bashungwa alisema mnada huo pia utasaidia faida inayopatikana iongeze bei ya mkulima.

Alifafanua kuwa Bodi ya Chai Tanzania iliitisha kikao cha wadau wa chai kilichofanyika Aprili 2019 kutafuta ufumbuzi wa changamoto mbalimbali za wakulima ikiwa ni pamoja na kupanga bei elekezi ya chai kwa mwaka 2019 kwa kuwashirikisha wadau wote.

"Mkutano huo wa wadau wa zao la chai uliofanyika Aprili 3, mwaka 2019 Mufindi mkoani Iringa na wajumbe walipitisha bei elekezi ya majani mabichi ya chai kwa mwaka 2019 kuwa Sh. 315 kwa kilo," alisema.

Alieleza kuwa jitihada za serikali kutafuta masoko ya mazao ya kilimo nchini ni jukumu endelevu na kwa upande wa zao la chai jitihada zinafanyika ili kuhakikisha kuwa chai inayozalishwa inauzwa hapa hapa nchini bila kuwalazimu wakulima kusafirisha kwenda kwenye mnada Mombasa.

Alisema katika kutekeleza uanzishwaji wa mnada wa chai nchini kikosi kazi kiliundwa ambacho kinajumuisha Bodi ya Chai Tanzania (TBT), Soko la Bidhaa Tanzania (TMX), Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB), Chama cha Wakulima wa Chai Tanzania (TAT), Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara (TANTRADE), na Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai Tanzania (TSHTDA).

"Maandalizi ya mnada huo yanatarajiwa kukamilika Septemba 2019 ili tuwe na mnada wetu utakaosaidia kupunguza gharama za usafirishaji wa chai nje ya nchi."

# Baraza la Madiwani lamfagilia JPM

**Na Allan Isack, MBULU**

BARAZA la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu mkoani Manyara, limempongeza Rais John Magufuli, kwa kukamilisha ujenzi wa miradi ya maendeleo ikiwamo hospitali ya wilaya pamoja na jengo la utawala la makao makuu ya halmashauri hiyo.

Akizungumza katika mkutano wa baraza hilo, Mwenyekiti Joseph Mandoo, alisema wanampongeza Rais Magufuli kwa kufanikisha ujenzi wa miradi ya maendeleo.

Mandoo alisema, halmashauri ya Mbulu, imepiga hatua ya kimaendeleo kwenye sekta ya elimu, afya, utawala, miundombinu, kilimo na ufugaji.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, Hudson Kamoga, alisema kutokana na kutengwa kwa fedha hizo, halmashauri hiyo, imezidi kupiga hatua za kimaendeleo kupitia miradi mbalimbali inayoendelea kutekelezwa.

"Jengo la utawala la makao makuu linaendelea vizuri na hospitali nayo inajengwa katika kata ya Dongobesh, natarajia ujenzi huu utakamilika baada ya miaka mitano," alisema Kamoga.

Aliwaambia wanatarajia kutenga eneo la kumbukumbu ambalo litaandikwa majina ya madiwani waliokuwapo madarakani kipindi cha utekelezaji wa miradi hiyo, wakiongozwa na mwenyekiti wa halmashauri hiyo, na mkurugenzi mtendaji.

Mkuu wa Wilaya ya Mbulu, Chelestino Mofuga, alisema Rais Magufuli, amefanya maendeleo mengi kwenye wilaya hiyo, ikiwamo ujenzi wa miradi ya kimkakati ya muda mfupi ya kipindi cha miaka minne aliyoongoza tangu alipochanguliwa

"Tumeona barabara za ghorofa, elimu bila malipo, ujenzi wa reli ya kisasa, umeme, ujenzi wa hospitali mpya za wilaya zimejengwa vituo vya afya, utadhani ameongoza kwa miaka 40, kumbe ni miaka minne," alisema Mofuga.



Mkurugenzi wa Tiba wa Hospitali ya Rufani ya Kilutheri ya Haydom mkoani Manyara, Dk. Emmanuel Nuwass (kulia), akijadiliana jambo na madaktari wengine hospitalini hapo, jana, baada ya kupokea mashine ya uchunguzi ya mionzi (CT Scan), iliyogharimu Sh. milioni 800. **PICHA: GIFT THADE**

# Ziwa Manyara hatarini kutoweka

**Na Allan Isack, ARUSHA**

HIFADHI ya Ziwa Manyara mkoani Arusha, iko hatarini kutoweka baada ya kujaa matope, kutokana na wakulima na wafugaji wanaolizunguka kufanya shughuli zinazoingiza matope na taka ziwani.

Wakulima na wafugaji wanalima na kufuga pembezoni mwa ziwa hilo, na kusababisha udongo kuingia kwa wingi na kuchafua ziwa.

Hayo yalisemwa na Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Hifadhi ya Manyara, Noelia Myonga, wakati akitoa taarifa ya hifadhi ya ziwa hilo, kwa wataalamu na wanasayansi wa mazingira waliotembelea hifadhi hiyo, kwa lengo la kuangalia changamoto zinazoikabili.

Myonga alisema, wanakijiji wanaozunguka ziwa hilo, wanaofanya shughuli za kilimo zisizokuwa endelevu na wamesababisha kina cha ziwa hilo kuwa kifupi zaidi na maji kupungua.

Alisema kuna umuhimu mkubwa kwa wizara zinazohusika kuchukua hatua ya kutoa elimu kwa wananchi kuhusiana na umuhimu wa ziwa hilo kuendelea kuwapo.

Alisema hifadhi hiyo, kwa kushirikina na Shirika la Hifadhi za Taifa wametoa elimu ya matumizi bora ya ardhi kwa vijiji 25, ili kuwepo na matumizi sahihi ya ufugaji na kilimo chenye tija ambapo itasaidia kupunguza uharibifu wa mazingira ndani ya hifadhi hiyo.

Ofisa Mazingira wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Fredrik Mulimba, alisema baada ya kufanya ziara hiyo, wamebaini kuwa maji yanapungua kwa kiasi kikubwa kutokana na mabadiliko ya tabia ya nchi.

Aidha, alisema mamlaka husika inatakiwa kuwekeza nguvu nyingi katika hatua ya kutatua tatizo hizo kwa muda mwafaka ili kuilinda hifadhi hiyo, viumbe hai na wanyamapori wanaoishi katika eneo hilo.

"Kutokana na changamoto zinazoikabili hifadhi ya ziwa serikali inapaswa kuchukua hatua ili kulinda Hifadhi ya Ziwa Manyara na viumbe hai na wanyamapori wanaoishi katika eneo hilo," alisema Mulimba.

# Wanunuzi wakomeshwa kula rushwa za zabuni

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

ILI kupambana na kudhibiti rushwa kwenye manunuzi ya umma, serikali imewataka maofisa manunuzi na wa mifumo ya thamani kuacha ufisadi na kutumia taratibu mpya zinazozuia wizi kupitia sekta hiyo.

Aidha, maofisa hao wameaswa kuachana na rushwa ili kuisaidia serikali kufanya miradi ya maendeleo yenye tija na kutumia mfumo mpya wa manunuzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) ili kuisaidia serikali kufanikisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Onyo hilo, lilitolewa jana jijini Arusha na Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Gabriel Daqqaro, wakati akifungua mafunzo kwa watumishi wa umma 220, wa taasisi mbalimbali pamoja na maofisa Tehama, kutoka mikoa mbalimbali nchini yanayotolewa na PPRA.

Alisema ni vyema watumishi hao, kabla ya kupokea rushwa kuangalia bahasha za rushwa wanazopewa kama zinaendana na mafao yao watakapostaafu akimaanisha kuwa inaweza kuwa mwisho wa kazi na kupoteza hata hayo mafao wanayoyatarajia kwani rushwa ni mbaya na inaweza ikawasababishia matatizo katika maisha yao ya utumishi wa umma.

"Nasema hili sababu mfumo huu mkiutumia vyema ni suluhisho la kuhakikisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo, kwani wapo baadhi ya watumishi katika kada yenu wameishia mahakamani na wengine kufilisiwa mali zao sababu ya rushwa," alisema Daqqaro.

Alisema mfumo huo mpya unajulikana kwa jina la TANePS utasaidia kuondoa rushwa na kuleta ufanisi wenye tija katika manunuzi.

"Kwa mfumo huu yale magari ya kifahari mliokuwa mkinunua na kufanyia anasa nyingine mtaacha maana zamani dili zilikuwa nyingi sana ilikuwa muomba zabuni ili apate kazi lazima atoe bahasha kwanza, lakini sasa hivi mtaheshimiana, maana kila kitu kinafanyika kielektroniki," alisema Daqqaro.

Mhandisi Mtendaji Mkuu wa PPRA, Leonard Kapongo, alisema mfumo huo utasaidia kuepuka rushwa iliyosumbua kwa muda mrefu katika manunuzi.

Alisema mfumo huo, unaojulikana kama TANePS yaani Tanzania National e- Procurement System unapatikana katika anuani ya www.taneps.go.tz na unawezesha hatua mbalimbali za manunuzi kufanyika kuanzia utayarishaji wa mpango wa manunuzi hadi usimamizi wa mkataba. Kapongo alisema mfumo huo unakwenda kuonyesha uwazi katika ushindani wa manunuzi pia utasaidia kufanya tathmini katika mfumo huo na kuiwezesha serikali kupata thamani halisi ya manunuzi kupitia mtandao.

Alisema umewekwa ili kudhibiti wizi ili na kuiwezesha serikali kupata mapato sambamba na kudhibiti wazabuni kuzungumza kwenye korido kusubiri zabuni au kutoa fedha za rushwa kwa ajili ya kuhonga wapate kazi.

# Mpunga wanufaisha wakulima 300

**Na Godfrey Mushi, HAI**

ZAIDI ya wakulima 300 wa mpunga wanaoendesha shughuli za kilimo katika Skimu ya Mijongweni ya ukanda wa Kikavu Chini, Wilaya ya Hai, watanufaika na mradi wa kuzuia upotevu wa mpunga, baada ya mavuno kuongezewa mnyororo wa thamani.

Mradi huo maarufu kama skimu ya umwagiliaji ya Musa Mwijanga, ilianzishwa mwaka 1933.

Jana, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Yohana Sintoo, aliyasema hayo wakati akitoa taarifa ya maendeleo ya sekta ya umwagiliaji kwa kamati ya siasa ya CCM mkoa wa Kilimanjaro ilipozuru eneo hilo.

"Huu mradi ni mahususi kwa ajili ya kuwaunganisha wakulima, wasindikaji na wanunuzi kujikita zaidi katika kutetea jasho lao, kwa kuongeza thamani ya zao la mpunga. Serikali kuu, wahisani na mchango wa halmashauri yetu, tumeleta hapa Sh. 86,591,100.

Zaidi aliongeza: "Hizo ni kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa mashine ya kukoboa mpunga katika Kijiji cha Mijongweni, lakini lengo hasa la mradi huu ni kuongeza thamani ya zao la mpunga kwa kukoboa, kupanga mchele katika viwango na kufungasha kisasa."

Skimu hiyo ya umwagiliaji katika eneo la ukanda wa kikavu chini, ina jumla ya hekta 776, ambapo hekta 285 zinalimwa zao la mpunga.

Wakati hekta 140 zinalimwa zao la mahindi, hekta 81 zinalimwa zao la migomba na mboga na hekta 270 ni maeneo ya makazi ya watu na taasisi mbalimbali.

Kati ya mwaka 2013/2014 kijiji hicho kilipata ufadhili wa Benki ya Dunia (WB) wa kununuliwa mashine ya kisasa kwa ajili ya kukoboa mpunga, ambapo sharti la jumla lilikuwa ni wananchi kutoa eneo na kujenga jengo la kuweka mashine hiyo, jambo ambalo lilifanyika kwa mafanikio.

Alisema changamoto inayoukabili mradi huo ni ukosefu wa umeme mkubwa wa kufunga kwenye mashine ili mradi uanze kazi pamoja na kuwapo kwa miundombinu mibovu ya barabara itakayowezesha usafirishaji wa mazao kiurahisi.

Alisema kwa mwaka wa fedha 2019/2020 halmashauri imeidhinisha zaidi ya Sh. bilioni 1.331 kwa ajili ya matengenezo ya barabara zake kwa kiwango cha moramu, huku Sh. milioni 25 zikitengwa kwa ajili ya ukarabati wa barabara ya Shirinjoro - Mijengweni kwa kiwango cha moramu katika maeneo korofi.

Akipokea taarifa za mradi huo, Katibu wa CCM Mkoa wa Kilimanjaro, Jonathan Mabihya, alitoa wito kwa Shirika la Umeme mkoani hapa (Tanesco) kuhakikisha wanafikisha umeme mkubwa katika mradi huo ili kuruhusu kuanza kwa uzalishaji kama ulivyokusudiwa.

## Kero maji kijijini miaka 58 yaisha

**Na Godfrey Mushi, SAME**

HATIMAYE serikali kupitia Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (Ruwasa), imemaliza kero ya maji katika Kijiji cha Bendera, Wilaya ya Same ambayo imekuwa ikiwakabili wakazi wa eneo hilo kwa miaka 58.

Tangu kupatikana kwa Uhuru, kijiji hicho kimekuwa kikikabiliwa na tatizo la maji na hivyo kusababisha shughuli za kiuchumi kukwama kutokana na wazalishaji mali wakubwa ambao ni wanawake na vijana, kuhemea maji kutwa nzima katika vijiji vya jirani. Meneja wa Ruwasa na Mhandisi wa Maji wa Wilaya ya Same, John Casmiri, aliyasema hayo jana wakati mradi huo wa maji katika Kijiji cha Bendera ulipotembelewa na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama Cha Mapinduzi (NEC), anayewakilisha mkoa wa Kilimanjaro, Joseph Thadayo.

"Mradi huu wa maji katika Kijiji cha Bendera umeigharimu serikali kiasi cha zaidi ya Sh. milioni 308.159 ili kuondoa kero ya upatikanaji wa maji iliyokuwa ikiwakabili wananchi wa kijiji cha Bendera kwa muda mrefu.

"Kimsingi mradi wenyewe, una uwezo wa kuwahudumia wananchi 6,137 ambao ndio wanufaika wa maji haya yanayotokana na kisima kirefu." Alisema shughuli za uendeshaji wa mradi huo, zitasimamiwa na Jumuiya ya Watumia Maji iliyoundwa na wananchi wenyewe na kwamba kila mwananchi atapaswa kuchangia huduma ya maji kwa Sh. 25 kwa ndoo moja ya lita 20.

Meneja Mradi wa Maji Wilaya ya Same (Ruwasa), Mhandisi John Casmiri, aliyasema hayo katika taarifa yake kwa mjumbe wa Halmashauri Kuu Taifa ya CCM, Mkoa wa Kilimanjaro Joseph Thadayo, wakati alipotembelea mradi huo kukagua utekelezaji wa ilani ya uchaguzi mwaka 2015 na kuongeza kuwa mradi huo umekamilika na kutosheleza walengwa.

Baada ya kutembelea mradi huo, Thadayo alisema mradi huo ni mkubwa na kama inawezekana maji ya ziada yaliyopo katika mradi huo ni vyema yakasambazwa pia vijiji vya jirani ili kupunguza gharama za uendeshaji. "Huu mradi ni mkubwa na utekelezaji wa ilani ya uchaguzi kwa hapa naona mmetekeleza kwa asilimia mia moja nashauri kama fedha zikipatikana bora mradi huu upanuliwe ili uweze kuwa hudumia wananchi wa vitongoji vya jirani vyenye shida ya maji," alisema Thadayo.



Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (Tantrade), Edwin Rutageruka (wa pili kushoto), akikagua mojawapo ya banda katika Maonyesho ya Biashara ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yanayofanyika jijini Mwanza jana. **PICHA: ROSE JACOB**

# Serikali yajipanga ujenzi wa barabara ya Masama

**Na Paul William, HAI**

SERIKALI imepanga kuanza tena kazi ya ujenzi wa barabara ya Masama Junction, Wilaya ya Hai kwa kiwango cha lami, kuanzia Septemba 23, mwaka huu.

Ofisa Mipango wa Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads) mkoa wa Kilimanjaro, Mhandisi Baraka John, alisema barabara hiyo yenye urefu wa kilomita tatu, itajengwa kwa awamu ambapo awamu ya kwanza itahusisha ujenzi wa kilomita 1.6 kwa gharama ya Sh. bilioni 1.1

Akitoa taarifa hiyo jana kwa wajumbe wa kamati ya siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoa wa Kilimanjaro, Mhandisi John, alisema kabla uamuzi huo kufikiwa kulitokea changamoto ya ardhi kwa wananchi kujenga makazi yao katika eneo la hifadhi ya barabara.

"Tumeshapokea fedha za ujenzi wa mradi huu na tunatarajia mkandarasi ambaye ameshapatikana aanze kazi Septemba 23, tunafanya kila jitihada kuhakikisha kwamba mkandarasi huyo anaongeza kasi ili mradi huu uweze kukamilika kwa muda uliopo kwa mujibu wa mkataba," alisema.

Jimbo la Hai, linaongozwa na Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe, ambaye pia ni Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni (KUB).

Itakumbukwa kuwa Oktoba mwaka 2012, Rais mstaafu Jakaya Kikwete, alizindua sehemu ya barabara ya Kwa Sadala/Masama JCT, yenye urefu wa kilomita 12.5

Baada ya kupokea taarifa hiyo, Katibu wa CCM mkoa wa Kilimanjaro, Jonathan Mabihya, alitoa rai kwa Tanroads kusimamia vizuri fedha za miradi mbalimbali zinazotolewa na serikali ili wananchi wanufaike na kodi zao.

Kwa mujibu wa Mabihya, wapo baadhi ya watendaji wa serikali wamekuwa wakishindwa kusimamia kwa ukaribu miradi inayotekelezwa na serikali pamoja na kutojali thamani ya fedha halisi, jambo ambalo husababisha miradi hiyo kutodumu.

"Ipo baadhi ya miradi ikiwamo barabara ambazo hujengwa chini ya kiwango na kuisababishia hasara serikali katika kuifanyia ukarabati. Niwaombe wasimamizi wa miradi hii, tekelezeni majukumu yenu kwa ufanisi mkubwa ili thamani ya fedha ionekane," alisisitiza Mabihya.

Aidha, alionya baadhi ya watu ambao wamekuwa wakifanya upotoshaji kwa makusudi kwa kutengeneza propaganda kwamba mikoa ya kaskazini ya Kilimanjaro na Arusha, imetengwa katika miradi ya maendeleo, akisema hao ni vipofu wa maendeleo.



Ukurasa 18

**Afrika yaonywa itakabwa na mkate, siagi kutoka China**




Ukurasa 15

Mkutano wa 39 wa SADC umefanikiwa, tusonge mbele



Ukurasa 17

## Katibu Mkuu UN amaliza ziara Mashariki ya DRC


# siasa

JUMATANO SEPTEMBA 4, 2019

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU




Ukurasa 20

## Wafuasi wa Trump Italia wajitoa serikalini, waingia rasmi upinzani

# Ibrahim Mohamed Kaduma 1937-2019, mtawala, msomi na mzalendo

**Na Miki Tasseni**

MAUTI imemfikia mzee wetu Ibrahim Mohamed Kaduma, ambaye anafahamika kote nchini kutokana na kazi alizofanya katika miaka ya 1970 kwa kipindi kifupi kiasi.

Ya kwanza ni kuwa Mkurugenzi wa Taasisi ya Taaluma ya Maendeleo ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), nafasi iliyomwezesha kutumia muda wake wa ziada katikati ya mwaka 1975 kupeleka vipeperushi ambavyo alivitengeneza mwenyewe, vikisema 'Tumia kura yako vizuri. Mchague Nyerere,'

Na baada ya hapo kuwa Waziri wa Nchi (Ofisi ya Rais) Mambo ya Nje. Nafasi hiyo ilimpa upana wa kufahamika zaidi, halafu akarudi UDSM kukamilisha utumishi wake hapo kama Makamu Mkuu wa Chuo, kwa dhamira ile ile ya ukereketwa wa chama cha TANU,

INAENDELEA UK.16



Marehemu Ibrahim Kaduma. **PICHA: MTANDAO**

## DC Muwango: Nachingwea ni ya maendeleo kwanza, ndipo vyama

Ukurasa 19

# Ajenda ya Katiba kuakisi Uchaguzi Mkuu 2022 Kenya

**Na Mashaka Mgeta**

MFUMO wa Uchaguzi Mkuu wa Kenya umekuwa ukiathiriwa na mahitaji ya nyakati yanayopata nguvu kwa kuungwa mkono na mafungamano ya vyama vya siasa yaliyorasimishwa katika kutafuta mamlaka ya dola nchini humo.

Hali ndivyo ilivyokuwa katika kuelekea uchaguzi Mkuu wa 2007 ambapo Mwai Kibaki alipata ushindi uliotiliwa shaka dhidi ya aliyekuwa mshindani wake wa karibu, Raila Odinga.


Wakati huo, ajenda iliyotawala kwenye mafungano ya vyama hivyo ilikuwa ni Katiba mpya iliyowagawa Wakenya katika makundi yaliyojulikana kama 'Chungwa' la kinara wa siasa za upinzani nchini humo, Odinga na 'Ndizi'.

Lakini katika Uchaguzi Mkuu wa 2013, suala la muhimu kwa mafungano ya vyama hivyo ilikuwa ni kushtakiwa kwenye Mahakama ya Kimataifa ya Makosa dhidi ya Ubinadamu (ICC) kwa Kenyatta, Naibu Rais wa sasa, William Ruto na watu wengine kadhaa.

Upande wa Odinga uliokuwa ukisisitiza umuhimu wa sheria kuchukua mkondo wake dhidi ya viongozi hao, wahusika katika kadhia hiyo walifika kila kona ya Kenya na kukanusha kuhusika kwao katika tuhuma za mauaji ya baada ya Uchaguzi Mkuu wa 2007.

Hivi sasa wakati Kenya ikijiandaa na Uchaguzi Mkuu wa 2022, hoja inayotawala ni kuhusu kuwa po mabadiliko ya Katiba yanayotarajiwa kuwa sehemu ya mapendekezo ya kamati maalum iliyoundwa na Rais Kenyatta kuratibu shughuli za serikali ili kuongeza ufanisi nchini humo maarufu kama BBI.

Kamati hiyo inadaiwa kumuweka kando Ruto na washirika wake, hivyo kutafsiriwa kwamba ni hatua muhimu ya 'kumfuta' Ruto katika siasa za taifa hilo lenye nguvu kubwa za uchumi katika ukanda wa Afrika Mashariki.



Rais Uhuru Kenyatta (kulia), Naibu Rais William Ruto (juu kushoto picha ndogo) na kiongozi wa upinzani nchini Kenya, Raila Odinga. **PICHA: MTANDAO**

### KENYATTA, ODINGA NA BBI

Lakini wakati upande wa Rais Kenyatta akishirikiana na Odinga wanaunga mkono kuwepo mabadiliko ya Katiba yenye kuwa na nafasi nyingi za uongozi kama Waziri Mkuu na Manaibu wawili, washirika wa Ruto wanaliona hilo kuwa litaongeza gharama za uendeshaji wa serikali, na hivyo wameanzisha kampuni inayojulikana ya 'punguza mzigo'.

Akizungumzia kampeni hiyo, Odinga, amefika hadi kaunti ya Migori hivi karibuni na kuwaambia wafuasi wa chama chake katika Bunge la kaunti hiyo, kuipuuzia kampeni ya 'Punguza Mizigo' itakapowasilishwa kwa ajili ya kujadiliwa.

Raila aliyekuwa anazungumza kwenye kijiji cha Rinya katika mji mdogo wa Uriri Ijumaa iliyopita, wakati wa mazishi ya Askofu Joseph Ogutu wa kanisa la St John Everlasting, akasema makubaliano ya BBI ndiyo yanayopaswa kufuatwa.

"Haya masuala ya 'Punguza Mizigo' hatuyajui, tunaomba Bunge la kaunti ya Migori kuyakataa pindi muswada utakapowasilishwa kwenye baraza lenu kwa kujadiliwa," anasema Odinga.

> "Muda tuliopewa kukabidhi ripoti hii ni Oktoba, lakini tutafanya kila linalowezekana kuhakikisha tunaikamilisha kazi hii kabla ya muda huo.

Odinga anamtaka Gavana wa Migori, Obado, kuhakikisha kuwa kaunti hiyo inafuata mfano wa wenzao wa Siaya (anapotokea Odinga) kwa kuukataa muswada wa 'Punguza Mizigo' uliopigiwa upatu na Ekuru Aukot.

Gavana Obado, anamthibitishia Odinga kumuunga mkono katika jitihada zake za kuanzia kushikana mkono na Rais Kenyatta, kulikoleta mafanikio yakiwamo uboreshaji wa bandari ya Kisumu utakaochochea maendeleo na ustawi wa wananchi wa eneo hilo.

Mbunge wa Uriri, Mark Nyamita, anaonya kuwa Bunge la Migori lisipoukataa muswada ama vinginevyo, watahitajika kujiandaa kurejea makwao kwa kukosa imani kwa wapigakura wao.

"Muswada wa 'Punguza Mizigo' hautaelezea masuala ya Wakenya na unakosa baraka za raia wa Kenya," anasema.

Raila katika msafara huo alifuatana na mkewe, Ida Odinga, Gavana wa zamani wa Kisumu, Jack Ranguma, Seneta wa Migori, Ochilo Ayacko, Mwakilishi wa wanawake kwenye kaunti hiyo, Pamela Odhiambo, Spika wa Kaunti, Boaz Okoth na Mbunge wa zamani wa Migori, John Pesa, miongoni mwa wengine kadhaa.

Awali, taarifa zilieleza kuwa Rais Kenyatta na Odinga, watafanya kampeni nchi nzima kuwaelezea raia wa nchi hiyo kuhusu mapendekezo ya kamati maalum ya BBI pindi itakapokamilisha kazi iliyopewa.

### MABADILIKO YA KATIBA

Katibu Mkuu wa Muungano wa vyama vinavyotawala Kenya wa Jubilee, Raphael Tuju na Mwenyekiti wa ODM, John Mbadi, wanasema ziara za viongozi zitawawezesha Wakenya kuelewa mwelekeo wa nchi hiyo kadri ya mapendekezo yatakayotolewa.

Tuju akasema waraka wa BBI utakaowekwa kuwa muswada, unaweza kupitishwa na Bunge ama kama yatatakiwa maoni ya wananchi, basi kura itapigwa.

Wakati akisema hivyo, kumbukumbu zinaonyesha kuwa Odinga aliwahi kuwataka Wakenya kujiandaa kwa ajili ya kura ya maoni ya mabadiliko ya Katiba mwakani.

Hiyo ikimaanisha kuwa pindi ripoti ya BBI itakapokamilika, ni wazi kwamba ziara ya Rais Kenyatta na Odinga italenga kuipigia kampeni. Rais Kenyatta na Odinga, wakapanga kufanya ziara katika eneo la Mlima Kenya katika mikutano yao ya awali ya pamoja.

Wakili Paul Mwangi ambaye ni Katibu Mwenza wa BBI, anasema walikuwa mahali tulivu kwa ajili ya kuandika ripoti itakayokabidhiwa kwa Rais Kenyatta na Odinga.

"Muda tuliopewa kukabidhi ripoti hii ni Oktoba, lakini tutafanya kila linalowezekana kuhakikisha tunaikamilisha kazi hii kabla ya muda huo," anasema Mwangi.

Mwanasheria Mkuu wa zamani wa Kenya ambaye kwa sasa ni Seneta wa Busia, Amos Wako, ambaye pia ni mjumbe wa timu ya BBI, anasema hawawezi kutoa maudhui ya dondoo walizozipata mpaka watakapokabidhi ripoti yao kwa viongozi hao.

Lakini kwa upande wake, Tuju anaamini kuwa ripoti ya BBI, itatoa mapendekezo yatakayochochea umoja wa kitaifa.

### KENYATTA AZIDI KUUNGWA MKONO

Licha ya historia ya wanasiasa wa Kenya 'kugeukana' wakati wa kuelekea Uchaguzi Mkuu, lakini kwa sasa upande wa Rais Kenyatta katika Jubilee unadaiwa kuungwa mkono na ODM ya Odinga, Wiper Democratic Movement ya Kalonzo Musyoka, Amani National Congress ya Musalia Mudavadi, Ford Kenya ya Moses Wetang'ula na KANU ya Gideon Moi

Muungano huo kama utadumu katika uimara wake, unakisiwa kutoa mwelekeo wa mgombea urais katika Uchaguzi Mkuu wa 2022.

### RUTO AZIDI 'KUMTESA' KENYATTA

Ruto hivi sasa, kupitia kwa washirika wake wanapinga waziwazi jitihada za BBI na hatua hiyo inamuweka katika mwendelezo wa 'kutembea njia tofauti'; na bosi wake, Rais Kenyatta na hasimu wake mkubwa wa kisiasa, Odinga.

Muungano wa vyama vinaunga mkono mabadiliko ya Katiba `vinabeba' dhana kuu kwamba, mfumo uliopo sasa wa Rais kuwa mkuu wa nchi haufai kwa vile unachangia kukuza ukabila, hivyo ipo haja ya kuuboresha.

Upande wa akina Rais Kenyatta na Odinga unataka mabadiliko ya Katiba yaruhusu utawala unaozingatia jinsia kwa theluthi mbili na uteuzi wa wabunge kuwa mawaziri.

### ODINGA NA URAIS 2022

Dalili za Odinga kutaka kuwania urais katika Uchaguzi Mkuu ujao zimeibua sintofahamu katika muungano wa NASA alioupitia kuwania kiti hicho katika uchaguzi uliopita wa mwaka juzi.

Katika uchaguzi huo, Nasa ilivijumuisha vyama vya Wiper Democratic Movement, Amani National Congress (ANC) na Ford Kenya.

Ingawa Odinga hajatamka hadharani nia ya kuwania urais 2022, mwenendo wake kisiasa baada ya kushikana mkono na Rais Kenyatta Machi 9, mwaka jana, unaashiria nia hiyo.

Vyama vya Wiper na ANC vilivyo washirika wa NASA vimewahi kutamka kwamba baada ya kujaribu kuwania urais wa Kenya mara nne bila mafanikio, safari hii anapaswa kuteuliwa mgombea mwingine tofauti na Odinga.

Mkurugenzi Mtendaji wa Wiper, Jared Siso, amekaririwa akisema chama hicho kinaamini kuwa shughuli za kisiasa za Odinga katika Kenya zinaashiria mpango wake wa kutaka kuwania tena urais.

Kwa hali hiyo, Mkurugenzi huo anasema kwa vile makubaliano ya muungano wa Nasa bado yapo, Odinga hatakuwa na namna nyingine isipokuwa kumuunga mkono Kalonzo anayepaswa kuteuliwa kuwania kiti hicho.

### RUTO AZIDI KUJIIMARISHA

Ruto amekuwa akimshutumu Odinga kwa kuingilia mambo ndani ya Jubilee, huku akitumia kigezo cha kushikana mkono kwake na Rais Kenyatta.

"Wanaotuletea matatizo katika chama cha Jubilee ni watu kutoka nje ya chama chetu, tuna chama chetu cha Jubilee kwa hiyo wengine wanapaswa kujipanga kivyao," anasema Ruto.

Ruto anaamini kwamba walio nje ya Jubilee ni wajuzi wa kupiga kelele tofauti na ilivyo Jubilee inayolenga kuchagiza kasi ya maendeleo ya Kenya na watu wake.

***Makala haya yameandikwa kwa msaada wa vyanzo mbalimbali. Mwandishi wake anapatikana kupitia simu namba +255 754 691540 ama barua pepe:mgeta2000@yahoo.com***

# Mkutano wa 39 wa SADC umefanikiwa, tusonge mbele

**Na Dk. Felician Kilahama**




Mwenyekiti wa sasa wa SADC, Rais John Magufuli (wa tatu kutoka kushoto), akikabidhiwa vitendea kazi na mwenyekiti aliyemaliza muda wake, Rais wa Namibia, Dk. Hage Geingob (wa pili kushoto). **PICHA: MTANDAO**

NIANZE Mada hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye sina wa kumfananisha naye kwa kutujalia zawadi ya Uhai na kwa mema mengi anayotujalia kila siku.

Kipekee namshukuru Mungu kwa kuwezesha kikao cha kawaida cha 39 kwa nchi wanachama 16 wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kufanyika hapa Tanzania.

Vilevile, ni heshima kwa nchi yetu kuona Rais wa Awamu ya Tano Dk. John Magufuli akikabidhiwa madaraka ya kuiongoza SADC.

Mkutano ulifanyika kwenye Ukumbi wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere Jijini Dar-es-Salaam: kwanza Wataalamu wakakutana wakafuatiwa na Kikao cha Baraza la Mawaziri na hatimaye Kikao cha Wakuu wa Nchi na Serikali kilichofanyika Agosti 17 na 18, 2019.

Ulikuwa mkutano wa kihistoria kwa taifa letu hasa kutokana na Rais wetu kuwa Mwenyekiti wa SADC baada ya Rais wa Namibia Dk. Hage Geinhob kumaliza muda wake. Hakika Mungu ni mwema maana ni kwa mapenzi yake tukio hilo kufanyika kwenye ardhi ya nchi yetu na kwa wakati ambao Dk. Magufuli akiwa kiongozi mkuu wa Serikali.

Mkutano ulimalizika kwa mafanikio makubwa hivyo naamini Wakuu wa Nchi na Serikali pamoja na walioambatana nao waliondoka wakiwa na kumbukumbu nzuri kuhusu taifa letu na hasa vivutio vya utalii vilivyopo nchini.

Watanzania tuangalie tukio hilo kama mwanzo wa fursa za kufanya vizuri zaidi hasa kuhusu kujiendeleza kiuchumi kupitia Sera ya Uchumi wa Viwanda na kufikia kipato cha kati 2025.

Iwapo Wakuu wa Nchi na Serikali wamedhamiria kwa dhati kuwa nchi wanachama wa SADC ziwe kinara katika kujiletea maendeleo endelevu; ni dhahiri kuwa tunahitaji kujizatiti vya kutosha kuweza kukidhi nia hiyo njema kupitia fursa za elimu, afya, madini, kilimo, viwanda, ufugaji, maliasili na utalii.

Dk. Magufuli, Rais wa Tanzania alipokabidhiwa Uenyekiti wa SADC; alisema kuwa nchi zinazounda umoja huu ikiwamo Tanzania ni tajiri na siyo maskini kama ilivyozoeleka. Kwa mtazamo huo hajafurahishwa na hali halisi ndani ya SADC kutokana na rasilimali tulizonazo hazijatumika ilivyotarajiwa ili kuinua uchumi wa nchi husika pamoja na kuboresha hali ya maisha kwa wananchi wake.

Nchi za SADC ziliweka lengo la asilimia saba kama matarajio ya kupanda kwa pato la eneo la SADC kila mwaka. Hali halisi inaonyesha kuwa pato limekuwa likipanda kwa wastani wa asilimia tatu tu kwa mwaka.

Inawezekana kumekuwapo na changamoto kama madhara ya mabadiliko ya tabianchi kusababisha ukame wa muda mrefu au mafuriko ya mara kwa mara; wakulima kutowezeshwa vya kutosha ikiwamo ukosefu wa mbegu bora au miundombinu ya umwagiliaji, masoko nakadhalika.

> Naomba Baraza la kuendeleza Kiswahili liwe mstari wa mbele kuhakikisha maneno ya Kiswahili ni sahihi katika kutamka na kuandika.

Hivyo hatunabudi kuchangamka na kuhakikisha changamoto za aina hiyo zinatafutiwa ufumbuzi wa kutosha.

Mwenyekiti Rais Dk. Magufuli alisisitiza kuwa SADC inazo rasilimali za kutosha ikiwamo ardhi kilometa za mraba 9,882,959 au tatribani hekta milioni 988.3 pamoja na rasilimali watu zaidi ya milioni 327 ambao ni nguzo kubwa ya kujiletea maendeleo endelevu.

Kwa mantiki hiyo iwapo nchi wanachama wa SADC zitajipanga vizuri na kuweka mikakati ya pamoja juu ya namna bora ya kutumia rasilimali hizo kwa maendeleo yetu pato litaongezeka.

Aliyekuwa Rais wa Tanzania wa Serikali ya Awamu ya Kwanza (1961 mpaka 1985); Marehemu Mwalimu Julius Nyerere, aliwahi kusema kuwa ili tuendelee tunahitaji vitu vinne: "Ardhi, Watu, Siasa safi na Uongozi bora." Nathubutu kusema kuwa mpaka leo nyenzo hizo bado ni muhimu kwa taifa kuweza kujiletea maendeleo endelevu.

Nchi 16 wanachama wa SADC zinamiliki ardhi ya kutosha, rasilimali hii ikiambatana na uongozi bora; siasa safi na wingi wa rasilimali watu pamoja na maliasili zilizopo ikiwemo misitu, wanyamapori, madini, maji, na uvuvi: tukiunganisha nguvu ya pamoja hakuna sababu ya SADC kutosonga mbele kiuchumi ipasavyo kwa manufaa ya wote.

Naamini kwa kutumia vyombo kama Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) tutafanya kweli tukizingatia kuwa kwa miaka mingi sana changamoto za umaskini, maradhi na ujinga zimetusumbua sana.

Sasa ni wakati wa kukabiliana na changamoto husika ipasavyo na bila kutetereka.

Hata hivyo, uzoefu unaonyesha kuwa, wakati mwingine, ni rahisi kusema kuliko kutenda lakini naamini kutokana na mshikamano ulioonyeshwa wakati wa mkutano wa 39 wa SADC yawezekana tukafanikisha malengo kwa kiasi kikubwa.

Pamoja na kujiwekea malengo ya kiuchumi Jumuiya hii pia inahitaji kuwapo na hali ya kuridhisha kiusalama na amani kwa wote.

Hili ni suala muhimu sana maana bila utulivu na usalama, yaani kuwapo amani tele inabakia kuwa hali ya kutoaminiana.

Uchumi wa viwanda na kufikia kipato cha kati kwa nchi wanachama wa SADC itawezekana iwapo kuna utulivu na amani mijini na vijijini.

Mfano, wakulima na wafugaji pamoja na wafanyakazi ikiwamo wafanyabiashara, shughuli zao zitaenda vizuri iwapo miundombinu imara na masoko vitakuwapo.

Kwa bahati nzuri soko kwenye eneo la SADC na Afrika Mashariki halina shaka, kinachotakiwa ni kuzalisha bidhaa na huduma bora ili kukidhi mahitaji ya soko.

Hayo yote yanawezekana ndani ya nchi iliyo tulivu na yenye amani ya kutosha.

Vivyohivyo mafanikio yatapatikana iwapo umoja ndani ya SADC utaimarika zaidi: kukawapo kusikilizana na sauti moja yenye lengo la kuinua mapato ya nchi wanachama lakini pia kuboresha maisha ya wananchi ndani na nje ya nchi husika.

Mathalani kupitia biashara, kusimamia masuala ya forodha vizuri, ulinzi au usimamizi wa pamoja na kadhalika.

Penye mafanikio hapakosi kuwapo wasiyopenda kuona nchi za SADC zinasonga mbele kiuchumi, hivyo tukae chonjo na kuchukua hatua kwa faida ya wote.

Kwa Tanzania tunashukuru Wakuu wa SADC kukubali Kiswahili kiwe lugha rasmi ya nne na kitumike ipasavyo.

Hili ni jambo jema kwetu Watanzania maana kupitia uamzi huo tutakuwa na fursa za kuendeleza Kiswahili Kusini mwa Afrika.

Hii ni pamoja na fursa za ajira na matumizi ya ndani na nje ya SADC.

Naomba Baraza la kuendeleza Kiswahili liwe mstari wa mbele kuhakikisha maneno ya Kiswahili ni sahihi katika kutamka na kuandika.

Nimekuwa nasikia maneno kama "lisaa limoja"; masaa mawili na kadhalika mpaka najiuliza "hilo lisaa limoja likoje"? kwa nini hatusemi "saa moja au saa tano" ukiulizwa utatumia muda gani badala ya kusema "lisaa limoja au masaa mawili" ukasema nitatumia saa moja au saa mbili?

Tumeegemea sana matumizi ya Kiswahili cha mitaani badala ya Kiswahili sanifu hivyo tutahitaji maboresho sana.

Mungu Ibariki Afrika, Mungu Ibariki SADC na Mungu Ibariki Tanzania.

***Dk. Felician Kilahama***
***Mwenyekiti Bodi ya Ushauri-Misitu Africa***
***P.O. Box 79011, Dar-es-Salaam, Tanzania,***
***fkilahama@gmail.com; +255756007400; +255714250050;***

# Ibrahim Mohamed Kaduma 1937-2019, mtawala, msomi na mzalendo


Marehemu Mzee Ibrahim Kaduma (mwenye suti nyeusi), akiteta jambo na Waziri Mkuu Mstaafu, Salim Ahmed Salim (wa pili kulia) enzi za uhai wake wakati wa kutoa maoni ya katiba mpya.

**INATOKA UK.13**

kikiwa ni CCM sasa.

Kama ilivyo kwa viongozi wengi wa kipindi cha awamu ya kwanza, aliingia katika madaraka ngazi za juu mara baada ya kumaliza elimu ya chuo kikuu; wengi walianzia ukurugenzi halafu ukatibu mkuu, kwani waliokuwa chini yao walikuwa watu wa diploma na vyeti waliopanda vyeo wakati wasimamizi kutoka Uingereza wakiondoka.

Mzee Ali Hassan Mwinyi kwa mfano alirudi Zanzibar mwaka 1964 kutoka Chuo Kikuu cha Durham nchini Uingereza na kuingia katika jukumu la ukatibu mkuu Wizara ya Elimu ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kwa haraka tu.

Hayati Kaduma alifanya kazi kama hiyo kule Mawasiliano, na wakati huo watawala walikuwa wanatumia vifupisho vya idara ikipelekewa ujumbe kwa ‘telegram’ hivyo Mawasiliano ni Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, halafu akaenda Hazina, yaani Wizara ya Fedha.

Ni hapo ambako alishuhudia tatizo la kukwama kwa mkakati wa dhana ya Devplan, yaani Wizara ya Mipango ya Maendeleo.

> Huko alitumikia wizara mbili, Biashara halafu Mawasiliano na Uchukuzi, lakini kuna wanaosema ni wazi asingedumu muda mrefu.

Dhana ya msingi ilikuwa ni kuweka mikakati ya uchumi Devplan, ili Hazina iandae mpangilio wa matumizi ya fedha kufuatana na vipaumbele vilivyoainishwa lakini hitilafu kadhaa zikajitokeza.

Madai na mahitaji ya rasilimali yaliizidi nguvu Devplan, na maamuzi ya mwisho ya matumizi ya fedha hayakuwa huko ila Hazina na mwisho kabisa ni Ikulu ndiyo ilikuwa inaamua.

Licha ya kuwa watawala wanaondolewa kutoka eneo moja au jingine kutokana na mvutano au ugomvi, na labda ionekane kuwa kuna upungufu wa unyenyekevu mahali fulani, mtawala wa ngazi ya juu anayesoma dhamira za watu kama Rais Nyerere, angetofautisha ugomvi wa masuala ya kijinga na ukereketwa.

Ibrahim Kaduma alikuwa mkereketwa wa mstari wa mbele katika kazi zake zote, hali iliyosaidia kupunguza urefu wa kipindi chake cha uongozi katika ngazi za juu, kwani angejitambulisha mapema mno yuko upande gani katika suala lolote lile.

Ziko hekaya za hapa na pale za ukereketwa wa Kaduma na jinsi ulivyokuwa unapokelewa na ‘silent majority’ ya wakati huo, yaani kundi la watiifu wapitisha muda, wasio na uzalendo kwa kile wanachosema.

Moja ya hekaya hizo ni jinsi hayati Ibrahim Kaduma alivyojitahidi kukusanya vikaratasi dhidi ya utawala wa Rais Nyerere mwaka 1968 vilivyotawanywa na watu wa Oscar Kambona, ‘kigogo’ aliyekuwa waziri wa Mambo ya Nje, akahamishiwa Tawala za Mikoa (akiaminiwa eti anapinga Azimio la Arusha) halafu akakimbia nchi.

Kijana mmoja wa wakati huo akielezea jambo hilo miaka ya 1980 masomoni ng’ambo alisema watu walikuwa na hamu ya kusoma kilichoandikwa halafu Kaduma anakusanya vyote na kuchoma moto. Hawakuweza kumzuia, wanasaga tu meno.

Hapakuwa na hekaya za maana Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuhusu usimamizi wa IDS (taasisi ya maendeleo) hadi mwaka 1975, lakini kipindi chake cha umakamu Mkuu wa Chuo una visa kadhaa vinavyoelezea ukereketwa.

Cha kwanza ni jinsi alivyoanza kwa kuwaondoa wahadhiri kadhaa wa ngazi za juu kwa sababu za kinidhamu, ila wengi waliona kuwa kuna chembe ya itikadi iliyokuwa inaleta tatizo, ila suala hilo lilisisimua watu mwaka 1977 likapita na kukawa kimya; akarudi serikalini mwaka 1980.

Huko alitumikia wizara mbili, Biashara halafu Mawasiliano na Uchukuzi, lakini kuna wanaosema ni wazi asingedumu muda mrefu.

Kuna kisa kinasema wakati anaingia uwaziri, mmoja kati ya mawaziri wa siku nyingi alimsikiliza halafu akamwambia ‘kuna mawaziri wa aina mbili, wa kudumu na wapita njia. Wewe ni mpita njia.’

Katika kipindi chake cha umakamu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, nje ya kuwaondoa maprofesa ambao alisema wana utovu wa nidhamu, aliwahi kuvutana na uongozi wa Umoja wa Vijana wa CCM Mlimani.

Katika kikao walipoona hawaelewani wakamwambia watamshitaki makao makuu ya chama, na alichojibu kilimtofautisha na mtangulizi wake katika nafasi hiyo, Pius Msekwa.

Mtangulizi wake alipovutana na viongozi wa umoja huo uliokuwa ndio sikio la uongozi wa chama kufuatilia hisia za vijana UDSM alipoambiwa atashtakiwa TANU aliwaangalia usoni, akawaambia, ‘Vijana, mnaposikia TANU, ni sisi.’

Ukimsikiliza, utaielewa TANU na hata ungekwenda kutafuta ufafanuzi wa suala fulani, Sekretariat itamwomba autoe....

Hayati Kaduma hakuwa na ukaribu wa kiwango hicho na uongozi wa juu wa TANU au waasisi wake, ila alikuwa kada wa mstari wa mbele kwa utetezi na uhamasishaji wa malengo yake na serikali kwa jumla.

Alipovutana na vijana aliwaambia ‘Vijana, damu ya CCM inapita katika mishipa yangu,’ walipohoji utiifu wake kwa kile walichokielewa kuwa ndiyo itikadi ya CCM na hasa kwa fikra za mwenyekiti wa chama, Rais Nyerere.

Mchango wake utakaokumbukwa kwa muda mrefu au tuseme uliodumu chuoni hapo ni pamoja na kukusanya na kuhariri kitabu akiwa na Profesa Gabriel Ruhumbika, ‘20 Years of TANU Leadership, 1954-1974.’

Walitafuta mada nzito kwa sekta kadhaa hadi wakati huo, zilizowezesha rejea hadi miaka ya 1990, hata mbeleni.

Katika kipindi chake cha kustaafu utumishi wa juu serikalini hakuwa anasikika sana, na licha ya kuitwa mwanasiasa mkongwe siyo rahisi kusema kuwa hayati Kaduma alikuwa mwanasiasa, kwa maana ya kutafuta kufahamika katika CCM na hata kugombea ubunge, n.k.

Alitoa ‘mpya’ katika miaka ya 1990 alipobadili dini kutoka Uislamu kuingia Ukristo, na akiwa katika hulka halisi ya mfuasi wa Mwalimu, na akizingatia historia ya majina hasa katika Biblia, hakubadili jina.

Taarifa fupi redioni ilisema Ndugu Ibrahim Mohamed Kaduma amebadili dini na sasa ni Mkristo. Majina yake yako pale pale, Ibrahim Mohamed Kaduma,’ kuainisha undugu, si vita.


Labda tu kwa wanaokifahamu Chuo Kikuu, UDSM itakumbukwa kuwa yalikuwapo maandamano ya wanafunzi dhidi ya sera za kukata mishahara za Rais Nyerere, pamoja na kwenda Jeshi la Kujenga Taifa miezi sita halafu kulipwa nusu mshahara miezi 18.

> Walitafuta mada nzito kwa sekta kadhaa hadi wakati huo, zilizowezesha rejea hadi miaka ya 1990, hata mbeleni.

Mkuu wa chuo kikuu kishiriki wakati huo (Profesa Cranford Pratt ambaye alimfundisha Nyerere chuoni Makerere) alishangaa vijana wakipita Manzese na majoho ya chuo, mabango ya Kiingereza ‘Colonialism Was Better,’ ambayo Nyerere alitafsiri ‘Afadhali Mkoloni.’

Licha ya kuwafukuza na kuwarudisha baadaye viongozi wa maandamano hayo, aliona umuhimu wa kujengewa uzalendo wanafunzi wa chuo kikuu, ndiyo ikaundwa ‘common course,’ ilenge kuelewa dhamira ya TANU na serikali yake, na mapana ya usahihi wa dhamira hiyo kihistoria na maendeleo kwa jumla.

Ndiyo Development Studies iliyoanza mwaka 1967 na miaka sita baadaye Kaduma akapelekwa UDSM kuisimamia.


Mzee Ibrahim Kaduma akichangia mada zilizokuwa zikitolewa na baadhi ya wajumbe waliohudhuria Mdahalo kuhusu suala la kupatikana kwa Katiba mpya ya nchi. Mzee Kaduma alikuwa mmoja wa wanataaluma wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

# Katibu Mkuu UN amaliza ziara Mashariki ya DRC


Katibu mkuu wa UN, Antonio Guterres (aliyeshika karatasi), akiwa katika ziara yake Mashariki mwa DRC katika mji wa Beni. **PICHA: MTANDAO**

KATIBU Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Guterres, amekamilisha ziara yake Mashariki ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), kwa kutembelea kituo cha afya wanakotibiwa wagonjwa wa Ebola Magharibi mwa mji wa Beni.

Katika ziara yake kwenye kituo hicho kilicho katika mji mdogo wa Mangina kilomita 30 Magharibi mwa mji wa Beni, Guterres aliwasihi manusura wa Ebola kuwahamasisha watu walio karibu nao, kutokuwaficha majumbani wagonjwa, ili kusaidia kuitokomeza haraka homa hiyo.

Baada ya kupokewa na matabibu pamoja na manusura wa homa ya Ebola katika kituo cha afya wanakotibiwa wagonjwa, Guterres aliwahutubia manusura wa Ebola katika kituo cha afya cha Mangina, na kutoa wito wa kusambaza ujumbe kuwa wote wanaofika katika kituo hicho wanaweza kupona.

Amewataka pia wananchi kutoficha dalili za homa ya Ebola, bali watumie fursa ya kuushinda ugonjwa huo kwa kupata tiba katika kituo hicho.

Kwa upande wake Gavana wa Mkoa wa Kivu ya Kaskazini, Charly Nzanzu Kasivita, amewasihi watu wanaopinga uwepo na makali ya Ebola kuondokana na dhana hiyo potofu, bali wafike kupata matibabu katika eneo lililotengwa kwa ajili ya tiba ya Ebola

**USALAMA KIKWAZO KUKABILI EBOLA**

Kwa upande wa hali ya usalama kuwa mdogo katika eneo hilo, ikitajwa kama mojawapo ya vikwazo katika mpango wa kukabiliana na Ebola, Guterres ameahidi kwamba patafanyiwa mageuzi katika utendaji kazi wa Tume ya Umoja huo nchini DRC (MONUSCO).

Lengo likiwa ni raia wapate kunufaika na uwepo wa tume hiyo, na kwamba hilo litakuwa mojawapo ya masuala yatakayojadiliwa katika mkutano baina yake na Rais Félix Tshisekedi jijini Kinshasa.

Tume ya MONUSCO kwa ajili ya kustawisha amani katika DRC, ndio tume kubwa ya Umoja huo duniani na iliyo na vifaa vya kutosha.

Hata hivyo, imekuwa ikilaumiwa na raia nchini humo kwamba haijafanya vyema katika utendaji kazi wake, hasa kuyatokomeza makundi ya waasi katika mji na wilaya ya Beni na kubwa kuliko yote likiwa ni lile la ADF kutoka Uganda.

Kundi hilo linalotajwa kuhusika na mauaji ya watu zaidi ya 2,000 katika eneo hilo kwa kuwakata kwa mapanga pamoja na kuwapiga risasi. **DW**

# Afrika yaonywa itakabwa na mkate, siagi kutoka China

Na Gaudensia Mngumi

MKUTANO wa Mataifa ya Afrika na Japan, uliomalizika Japan wiki iliyopita haujainyamazia China kuhusu ushirikiano na Afrika ambao unaacha mzigo wa madeni.

Mkutano huo maarufu kama Tokyo International Conference on African Development (TICAD), unasimamiwa na Serikali ya Japan kuanzia mwaka 1993, ukishirikisha wadau kama Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Benki ya Dunia (WB) na Kamisheni ya Uchumi ya Umoja wa Afrika (AUC).

Waziri Mkuu wa Japan, Shinzo Abe, amewaambia viongozi wa Afrika wagutuke kuhusu deni la China na kuchukua tahadhari kwenye ushirika na taifa hilo ambao kwa mujibu wa madai yake unawaingiza Waafrika hatarini.

Abe, anaonya dhidi ya kuzibebesha madeni makubwa nchi za Afrika, akisema wawekezaji katika bara la Afrika hawana budi kuwa na tahadhari dhidi ya kuzitwika mzigo mkubwa wa madeni nchi hizo zenye uchumi unaokua na watu maskini, japo bara lao limejaa rasilimali za kutosha.

Japo Abe anaonekana kuelekeza zaidi ujumbe huo kwa China, ambayo sera yake ya ujenzi wa miundombinu ya reli na barabara imekuwa ikikosolewa kwamba inaziangamiza nchi maskini kwa kuzibebesha madeni makubwa, angalizo lake ni muhimu.

Kiongozi huyo akizungumza baada ya kumalizika kwa mkutano huo wa ushirikiano jijini Tokyo, anasisitiza kwamba nchi za kundi la mataifa yenye uchumi mkubwa duniani za G20 ikiwamo China zimejitolea.

Ni katika mpango wa kuyadhibiti madeni ili kuiepusha Afrika na mzigo mkubwa inayoubeba, jambo linalopaswa kuzingatiwa ili yasipite kiwango cha uwezo wa Afrika.

Baadhi ya miradi ya reli ambayo anaizungumzia Abe ni kama ile iliyoko Nigeria, Angola na Kenya.

Kwa mujibu wa taarifa za Shirika la Habari la China- Xinhua, China imejenga na inaendelea kukamilisha ujenzi wa reli za kisasa za (SGR) kutoka Mombasa hadi Nairobi nchini Kenya na ya Addis Ababa Ethiopia hadi nchi jirani ya Djibouti.

Xinhua linasema mwaka 2015, China ilikamilisha ujenzi wa kilometa 1,344 za reli ya kisasa nchini Angola, iliyounga miji ya pwani ikianzia Lobito hadi jiji la Luau lililoko mpakani na Congo.

Hii ni reli ndefu Afrika iliyojengwa na kampuni ya China ikiwa ni ya pili baada ya TAZARA. Reli hiyo inaunga miji mikuu na majiji ya Angola, Zambia, Tanzania na Congo pia.

Aidha, China imejenga SGR kutoka Abuja hadi jiji la Kaskazini la Kaduna nchini Nigeria, ikiwa na kilometa 187, iliyokamilika mwaka 2016 kwa mujibu wa Xinhua.

Nigeria imeendelea kunufaika na China kwenye ujenzi wa reli nyingine ya kisasa inayounga majiji ya Lagos na Ibadan na kwa ujumla China inashirikiana na Umoja wa Afrika (AU), kujenga reli ya kisasa itakayounga miji mikuu ya bara hili.

Miaka miwili iliyopita katika moja ya mikutano yake na wakuu wa serikali za Afrika, ilitangaza mpango wa kutoa Dola bilioni 60 (zaidi ya trilioni 130) kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya Afrika.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa (kushoto) akiwa na Waziri Mkuu wa Japan, Shinzo Abe wakati alipomwakilisha Rais John Magufuli kwenye Mkutano wa Afrika na Japan, uliomalizika karibuni. PICHA: MTANDAO

> Pembeni ya makao hayo makuu ndiko yaliko makao makuu ya Shirika la Misaada la China la China-Aid.

### AU MAKAO MAKUU

Sekretariati na Ofisi za Umoja wa Afrika, vituo vya mikutano na kwa ujumla makao makuu ya AU yaliyoko Addis Ababa nchini Ethiopia maarufu kama (AUCC), ni kazi iliyofanywa na China.

Lakini, pembeni ya makao hayo makuu ndiko yaliko makao makuu ya Shirika la Misaada la China la China-Aid.

Gharama za ujenzi huo zilizoko kwenye mtandao zinaonyesha kuwa ilitumia zaidi ya Dola milioni 200 sawa na bilioni 460 kujenga makao ya AU.

### UMEME WA INGA

China pamoja na AU zina ubia wa ujenzi wa bwawa la umeme la Grand Inga, lililoko kwenye Mto Inga nchini Congo.

Maporomoko yaliyoko ndani ya Mto Inga yanatarajiwa kuzalisha takribani megawati 40,000 za umeme zitakazolisha umeme Afrika nzima na kupunguza tatizo la nishati hiyo.

### KUOGOPA MADENI

Kwa hiyo, akiangalia mambo mengi yanayotumia mabilioni ya dola, Waziri Mkuu wa Japan, Shinzo Abe, anawaambia viongozi wa Afrika wawe macho na kujilimbikizia madeni kutokana na mikopo na kandarasi nyingi za miundombinu ya kisasa inayofanywa na China, kwa vile mambo yatawaangukia na kuwaumiza.

Katika mkutano wa Yokohama, Abe anahoji nini kifanyike na anaahidi kuwa Japan katika miaka mitatu ijayo inatarajia kufunza wataalamu 30 wa Afrika kufahamu jinsi ya kukabiliana na hatari ya madeni ya umma.

Hata hivyo, angalizo la Abe linaikumbusha Afrika mambo mengi.

### AFRIKA IFANYEJE ?

Afrika lazima itambue vipaumbele vyake, iwekeze itekeleze majukumu yake na si lazima kufuata utaratibu wa maendeleo unaofanyika Ulaya na Marekani.

Ni lazima ijiondoe kwenye utegemezi wa nchi za Magharibi, AU ijizatiti kwenye kusimamia na kuendeleza ushirikiano wa kikanda ili kuwa na mtangamano unaokuzwa na ushirika wa kikanda.

Afrika iwekeze kwenye ushirikiano wa kibiashara, ushindani wa viwanda, kilimo na kuimarisha miundombinu yake kwa utaratibu unaolifaa bara hilo na si kuigiza.

Bara la Afrika lifanikishe kuanzishwa kwa ukanda huru wa kibiashara 'Free Trade Area' na mataifa yote 54 yashiriki kwenye mtangamano huo wa kibiashara na kiuchumi badala ya kutegemea biashara na China, Umoja wa Ulaya na mipango kama ule wa Marekani wa AGOA, ambao si vitu endelevu.

Waziri Mkuu Shinzo Abe, anamaanisha kuwa hatma ya Afrika iko mikononi mwa viongozi wa bara hilo tajiri japo maskini. Ni lazima viongozi wajue kufanya mikataba ya kibiashara ya 'kijanja' wasikubali kutapeliwa na wajihusihe kwenye uwekezaji wa tija na siyo kukubali ili wapate kile wanachohitaji kwa wakati huo bila kujali athari za baadaye.

Wakitaka SGR leo, miradi mikubwa ya umeme kama wa Inga na barabara za kisasa wajue kuwa leo ni kukopa harusi lakini kesho kulipa ni matanga.

Si kwamba anawapenda sana Waafrika kila mmoja hapa anaangalia maslahi yake. Japan kupitia mkutano wa TICAD kila mwaka inaangalia namna ya kuendeleza maslahi yake na ushirikiano na Afrika.

Wakati china ina shirika la ukandarasi la China Railway Construction Corporation Limited (CRCC) linalojenga reli kila mahali, Japan nayo ina Konoike na Kajima. Kwa ujumla Afrika ijitegemee isimame yenyewe kama ina watu bilioni moja ni soko la kutosha. Izingatie mikataba yake kama ule wa Demokrasia, Uchaguzi na Uongozi (ACDEG) ,ambao ni dira inayoielekeza Afrika cha kufanya ili ifikie maendeleo ya kweli na endelevu.

Hofu ya Japan ni kwamba pengine itafika kipindi Congo na AU ikashindwa kuendesha mradi wa umeme wa Inga kulipa deni hapo , italazimika kaacha jukumu hilo kwa China isimamie uendeshaji ili kulipa fedha zake.

Aidha, Kenya na Ethiopia zikishindwa kulipa deni la ujenzi wa SGR, Serikali ya Beijing italazimika kuichukua ili kujilipa madeni yake.

Yote hayo yatahatarisha 'sovereignty' ambayo ni haki ya kila taifa kuwa huru kujiamulia mambo yake bila kuingiliwa na yeyote.

# DC Muwango: Nachingwea ni ya maendeleo kwanza, ndipo vyama

**Na Sabato Kasika**



Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea, Rukia Muwango, akiwa ofisini kwake. **PICHA: SABATO KASIKA**

MOJA ya mambo, ambayo Rais Dk. John Magufuli amekuwa akihimiza, ni watu kufanya kazi bila kubaguana kwa namna yoyote ile ikiwamo ya itikadi za vyama, kwa vile maendeleo hayana chama.

Rais anaamini kwamba viongozi huteuliwa kushika nafasi mbalimbali kutokana na uwezo wao wa utendaji kazi pamoja na uadilifu wao na pia wanatakiwa kuwasilikiza wananchi na kutatua matatizo yao.

Viongozi wanakumbushwa kuwa jukumu lao ni kusimamia kikamilifu shughuli mbalimbali za serikali zitakazochochea maendeleo ya wananchi kwa ngazi zote, wakitambua kuwa maendeleo hayana chama.

Anawashangaa baadhi ya watu wanaosema kuwa ameteua wapinzani, lakini anaamini kwamba kwa Tanzania anayoijenga ya umoja, vyama na ukabila vikitangulizwa, nchi haiwezi kufika mbali.

Kwa kuzingatia kauli hiyo ya mkuu wa nchi, wapo baadhi ya viongozi ambao wanaitekeleza kwa vitendo ili kuhakikisha wananchi kwenye maeneo yao wanafanya shughuli za maendeleo bila kubaguana kwa itikadi za vyama.

Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea, Rukia Muwango ni miongoni mwa viongozi hao, ambaye amejiwekea utaratibu wa kukutana na madiwani wa vyama vya upinzani na kuweka mikakati ya maendeleo.

Anasema upinzani wilayani mwake upo, lakini hauna nguvu sana, kwa vile unaongoza kata tisa kati ya 36.

Pamoja na ukweli huo, bado anashirikiana nao kwa vile maendeleo hayana chama.

Muwango anafafanua zaidi jinsi anavyoshirikisha upinzani kwenye shughuli za maendeleo wilayani mwake, katika mazungumzo aliyoyafanya na gazeti hili. Fuatilia mahojiano hayo:

**SWALI: Unasema unashirikisha upinzani kwenye shughuli za maendeleo, unaushirikisha vipi?**

**JIBU:** Kwanza kabisa nikuhakikishie kwamba upinzani wilayani kwetu unatambua kazi kubwa ya kuleta maendeleo inayofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano na madiwani wa kata sita wakiwamo wa Chadema na CUF wanatoa ushirikiano mkubwa kwangu, kwani ninakutana nao na kupanga shughuli za maendeleo na wanazitekeleza vyema kwenye maeneo yao. Kwa mfano, wanahamasisha ujenzi wa vyumba vya madarasa, zahanati na pia kituo cha afya cha Kata ya Namapwiya. Yaani kwa ujumla ni kwamba huku kwetu ni maendeleo kwanza vyama baadaye, kwa sababu nchi hii inajengwa na Watanzania wenyewe bila kujali itikadi za vyama vyao. Na kwa kutambua hilo tunashirikiana vizuri tu kuijenga Nachingwea yetu. Binafsi kama mkuu wa wilaya sijapata ugumu wa kusimamia shughuli za maendeleo kwenye maeneo yao, kwani ninatoa maagizo, wanatekeleza. Yaani wananipa ushirikiano mzuri tu kwa ajili ya maendeleo ya maeneo yao na Nachingwea kwa ujumla. Ninapoitisha mikutano wanahudhuria kwa wingi na wanasaidia kuhimiza wananchi kuhudhuria mikutano yangu. Ni muhimu kila mmoja wetu atambue kuwa maendeleo ya kweli hayana chama, kwani shida za kimaisha hazibagui chama. Hivyo, hatuna budi kufanya kazi kwa pamoja kama Watanzania na si kwa sababu ya kuwa wanachama wa chama fulani.

> Ninakutana nao kwenye tarafa ili kama kuna maelekezo nimeyatoa, basi viongozi wa tarafa washushe kwenye kata na wa kata washushe kwenye Serikali za Mitaa.

**SWALI: Unasema wapinzani wana kata sita ni zipi hizo?**

**JIBU:** Kata zinazoongozwa na upinzani ni Mpiruka, Marambo, Naipanga (Chadema), Mkoka, Ndomoni, Kiegei, Chiola, Namapwia na Kipara Mnero zote ziko chini ya Chama cha Wananchi (CUF). Kata zingine 27 ambazo ziko CCM ni Boma, Chiumbati Shuleni, Kilimani Hewa, Kilimarondo, Kipara, Mtua, Lionja, Matekwe na Mbondo. Zingine ni Mchonda, Mitumbati, Mkotokuyana, Mnero Miembeni, Mnero Ngongo, Mutua, Nachingwea Mjini, Naipingo na Namatula.

Aidha kata za Nambambo, Namikango, Nang'ondo, Nangowe, Nditi, Ngunichile, Raha leo, Ruponda, Stesheni na Ugawaji. Hata hivyo, hatuwezi kudharau uwakilishi na mawazo yao yanayohusu maendeleo ya wilaya yetu. Sisi sote ni wana Nachingwea na kimsingi maendeleo hayana chama.

**SWALI: Ni njia gani unazotumia kutatua kero za wananchi?**

**JIBU:** Binafsi nimejiwekea utaratibu wa kukutana na wananchi Alhamisi ya kila mwisho mwezi nikiwa na wakuu wa idara zote na taasisi za Serikali kusikiliza kero zao, huwa ninakwenda kila tarafa. Hapa kwetu tuna tarafa tano za Kilimarondo, Naipanga, Nambambo, Lionja na Ruponda. Ninakutana nao kwenye tarafa ili kama kuna maelekezo nimeyatoa, basi viongozi wa tarafa washushe kwenye kata na wa kata washushe kwenye Serikali za Mitaa. Lengo ni kuhakikisha wananchi wote wanapata taarifa au maelekezo kutoka kwa mkuu wao wa wilaya. Lakini lengo la kutembea na wakuu wakuu wa idara na taasisi za Serikali ni kutaka kila mmoja ajibu kero za wananchi kama zitaelekezwa kwake na mwisho wa siku kama kuna tatizo basi linapatiwa ufumbuzi kama utakuwa ni wa hapo hapo au kusubiri. Njia hiyo imesaidia kuwa karibu na wananchi, kwa kuzingatia kwamba kuongoza ni kuelekeza na pia siyo kukaa ofisini tu bali kufika kwa wananchi ili kusikiliza kero zao. Siishii hapo tu bali pia pamoja na viongozi wenzangu wakiwamo wanasiasa wanafanya kazi ya kuelimisha wananchi kutambua umuhimu wa Daftari la Kudumu la Mpigakura ili hatimaye litakapofika hapa wajitokeze kwa wingi kujiandikisha na hatimaye waweze kushiriki katika uchaguzi ujao. Kazi hii ya kuhamasisha inafanywa na wanasiasa wa vyama vyote, kwani kama nilivyosema, maendeleo hayana chama... kuhamasisha wananchi kwa ajili ya kujiandikisha kwa lengo la kupiga kura ni hatua mojawapo ya kuwatambua viongozi watakaosimamia shughuli za maendeleo kwenye maeneo yao.

**SWALI: Kiutaratibu wewe ndiye mwenyekiti wa kamati ya ulinzi na usalama wilayani mwako. Je, hali ya usalama Nachingwea ikoje?**

**JIBU:** Nachingwea ni shwari kabisa na suala la udokozi mdogo mdogo unaofanywa na baadhi ya vijana wasiotaka kufanya kazi siwezi kulichukulia kwamba linahatarisha usalama wetu. Kwa hiyo Nachingwea ni shwari kabisa, askari wanafanya kazi vizuri kuhakikisha wakati wote watu wanakuwa salama. Lakini pamoja na usalama huo, hatuwezi kubweteka bali tunaendelea kuimarisha ulinzi, na ninakuhakikishia kuwa Nachingwea ni miongoni mwa wilaya ambazo hazina changamoto za vitendo vya uhalifu. Kwa sababu kila ninapokutana na wananchi pamoja na mambo mengine, huwa siachi kuhimiza suala la usalama na wananchi katika maeneo yao wameunda vikundi ambavyo vinahakikisha wananchi wanaishi kwa amani. Ikumbukwe kuwa shughuli za maendeleo haziwezi kufanyika iwapo hakutakuwa na usalama, hivyo kwetu usalama ni jambo la kwanza ndio maana tupo shwari.

# Wafuasi wa Trump Italia wajitoa serikalini, waingia rasmi upinzani



Matteo Salvini, aliyekuwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Mambo ya Ndani wa Italia, ambaye amesababisha serikali nchini humo kuvunjika na kujiuzulu kwa Waziri Mkuu Guiseppe Conte. **PICHA: MTANDAO**

**Na Anil Kija**

WAFUASI wa Rais Donald Trump wa Marekani ambao walikuwa sehemu ya serikali ya pamoja ya mrengo wa kulia wamelazimisha kuvunjwa kwa Serikali iliyokuwapo madarakani tangu Juni 1 mwaka jana.

Wanaongozwa na Matteo Salvini, aliyekuwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Mambo ya Ndani aliyesababisha kujiuzulu kwa Waziri Mkuu Guiseppe Conte, mtaalamu wa uchumi asiyekuwa kiongozi wa mojawapo kati ya vyama vilivyounda Serikali.

Alitaka ufanyike uchaguzi mkuu kwa haraka, na kwa vile alishinda viti vingi uchaguzi wa Bunge la Ulaya, akadhania kuna uwezekano wa kuukwaa uwaziri mkuu. Sasa imeundwa Serikali nyingine.

Conte alitangaza kujiuzulu hapo Agosti 20, ikiwa ni miezi 17 tangu kufanyika uchaguzi mkuu mwezi Machi mwaka jana ambako chama cha Salvini, The League (kilichoanza kama Northern League alikozaliwa, jijini Milan, halafu kikafungua vyama shirika maeneo mengine ya Italia) kilipata 265.

Lakini kwa vile ni mkusanyiko wa vyama, ikabidi waunde Serikali wakishirikiana na Five Star Movement (M5S), chama kingine cha mrengo wa kulia kilichopata viti 227 bungeni.

Sasa M5S imeafikiana kupitia mchakato uliosimamiwa na Rais Sergio Matarella kuunda Serikali na Democratic Party, chenye siasa za kati/kushoto kwa kiasi, kuiacha siasa kali ya League, Liga.

Katika Serikali iliyoundwa Juni 1, 2018, miezi takriban mitatu baada ya uchaguzi wa Bunge, mwanachama wa Five Star Movement, Profesa Guiseppe Conte aliteuliwa kuwa waziri mkuu na viongozi wa vyama hivyo viwili kuwa manaibu mawaziri wakuu.

> Salvini aliitisha kura bungeni ya kutokuwa na imani na umoja wa vyama ulioko madarakani, kufuta matumaini ya wahafidhina kuwa utadumu.

Hapo ndiyo kumekuwa na mzizi wa fitina, kuhusu nini kifanyike, nani amshauri waziri mkuu kuhusu uteuzi wa waziri huyu au yule, au kubadilisha mawaziri inapobidi, kutokana na mivutano inayotoka bungeni na miongoni mwa makundi yanayowaunga mkono.

Salvini aliitisha kura bungeni ya kutokuwa na imani na umoja wa vyama ulioko madarakani, kufuta matumaini ya wahafidhina kuwa utadumu.

Serikali mpya iliyoundwa ina uwezo wa kisheria wa kukaa madarakani hadi 2023 ambako lazima ufanyike uchaguzi mkuu, hali inayomfanya Salvini, aliyekuwa na uchu mkubwa wa kutwaa madaraka, kuanza kuzoea maisha mapya ya upinzani.

Baadhi ya wachunguzi wa habari wanaamini kuwa hali hiyo itampa mwanga mpya wa jinsi ya kutawala, yaani kufikia makubaliano na kuyalinda hadi wakati uliopangwa wa kufanyika uchaguzi mkuu.

Kinyume chake ni kuangalia upepo uone kuwa chama chako kinaungwa mkono zaidi, uvunje Serikali ili utawale.

Bado kuna mtihani si mdogo katika kuundwa Serikali ya kujumuisha Five Star Movement na Democratic Party, kwani Five Star imeundwa kufumua 'business as usual' (hulka za kawaida) katika uendeshaji wa Serikali.

Kimsingi ni chama kinachobeza utawala na taratibu zake, kujali makundi ya washikadau asilia katika siasa za Italia wakati PD ni kielekezo cha taratibu na hulka hizo.

Ila kwa vile wote wanataka kuelekeza Serikali upande huu au ule katika kile wanachodhania ni muhimu kwa Italia kufuata, watajitahidi kubaki madarakani kwa kutegemea kufanikiwa, kila mmoja kwa mwelekeo wake.

Hapo ndipo baadhi ya wachunguzi wanaona haitazamiwi Serikali hiyo ikabaki madarakani miaka minne kwani tofauti zao ni nyingi, na suala la kukubaliana na Umoja wa Ulaya.

Salvini alikataa mapendekezo ya EU kupunguza matumizi, kupunguza kodi.

Aliungwa mkono na Conte, ambaye ni mwanasiasa huru anayeendana na Five Star, lakini PD inajua haina njia inayoweza kukwepa kushirikiana na Five Star, kwani ina wingi wa asilimia 17 tu bungeni, wakati Five Star wana asilimia 32.

Ina maana wakiungana wanaweza kuunda serikali yenye asilimia 49 ya viti bungeni; siyo wingi kamili lakini wapinzani wao, licha ya kuwa na asilimia moja ya ziada, hawawezi kuungana kwa suala lolote ili kuweza kuiangusha Serikali na kulazimisha uchaguzi mkuu.

Hata hivyo, tofauti zao zinatazamiwa kumsaidia Salvini ashamiri.

Moja ya maeneo nyeti katika kuundwa Serikali mpya ilikuwa ni nafasi ya kiongozi wa Five Star, Luigi Di Maio ambaye alikuwa naibu waziri mkuu katika serikali iliyotangulia hadi kufikwa na kashfa ya 'mipango' yenye ladha ya rushwa au uwakala kwa niaba ya Russia.

Ni nchi yenye ushindani mkali na Umoja wa Ulaya na inapendelea vyama vya mrengo mkali wa kulia, wa kizalendo nchini Italia ili kupunguza ushawishi wa EU nchini humo. Bado hana ushawishi wa kutosha hata kwa wanachama wa Five Star, kiasi kwamba Waziri Mkuu Conte anaonekana ndiye kiongozi halisi wa chama hicho.

PD ilikataa kata kata Di Maio kuwa waziri wa Mambo ya Ndani, ikisema kuliko hatua hiyo ifikiwe majadiliano yangeisha; uchaguzi mkuu mwingine ungeitishwa.

Ina maana kuwa sasa kuna viongozi wawili wa vyama vya siasa ambao kwa mbali au karibu wangependa kuangusha Serikali iliyoundwa kati ya chama cha mrengo wa kulia na wa kati/kushoto.

Wa kwanza anayetaka ianguke ni Salvini ambaye chama chake ni kikubwa zaidi bungeni na si ajabu ushawishi wake umeongezeka kutokana na kuikatalia EU kata kata kuhusu mipango yake ya Bajeti, wakati PD inatazamia kuelewana na EU kwa kiwango kinachoridhisha.

Mwingine mwenye usongo kiasi fulani kuanguka Serikali hii, bali angoje hadi ushawishi wake binafsi uongezeke mbeleni, ni Di Maio, ila atapata wakati mgumu kumfunika Conte.

Hata hivyo, suala hilo linategemea mazingira ya kisiasa kwani Di Maio ni mpambanaji, na Conte aliletwa tu.

Wachunguzi wa habari wanasema wafuasi wa Salvini, ambao ni mashabiki wakubwa wa mwelekeo wa kisiasa na mtindo wa kutawala wa Rais Trump, walikuwa wanajenga kampeni ya uchaguzi wakisisitiza umuhimu wa kurudisha Ulaya ya Kikristo.

Wanasema makundi ya wanaharakati wa kidini nchini Marekani, yaani makundi ya wahubiri wa makanisa huru, wamechochea kwa nguvu kuzuka kwa mwelekeo wa kijadi katika vyama vya siasa barani Ulaya, wasiopenda taasisi kama Umoja wa Ulaya zinazosimamiwa kiliberali au kiutandawazi.

Hata hivyo, baadhi wanasema haitakuwa rahisi kwa Salvini kufaulu katika lengo lake la kuukwaa uwaziri mkuu kupitia uchaguzi mkuu mwingine, yaani apate ushindi wa kutosha.

Katika wiki za karibuni Salvini alikuwa akitoa ishara mchanganyiko kuhusu dhamira yake kisiasa, huku akisema siyo wakati wa Italia kurudi tena katika kampeni na kupiga kura, halafu akitoa maelekezo kwa Waziri Mkuu Conte kuhusu mawaziri wa kubakizwa na wa kuondolewa.

Moja ya sababu zilizotajwa katika majarida kadhaa ni mwito wa Conte kutaka vyama vya siasa na makundi ya kijamii yasitumie alama za dini katika harakati zao, kwani zinavuruga kanuni ya mfumo wa kisasa wa utawala, ambao unatenganisha dini na siasa.

Akitofautiana naye, Salvini alibusu rozari huku serikali ikianza kuanguka.

Ulipaji wa riba na sehemu zilizoiva za deni la Italia katika Umoja wa Ulaya lilikuwa suala muhimu, ambako Salvini alitaka kodi zipunguzwe kwa euro bilioni 10 (dola bilioni 11).

Ni pendekezo ambalo alilitoa akijadiliana na mawaziri wa Umoja wa Ulaya, wakalikataa kwa nguvu. Alisimama kidete; hilo litaisumbua Serikali hii, wakijua kuwa Salvini ana msimamo mkali wa kutokutaka Italia ichezewe na wasomi Brussels.

Ina maana EU ikifikia maafikiano na Italia itakuwa inajua kuwa ni ya muda, ya vyama dhaifu.

# Tarura yatakiwa kujenga daraja kabla mvua

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

KAMATI ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Wilaya ya Mbeya Vijijini, imemwagiza Meneja wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura), kuharakisha ujenzi wa daraja la Idiwili kabla msimu wa mvua haujaanza ili kuwaondolea kero wananchi hao.

Kamati hiyo ikiongozwa na Mwenyekiti wa Chama hicho wilaya, Hakimu Mwalupindi na Mkuu wa Wilaya hiyo, William Ntinika, ilitoa agizo hilo juzi ilipokuwa kwenye ziara ya kukagua miradi ya maendeleo.

Mwenyekiti wa chama hicho, Mwalupindi alisema daraja hilo liliharibika miaka miwili iliyopita kutokana na mafuriko na hivyo kuwakoseha mawasiliano wananchi wa Kijiji cha Idiwili.

Alisema mradi huo umechukua muda mrefu na unaelekea kuwa kero kwa wananchi hivyo wao kama wasimamizi wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama hicho lazima wahakikishe wanawasimamia watekelezaji kikamilifu.

"Wananchi wamechoshwa na ahadi ambazo wamekuwa wakiahidiwa mara kwa mara, wanahitaji kuona vitendo na sisi lazima tuisukume serikali kufanya vitendo," alisema Mwalupindi.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Ntinika alisema daraja hilo limekuwa likisababisha wananchi kushindwa kuiamini serikali yao kwa madai kuwa awali lilikuwa limekamilika, lakini likabomoka muda mfupi.

Alisema kulikuwa na changamoto ya baadhi ya watendaji wa serikali katika usimamizi wa mradi na hivyo akamtaka Meneja wa Tarura Wilaya kuhakikisha wanakamilisha haraka mradi huo ili wananchi waanze kulitumia.

Alisema daraja hilo ni kiungo muhimu cha wananchi wa kijiji hicho na vijiji vingine vya Kata ya Isuto pamoja na Makao Makuu ya Wilaya hiyo ambako ndiko wananchi hao wanapata huduma.

"Daraja hili linatumiwa na wananchi hawa katika kusafirisha mazao yao kupeleka kwenye soko na hata wanapotaka kupata huduma katika makao makuu ya wilaya lazima wapitie hapa, sasa linapochelewa kukamilika inakuwa kikwazo kwao," alisema Ntinika.

Mwakilishi wa Meneja Tarura, Allan Mhauka, alisema ujenzi wa daraja hilo utaanza muda wowote watakapokuwa wamepokea fedha kutoka Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na kwamba kwa sasa fedha hizo hazijatoka.

# Bil. 1.4/- za wakulima wa mpunga zayeyuka

**Na Nebart Msokwa, MBARALI**

SHILINGI bilioni 1.4 za chama cha ushirika cha wakulima wa mpunga Madibira katika Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya hazijulikani zilipo, huku Wizara ya Kilimo ikituhumiwa kutolishughulikia suala hilo licha ya kuwa na taarifa.

Imedaiwa kuwa kati ya fedha hizo Sh. milioni 800 ni mali ya wanachama wa chama hicho na Sh. milioni 600 ziliwekezwa na Serikali Kuu kwa ajili ya kuwakopesha wakulima hali iliyowalazimu wananchi hao kuiomba kuingilia kati.

Upotevu wa fedha hizo uliibuliwa na mmoja wa wanachama wa chama hicho, Justine Mwandumbya, kwenye mkutano wa wadau wa maendeleo wilayani Mbarali ambao ulihudhuriwa pia na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila.

Mwandumbya alisema, wanachama wa chama hicho pamoja na serikali waliwekeza fedha nyingi, lakini kwa sasa hawajui hatima yao na kwamba wameanza hata kukosa mitaji kwa ajili ya kuendeleza kilimo cha mpunga.

"Tunakuomba Mkuu wa Mkoa utusaidie kama kuna jambo linaendelea kuhusu hesabu za fedha hizo basi tujue kwa sababu zimekaa muda mrefu na naamini wewe ulipewa taarifa za juu juu, lakini ukweli ni kwamba hatujui hatima ya fedha hizo," alisema Mwandumbya.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, alisema suala la upotevu wa fedha hizo lilifikishwa katika Wizara ya Kilimo kupitia kwa aliyekuwa Naibu Waziri wake, Dk. Mary Mwanjelwa, ambaye kwa sasa ni Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Alisema baada ya Dk. Mwanjelwa kupewa taarifa hiyo, alimtuma mrajisi wa vyama vya ushirika kwa ajili ya kulishughulikia, lakini mpaka sasa hawajawahi kuletewa mrejesho wowote waliopewa kuhusu kile kilichobainika. "Tangu hapo hakuna chochote kilichoendelea, kwa hiyo suala hilo bado lipo wizarani na wao ndio wanaokwamisha maana hakuna hatua walizochukua juu ya chama hicho," alisema Mfune.

Akizungumzia suala hilo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Chalamila alisema ofisi yake imelichukua na italifanyia kazi kwa ngazi ya mkoa na kwamba endapo Wizara ya Kilimo itaendelea kuwa kikwazo atalifikisha kwa Rais Dk. John Magufuli.

Alisema kitendo cha watendaji wa Wizara ya Kilimo kulifumbia macho suala hilo kinaleta wasiwasi kuwa yawezekana na wao walihusika katika kuzitafuna fedha hizo.

"Kwanini wakae kimya kama hawahusiki, zama hizi ni za uwazi na ukweli kwa maana ya moja ni moja na mbili ni mbili, kwahiyo sisi tutalishughulikia ngazi ya mkoa na tukishindwa tutalifikisha ngazi za juu," alisema Chalamila.

Alisisitiza kuwa fedha zinazotajwa ni nyingi na zingewekezwa kama ilivyokuwa imekusudiwa zingekuwa zimezalisha kwa kiwango kikubwa na kuwanufaisha wakulima wa chama hicho.



Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani (wa pili kulia), akitoa maelekezo baada ya kutembelea chumba cha kujifungulia wajawazito katika Kituo cha Afya cha Ihalula katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe mkoani Njombe jana, baada ya kuwasha umeme katika zahanati hiyo. **PICHA: WN**

# Chama cha wakulima chaishtaki serikali fidia

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

CHAMA cha Ushirika wa Wakulima cha Luhanga Amcos cha jijini Mbeya, kimeishtaki serikali katika Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Mbeya, kikidai kulipwa zaidi ya Sh. milioni 979 kama fidia baada ya wanachama wake kunyang'anywa ardhi ya mashamba yao yenye ukubwa wa hekta 5000.

Ardhi ambayo wanachama hao wanadai kuporwa na serikali ipo katika Kata ya Luhanga wilayani Mbarali ambayo mwaka 2016, aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Amos Makalla, aliagiza ichukuliwe na kugawiwa wananchi.

Kufuatia uamuzi huo wa Mkuu wa Mkoa, wanachama wa Luhanga Amcos, waliamua kufungua kesi Mahakama Kuu wakitaka walipwe fidia na serikali.

Katika hati ya mashtaka, wanachama hao wanadai walipwe fidia ya upimwaji wa ardhi hiyo inayofikia zaidi ya Sh. milioni 14 na gharama za kufanya utafiti wa kupata chanzo cha maji kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji zinazofikia Sh. milioni 40.

Katika madai hayo wanachama hao pia wanahitaji walipwe fidia ya gharama za ujenzi wa ofisi ya Kijiji cha Luhanga kiasi cha Sh. milioni 123 pamoja na gharama za ununuzi wa samani za ofisi hiyo kiasi cha Sh. 1,656,000.

Pia wanachama hao wanadai mahakamani kuwa walijenga barabara yenye urefu wa kilometa 15 kwa kiwango cha changarawe kutoka Kijiji cha Luhanga hadi shambani kwa gharama za Sh. milioni 45.

Kwa mujibu wa hati ya mashtaka, wanachama hao wanadai kuwa walianza ujenzi wa mabwawa mawili kama chanzo cha maji ya kilimo cha umwagiliaji katika maeneo ya Udinilo na Tambalare katika kijiji cha Luhanga na kila bwawa liligharimu Sh. milioni 60, hivyo katika eneo hilo wanahitaji walipwe fidia ya Sh. milioni 120.

Wanachama hao wanadai kuwa katika uamuzi wa kupora ardhi yao uliofanywa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya Aprili 4, 2016, hakueleza kuwa gharama hizo ambazo tayari walikuwa wamezitumia zitalipwa na nani, hivyo wanaiomba mahakama iamuru serikali kuwarejeshea gharama zao.

Wanachama wa Luhanga Amcos katika kesi hiyo wanawakilishwa na Wakili Msomi, Victor Mkumbe, dhidi ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Jana ilitajwa mbele ya Hakimu Mkazi wa Mkoa wa Mbeya, Zawadi Laiser, ambaye alidai kuwa Jaji anayepaswa kusikiliza kesi hiyo kwa sasa ana majukumu mengine na atakuwa tayari kuanza kuisikiliza Oktoba 2, mwaka huu.

Mwaka 2016, aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Amos Makalla, alichukua uamuzi wa kutaifisha ardhi ya wanachama wa Luhanga Amcos, iliyopo Kata ya Luhanga wilayani Mbarali na kuamuru igawiwe kwa wananchi kwa madai kuwa ushirika huo haukufuata sheria katika kununua ardhi hiyo kwenye Serikali ya Kijiji na kujimilikisha.





# Madiwani wanawake waupinga mfumo dume uchaguzi S/Mitaa

**Na Peter Mkwavila, CHAMWINO**

MADIWANI wa Viti Maalum kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) Jimbo la Mtera na Chilonwa, wamewataka wanaume kuacha mfumo dume kwa wake zao kwa kuwanyima nafasi za kugombea katika uchaguzi wa serikali za mitaa.

Akizungumza na waandishi wa habari kwa niaba ya madiwani wenzake wa viti maalum, Hilda Kadunda, alisema kumekuwapo na tabia kwa wanaume wenye tabia ya mfumo dume ambao umekuwa ukiwanyima haki ya msingi ya kugombea nafasi mbalimbali za uongozi zinapotokea.

Alisema wanawake wana uwezo wa kuongoza, lakini wanaume wanawanyima haki hiyo ya msingi kuwa viongozi kwa dhana potofu kuwa watakuwa wakifanya mambo mabaya tofauti na malengo aliyogombea nafasi hizo.

"Kimsingi imani kama hiyo ya mfumo dume imepitwa na wakati ukizingatia kuwa wanawake wanaweza, tena ni wabunifu, hivyo ni muhimu wakapewa nafasi za kuongoza kwa kuwa watakuwa wanafuata kanuni na misingi bora ya chama husika anachogombea," alisema.

Aliwataka wanawake wajishughulishe kwenye ujasiriamali ikiwamo shughuli zinginezo zitakazowaletea mapato ya kiuchumi ili waweze kuaminiwa na wanaume ambao wanaofikiri kuwa kinamama ni dhaifu.

Naye Diwani wa Dabalo (viti maalum), Fatuma Semninga, aliwataka wanawake wenye sifa ya uongozi kutowaachia wanaume kugombea peke yao na wao kuishia kuwafanyia kampeni, badala yake wajitokeze kwa wingi ili kuzishika nafasi hizo ambazo ni muhimu pia kwa kinamama.

Alisema badala ya kuishia kuwapigia kampeni wanaume kwenye uchaguzi huo wa serikali za mitaa, ni wakati wao pia kujitokeza kwa wingi kugombea na kupiga kura.

"Nawaomba wanawake wenzangu wa majimbo ya Chilonwa na Mtera mjitokeze kwa wingi ikiwamo kupiga kura, badala ya kutumiwa kufanya kampeni kwa wagombea wengine, ni wakati sasa wakatumia fursa hiyo wakachukua hatua ya kugombea," alisema.

Aidha, aliwataka wanawake kuunda vikundi vitakavyowawezesha kukukopeshwa ili waweze kupata mikopo itakayowawezesha kujiinua kiuchumi.



Mkuu wa Wilaya ya Bariadi, Festo Kiswaga (kulia), akikagua nyumba za wananchi zilizobomolewa na tembo katika kijiji cha Halawa wilayani humo, mkoani Simiyu, juzi. **PICHA: HAPPY SEVERINE**

# Watakiwa kutembelea vivutio vya utalii

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

WATANZANIA wametakiwa kujenga desturi ya kutembelea vivutio vya utalii nchini ili kujua thamani iliopo ndani ya hifadhi zilizopo, badala ya kusubiri wakati wa maonyesho pekee.

Hayo yalibainishwa na mhifadhi kutoka Idara ya Utalii ya Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, Filimon Temu, wakati akizungumza na gazeti hili kuhusiana na idadi ndogo ya watu wanaokwenda kutembelea hifadhi za taifa.

Temu alisema Watanzania wengi hawana desturi ya kutembelea mbuga za wanyama jambo linalopelekea wengi kushindwa kujua vivutio vilivyopo ndani ya hifadhi ambazo zinajumuisha wanyamapori.

Alisema hivi sasa jamii inapaswa kuwa na mwamko wa kutembelea katika vivutio vya utalii kutokana na idadi ya hifadhi kuongezeka kutoka hifadhi 16 hadi 21 ambapo kila mmoja kwa nafasi yake anapaswa kwenda kutembelea hifadhi ilio jirani na eneo analotoka ili kujua thamani ya utalii uliopo ndani ya nchi.

"Unakuta mtu hajui tuna hifadhi ngapi au haelewi vivutio vilivyopo kwenye mbuga zilizopo ndani ya hifadhi zetu, lakini mtu kutoka nje ya nchi anajua," alisema Temu.

Alisema jamii inapaswa kuamka na kuwa mabalozi wa wageni wanaowasili kuja kutembelea hifadhi zilizopo ikiwamo kuwasimulia thamani na uzuri wa vitu vilivyopo, jambo ambalo litasaidia kuongeza idadi ya watalii katika mbuga za wanyama na hifadhi nyingine ambazo zina vivutio vya kale.

"Kitendo cha kusubiri wakati wa maonyesho ndipo mjitokeze kuona wanyama kinarudisha nyuma sekta ya utalii na wingi wa jamii inavyojitokeza, wakati wa maonyesho inapaswa kuwa mwendelezo wa kila mara pale unapopata nafasi ya kutembelea," alisema.

Aliwataka wakazi wa Jiji la Dodoma kufanya jitihada za kutembelea hifadhi zilizopo Kanda ya Kusini ili kusaidia kutangaza hifadhi hizo ili watu wazijue kama ilivyo zile za Kanda ya Kaskazini.

Temu alisema wageni wengi wakija hujua hifadhi ni moja tu ambayo ni Serengeti kutokana na watu wa kanda hiyo hupenda kutembelea, jambo linalofanya watu wajue hiyo ndio hifadhi pekee wakati nyingine zipo.

Kutokana na hilo, alisema jamii iliopo Kanda ya Kusini kati na nyingine zijenge utaratibu wa kutembelea hifadhi za wanyama zilizopo Kanda ya Kusini ili kusaidia kuzitangaza hifadhi zetu.

## Vijana waitiwa mikopo h/shauri

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, amewataka vijana kuchangamkia mikopo inayotolewa na halmashauri ili kujikwamua kiuchumi.

Katambi aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusiana na asilimia 10 ya mikopo iliotengwa na serikali kwa ajili ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

Katambi alisema vijana wanapaswa kujitokeza kuchangamkia fursa hizo za mikopo kwa ajili ya kuanzisha taasisi mbalimbali ambazo zitawasaidia kujikwamua kiuchumi.

Alisema vijana wanapaswa kujipanga ikiwamo kupanga mikakati ya kile wanachotaka kufanya ili kujitokeza kuchangamkia fursa za mikopo inayotolewa na halmashauri. "Vijana mnapaswa kuchangamkia fursa za mikopo ambazo zinatolewa lengo ni kuinua vijana kiuchumi," alisema Katambi.

Alisema mikopo ya halmashauri imetengwa kwa ajili ya kuwasaidia makundi ya aina hiyo na kuwataka vijana kuchangamkia fursa hiyo ambayo ni muhimu kwao kwa ajili ya kufanya maendeleo.

Alisema anashangazwa kuona vijana hawajitokezi kwa ajili ya kuchangamkia fursa hizo za mikopo.

Mbali na hilo amesisitiza suala zima la watu kujiunga na Mfuko wa Bima ya Afya ya Jamii (CHF) itawasaidia kupata matibabu haraka hata kama hawana pesa mkononi.

Alisema bima hiyo ni muhimu hivyo kila mmoja anapaswa kuwa na kadi ya bima ambayo ni muhimu kwa ajili ya afya yao.

"Kadi ya bima ya afya ni muhimu kwa jamii hivyo mnapaswa kukata bima hiyo kwa gharama nafuu ambayo unaweza kwenda kutibiwa wewe na familia yako," alisema Katambi.

Alisema lengo la serikali ni kuona jamii yote inakuwa na kadi za bima ya afya ambazo ni muhimu kwa ajili ya afya yao.

Alisema mfuko wa CHF iliyoboreshwa umewarahisishia wananchi gharama lengo ni kuona kila mmoja anakuwa na bima ya afya ambayo inamrahisishia kupata matibabu hata kama hana pesa mfukoni.





Wakulima wa zao la shokishoki katika kijiji cha Donge Karange, mjini Zanzibar wakiwa katika harakati za uvunaji wa zao hilo, juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Watalii wapaisha uchumi Zanzibar

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WIZARA ya Fedha na Mipango imeeleza kuwa ongezeko la idadi ya watalii walioingia visiwani hadi kufikia 520,809 kumechangia kuinua na kukuza uchumi wa Zanzibar kwa kiwango kikubwa.

Kwa mujibu wa wizara hiyo, watalii walioingia nchini walikuwa 520,809 kwa mwaka 2018, kutoka watalii 433,474 waliorekodiwa mwaka 2017 sawa na ongezeko la asilimia 20.1.

Sekta hiyo imeongeza pato la taifa na kukua kwa uchumi wa Zanzibar, kwa mujibu wa Waziri wa Fedha, Balozi Mohamed Ramia Abdiwawa.

Aliyasema hayo, Ikulu mjini Zanzibar wakati wizara hiyo ilipowasilisha taarifa ya utekelezaji wa bajeti pamoja na mpango wa utekelezaji wake kwa mwaka 2019/2020.

Alieleza kuwa kwa mwaka 2018 uchumi wa Zanzibar umeendelea kuwa imara kwa kuongezeka kwa pato halisi la taifa pamoja na kushuka kwa kasi ya mfumko wa bei za bidhaa na huduma nchini na kufikia wastani wa asilimia 3.9 mwaka 2018 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 5.6 mwaka 2017.

Ramia alisema kuwa kuimarika kwa pato la taifa na ukuaji wa uchumi pia, kumechangiwa na kuendelea kuwa tulivu kwa thamani ya shilingi dhidi ya Dola ya Kimarekani kwa asilimia 1.6.

Alisema kuwa wakati serikali ikiendelea kutekeleza dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2020, Tume ya Mipango imeanza matayarisho ya dira mpya itakayotoa mwelekeo kwa kipindi kirefu kijacho kuanzia mwaka 2021 hadi 2050.

Alieleza kuwa mwelekeo mpya na vipaumbele vya uchumi wa Zanzibar wa uwezekano wa kuwapo kwa mafuta na gesi, mabadiliko ya sera na mipango ya kimataifa, mageuzi ya sayansi na teknolojia na mabadiliko ya tabianchi yanahitaji sera na mikakati mipya ya kusimamia na kutekeleza mipango ya maendeleo.

Alieleza kuwa ujenzi wa uwanja wa ndege wa Abeid Amani Karume ni lazima utafanyika na serikali imejipangia pamoja na miradi mengine, kuwa itajenga Bandari ya Mpigaduri.

Alisema kuwa viashiria vyote vinaonyesha kwamba uchumi wa Zanzibar ni imara na unakuwa kwa kasi kubwa kutokana na ufuatiliaji uliofanyika.

Rais Dk. Mohamed Shein, aliupongeza uongozi wa wizara hiyo pamoja na watendaji wake wote kwa kuwasilisha vyema mpango kazi na kuutaka kuongeza kasi na kufanya kazi kwa bidii ili mafanikio zaidi yaendelee kupatikana.

Dk. Shein alieleza kuwa zoezi hilo la mikutano ya utekelezaji wa mpango kazi linasaidia kwa kiasi kikubwa kuwapa fursa watendaji na viongozi kuzifahamu vyema taasisi zao.

"Kama Wizara ya Fedha haitafanya wajibu wake hakuna litakaloendelea, kwani lolote tunalotaka kulifanya ni lazima lipate fedha na pesa hizo hutafutwa na hiyo ndiyo kazi yenu," alisema Dk. Shein.

Aidha, alisema kuwa iwapo uwajibikaji utakwenda kama ilivyopangwa, mafanikio zaidi yanapatikana na kuupongeza uongozi wa wizara hiyo kwa kufanya wajibu wao na kusisitiza kuwa kila wizara ikitekeleza vyema wajibu wake mapato yataongezeka.

# Aeleza umuhimu wa kujua mambo ya kale

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAZIRI wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale, Mahmoud Thabit Kombo, amesema Wazanzibari wanahitaji kujua mambo mengi ya kale ili waweza kufahamu historia ya nchi yao.

Akizungumza wakati wa makabidhiano ya jengo la kihistoria la Bi Hole lililoko huko Bungi baada ya kufanyiwa ukarabati mkubwa, alisema hali ya jengo hilo hivi sasa ni ya ubora wa hali ya juu na amewataka wananchi kujenga utamaduni wa kutembelea sehemu za historia.

Maeneo hayo ni kama Bi Hole, Dunga, Mkandamume, Fukuchani na Mvuleni ili kuendeleza utalii wa ndani.

Alisema lengo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuweka idara maalum inayoshughulika Mambo ya Kale ni moja ya njia ya kuwekeza na kukuza uchumi hasa ukizingatiwa kwamba Zanzibar ina utajiri mkubwa wa mambo ya kale.

Aidha, alisema sehemu hiyo itakapokamilika itakuwa na uwezo mkubwa wa kupokea wageni na wenyeji watakaotembelea na kutakuwa kuna mvuto kama ilivyo kwa Forodhani na Fumba.

"Eneo hilo likikamilika linatarajiwa kuwa na mambo mengi yaliyo mazuri ikiwamo sehemu ya kupumzikia, biashara za vyakula, burudani ili kuweka mazingira bora pahala hapo," alisema Waziri Kombo.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari na Mambo ya Kale, Khadija Bakari, alisema serikali inafanya juhudi kubwa kwa makusudi ili kuimarisha majengo ya mambo ya kale na kuwa vivutio vya kukuza utalii.

Hivyo aliwaomba watakaokuwa wanashughulikia jengo hilo kuhakikisha wanaweka ulinzi ulio imara ili jengo hilo lisichafuliwe na liweze kudumu kwa muda mrefu.

"Nawaomba walinzi kuwa imara na kuhakikisha jengo hili isiwe watu wanaingia na kutoka na lisichafuliwe kwa makusudi ili liendelee kupendeza pia liweze kufanya kazi kwa muda mrefu," alisema Katibu huyo.

Kwa upande wake mhandisi wa kampuni ya Azim iliyojenga jengo hilo Abdullah Omar alisema ujenzi huo umeanza mwaka mmoja uliopita na mambo yote waliyokubaliyana kwenye mkataba yamemalizika.

Mradi huo wa jengo la Bi Hole hadi kukamilika umegharimu Sh. milioni 800 ambazo zimetolewa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

## Zanzibar kuanzisha jumuiya ya mawakili

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

KATIBU Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria Zanzibar, George Kazi, amesema jumuiya ya mawakili ni chombo cha wasomi wa sheria ambao wana mchango mkubwa katika masuala ya kusimamia sheria na kutetea na kutoa haki kwa jamii.

Alisema kukosekana kwa sheria zisizo rasmi zinazosimamia kazi za mawakili kumesababisha matatizo mengi ikiwamo kukosekana uwakilishi mzuri na wenye weledi kwa wananchi wanaohitaji kusaidiwa kwenye vyombo vya sheria na ushauri wa kisheria.

Aliyasema hayo huko Gombani Chakechake Pemba alipokuwa akitoa maelezo ya mapendekezo ya kuanzishwa kwa Jumuiya ya Mawakili Zanzibar kwa wajumbe wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Baraza la Wawakilishi.

Alisema miongoni mwa mapendekezo ya sheria za mawakili yanalenga kutatua kasoro zilizopo katika usimamizi wa mawakili kwa kuweka mifumo ilio rasmi kulingana na mahitaji, sambamba na kutojihusisha na masuala ya kisiasa. Akiwasilisha rasimu ya Sheria ya Jumuiya ya Mawakili, Mkurugenzi Idara ya Uandishi wa Sheria na Sera za Kisheria , Saleh Said Mubarak, alisema miongoni mwa sheria hizo ni kuiendeleza amani, umoja na mshikamano katika kusaidia masuala ya kikatiba, haki na utawala wa kisheria. Aidha ni kuhakikisha upatikanaji wa haki na kuzingatia maslahi ya umma na taifa na haki za binadamu kwa jumla.

Akifunga mkutano huo Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum za SMZ, Machano Othman Said, alisema wananchi wanawategemea sana wanasheria katika kupata haki zao, hivyo ni vyema wakazifuata taratibu zote zilizowekwa katika muswada huo ili kuepusha migongano kati ya wateja wao na serikali.

"Wananchi wamekuwa wakiwategemea sana wanasheria hivyo ni vyema kufanya kazi zenu kwa kuzingatia maadili ili kuweza kuisaidia jamii," alisema.

# Tembo kumi walivyoharibu makazi

**Na Happy Severine, BARIADI**

ZAIDI ya tembo kumi wamevamia makazi ya watu na kuharibu nyumba na mali mbalimbali katika Kijiji cha Halawa Kata ya Nkindwabiye Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi mkoani Simiyu.

Tembo hao wanadaiwa kuvamia kijiji hicho usiku wa kuamkia juzi saa saba usiku, ambapo waliezua nyumba 11 za familia saba zenye watu zaidi ya 50.

Mmoja wa wananchi walionusurika Mwalu Nsulwa, alisema tembo hao walivamia kwenye nyumba yake na kula mahindi yote gunia tano na viazi vilivyokuwa vimehifadhiwa ndani.

"Baada ya tembo kuvamia walianza kula mahindi na viazi vyote wakamaliza na wamehezua hadi nyumba na mpaka sasa sina sehemu ya kuishi, niliamua mimi na watoto wangu wawili kujificha uvunguni mwa kitanda ili kunusuru maisha yetu," alisema Nsulwa.

Mtendaji wa kijiji hicho, Mahenga Matongo, alisema tembo hao walivamia kaya saba na kuezua nyumba zote 11 na kula mahindi gunia 42, viazi gunia sita, huku akibainisha kuwa hakuna vifo vilivyotokea.

Matongo alieleza wananchi wote walioathirika na uvamizi wa wanyama hao, wamejihifadhi kwa majirani kutokana na kukosa sehemu za kuishi baada ya nyumba zao kuezuliwa. "Familia hizi hazina sehemu ya kulala tena maana nyumba zao zimeharibiwa vibaya, hawana hata chakula chochote kimeliwa na tembo na kilikuwa kimehifadhiwa ndani ya nyumba zao," alisema Matongo.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Festo Kiswaga, alifika eneo la tukio na kutoa pole kwa wananchi hao pamoja na kutoa msaada wa chakula, unga wa mahindi kilo 220, maharage kilo 50 na sukari kilo 20.

Kiswaga aliutaka uongozi wa Pori la Akiba la Maswa kuhakikisha wanabadili mfumo wa ulinzi wa tembo kutokana na kubadilika badilika mara kwa mara.

Alisema inashangaza kuona tembo wanakula mahindi, unga, maharage, viazi na mchele tofauti na ilivyozoelewa kuwa huwa wanakula nyasi na miwa.

"Niagize hapa viongozi wa Maswa Game lazima na nyie mbadilike katika kuwalinda hawa wanyama, askari wenu wakae karibu na hivi vijiji ambavyo vinapakana na hifadhi hii, maana inaonekana wameanza kuvamia sana."

Alisema serikali itafanya tathmini kwa waathirika wote ili kutoa fidia kama ulivyo utaratibu, na aliwataka wananchi kuendelea kutoa taarifa mapema ikiwa watawaona wanyama hao wamerudi kuvamia.

Meneja wa pori hilo, Lusato Masinde, alisema kwa sasa kuna tembo wengi wanatoka kwenye pori hilo na kuvamia makazi ya watu, hivyo aliwataka wananchi kuwa na tahadhari juu ya wanyama hao.

"Kwa kipindi cha wiki moja tumerudisha makundi makubwa ya tembo kuanzia Wilaya ya Meatu, Itilima na Bariadi ambao walikuwa wamevamia kwenye maeneo ya watu, tunaomba wananchi watoe taarifa mapema," alisema Masinde.



Mafundi wakiweka taa za barabarani zinazotumia nishati ya jua katika eneo la Sokota, Manispaa ya Temeke jijini Dar es Salaam wikiendi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Kasulu waomba taasisi za fedha kuongeza vituo

**Na Mwandishi Wetu**

BAADHI ya wananchi wilayani Kasulu mkoani Kigoma, wameziomba taasisi mbalimbali za kifedha kuongeza vituo vya kutolea huduma za kibenki katika maeneo ya vijijini, ili kupunguza changamoto ya wafanyabiashara kuvamiwa na kuporwa fedha zao pale wanaposafiri na fedha kwenda kununua bidhaa hasa nafaka.

Wakizungumza wakati wa mkutano wa biashara na wateja wa benki ya NMB wilayani Kasulu mkoani Kigoma, walisema kuwa kumekuwapo na matukio ya mara kwa mara ya wafanyabiashara kuvamiwa na kunyang'anywa fedha zao jambo walilodai kuwasababishia usumbufu na kushindwa kufanya biashara kutokana na kuwapo kwa vitendo hivyo.

Emmakulatha Mazina, mfanyabiashara wilayani humo, alisema uwapo wa taasisi za kifedha katika maeneo ya vijijini itasaidia pia kuongeza mzunguko wa fedha na kukuza biashara hasa kutokana na baadhi ya wakulima na wanunuzi wa mazao wakifanya biashara kwa hofu ya kuvamiwa, huku pia wakiomba serikali na wadau wengine wa maendeleo kutoa elimu kwa wananchi wa vijijini juu ya namna bora ya kuhifadhi fedha kwenye benki ili kuepuka hasara zisizokuwa za lazima zinazoweza kujitokeza.

"Wafanyabiashara kusafiri na pesa kwa sasa ni hatari sana katika maeneo yetu, unakuta mtu anaenda kijijini kununua mahindi au mihogo na hata mazao mengine akiwa na pesa mikononi, majambazi wakijua tu anatafuta bidhaa wanaanza kupanga njama za kumvamia," alisema.

Aidha, waliipongeza NMB kwa kutoa huduma za kibenki katika maeneo mengi ya mkoa wa Kigoma na kuomba benki hiyo kuendelea kuboresha huduma kwa wateja wake pamoja na kuona haja ya kutoza viwango vya riba za mikopo kwa kuzingatia hali ya kipato cha maeneo husika.

Pia waliiomba benki hiyo kuharakisha mchakato wa utoaji mikopo mikubwa kwa wateja kwa kuwaruhusu mameneja wa matawi kufanya tathmini na kumwidhinisha mteja kukopeshwa mkopo mkubwa tofauti na ilivyo sasa, ambapo mteja hulazimika kusubiri majibu kutoka ngazi ya kanda na makao makuu ya ofisi za benki hiyo, hali waliyosema imekuwa ikisababisha usumbufu mkubwa kwao.

Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Magharibi, Sospeter Magesse, alisema benki hiyo inaendelea kutatua changamoto zilizopo katika maeneo mbalimbali ili kuhakikisha malengo ya benki hiyo kuwahudumia wananchi yanafanikiwa kama ilivyokusudiwa.

Aidha, alisema benki hiyo imeanza utaratibu wa kushusha madaraka ya kutoa mkopo hadi bilioni moja kwa mameneja wa benki ngazi ya tawi ili baada ya kupokea maoni kutoka kwa wateja wake katika maeneo mbalimbali nchini.

000000

## TFS kuchochea viwanda nchini

**Na Mwandishi Wetu, ARUSHA**

WAKALA wa Huduma za Misitu nchini (TFS) imejipanga kuchagiza maendeleo ya sekta ya viwanda kupitia mazao yanayotokana na misitu sambamba na kusimamia utunzaji na uhifadhi endelevu wa misitu.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mkutano wa tano wa kisayansi juu ya mazingira endelevu, Mkurugenzi Mtendaji wa TFS, Prof. Dos Santos Silayo, alisema hatua ambazo zimechukuliwa katika uhifadhi wa mazingira zitatoa nafasi kubwa kwa sekta ya misitu kutumika kama malighafi viwandani.

"TFS tupo mstari wa mbele kwa kushirikiana na wadau wengine kama NEMC kuhakikisha kunakuwa na utunzaji bora wa misitu ili kuhakikisha inachangia katika ujenzi wa viwanda," alisema Prof. Silayo.

Alisema TFS kupitia wafanyakazi wake ambao wapo katika kanda zote nchini wamefanikiwa kudhibiti biashara haramu ya mazao ya misitu iliyokuwa inafanyika kipindi cha nyuma na kutoa fursa kwa mazao hayo kutumika katika kujenga viwanda.

"Tunaunga mkono jitihada za serikali kwa kusimamia na kulinda rasimali za nchi yetu na hivyo sisi kama TFS tunajukumu la kuhakikisha misitu iliyopo hapa nchini inawanufaisha Watanzania na pia inatumika kama sehemu ya malighafi ya viwanda," alisisitiza.

Alisema TFS inajumla ya hifadhi ya misitu ya asili 462 kati ya hiyo 23 ni misitu ya kupanda ambayo inasaidia kupunguza utegemezi malighafi katika misitu asilia hali inayosaidia kufanya misitu kuwa katika uhifadhi endelevu.

"Jumla ya viwanda 1,300 vinafanyakazi ya kuchakata malighafi za misitu ikiwamo kutengeneza karatasi, vibiriti, marine board pamoja na nguzo za umeme ambavyo vyote vinapata malighafi kutoka katika misitu ya kupanda," alisema.

Prof. Silayo alisema jukumu lingine la TFS ni kuhakikisha misitu inakuwa katika uoto wake wa asili ili kuondokana na uwezekano wa nchi kuingia kwenye jangwa hali ambayo inaweza kuepukika kwa kuendeleza juhudi za uhifadhi wa mazingira.

## HABARI KIMATAIFA

# Nyama choma yawapeleka mahakamani

**CANBERRA,** Australia

MWANAMKE mmoja nchini Australia, Cilla Carden, amejaribu kuwazuia majirani zake kuchoma nyama kwa kuwashtaki mahakamani.

Carden kutoka Jiji la Perth, Magharibi mwa Australia alidai kuwa shughuli zao za uchomaji nyama, uvutaji wa sigara na kelele za watoto unavunja sheria za makazi ya watu.

Aliamua kufuata njia hiyo ya kisheria ili shughuli hizo ziache kufanywa na majirani.

Hata hivyo, Mahakama ya Jimbo ilitupilia mbali madai yake kwa kusema kuwa hayana maana na ushahidi wa kutosha.

Madai yalihusisha pia familia zinazoishi jirani yake kupunguza mwanga wa taa zao, kuwanyamazisha wanyama wanofuga pamoja na kuweka miti kwenye bustani zao za kupumzika.

Alisema kuwa harufu ya moshi wa sigara na nyama choma zimemsababishia ashindwe kuishi vizuri.

"Siwezi kufurahia sehemu yangu ya kupumzika. Wameweka jiko la nyama choma ili nifikiwe na harufu ya samaki - harufu pekee ninayoipata ni ya samaki tu," alisema Carden ambaye hali nyama.

Uongozi wa jimbo hilo ulimjibu kuwa familia hizo zinajaribu kuishi kama familia. Hata hivyo familia waliokuwa wakilalamikiwa wamehamisha jiko lao la kuchomea nyama kama sehemu ya kumsaidia mlalamikaji.

Mahakama ilieleza kuwa familia hiyo, wamekuwa hawawashi taa usiku na kuwazuia watoto kucheza kutokana na hofu walioipata kwa kushtakiwa.

Carden alikata rufani ya uamuzi huo katika Mahakama Kuu ya Australia Magharibi, alikabidhi kurasa zaidi ya 400 zenye malalamiko ya kukata rufani.

Mwanasheria Mkuu wa Mahakama hiyo alisema kuwa kurasa zilikabidhiwa kwa mahakama zinashangaza.

"Hawaruhusu watoto wao kutoka nje usiku. Hawajawasha taa kwa siku kadhaa wakiogopa hatua atakazozichua mlalamikaji na jirani yao. Hili halikubaliki," alisema mwanasheria.

Mwezi Julai mahakama iliamua dhidi ya mlalamikaji wakisema malalamishi yake yamekuwa mzigo mzito kwa majirani.

Carden alisema kuwa atachukua hatua zaidi katika mahakama nyingine. **BBC**

# Madereva wa kigeni Afrika Kusini wawindwa

**JOHANNESBURG,** Afrika Kusini

POLISI Afrika Kusini wamewatia nguvuni watu kadhaa kufuatia vizuizi vya barabarani na vurugu zilizofanywa na waendesha malori wanaoandamana dhidi ya waajiriwa madereva wa kigeni nchini humo.

Msemaji wa Jeshi la Polisi katika Mkoa wa Kusini Mashariki mwa nchi hiyo KwaZulu-Natal (KZN), Jay Naicker alisema katika taarifa yake kuwa watu takriban 20 wamekamatwa kwa kushiriki katika matukio yanayohusishwa na maandamano katika sekta hiyo ya usafiri.

Siku ya Jumapili malori 11 yalifunga barabara inayoelekea Bandari ya Richard Bay, moja ya bandari kongwe barani Afrika.

Serikali ya Afrika Kusini imesema katika mji wa Cape Town baadhi ya waandamanaji walifunga barabara kwa magari yao.

"Barabara kadhaa ilibidi zifungwe kutokana na foleni kubwa ya magari kuanzia asubuhi kufuatia malori kufunga barabara na malori mengine yakionekana kumwaga michanga barabarani," ilisema taarifa kutoka ofisi ya waziri wa usafiri, Bonginkosi Madikizela.

**Madereva wa Afrika Kusini wana njaa na wanakaa tu nyumbani na wale wanaopata ajira ni madereva wa kigeni ambao hulipwa mshahara mdogo.**

Wiki iliyopita Shirika la kutetea Haki za Binadamu la Human Rights Watch liliripoti kuwa madereva kadhaa wa malori nchini Afrika Kusini waliuawa kutokana na mashambulizi dhidi ya madereva wa kigeni tangu Machi mwaka 2018. Ripoti hiyo ilitolewa baada ya mashambulizi ya hivi karibuni ya chuki dhidi ya wageni yaliyochochewa na kushuka kwa uchumi na kukosekana kwa ajira.

Shirika la waendesha malori nchini Afrika Kusini lililonukuliwa na Shirika la Human Rights Watch limeripoti matukio 75 tangu Machi mwaka huu, ambapo matukio 15 kati ya hayo yalithibitishwa na HRW.

Hata hivyo, mwenyekiti wa chama cha madereva alisema kwamba hawakuhusika kwa namna yoyote na maandamano yaliyofanyika Jumatatu, lakini kile wanachokipigania ni Waafrika Kusini kuajiriwa zaidi.

Alisema madereva wa Afrika Kusini wana njaa na wanakaa tu nyumbani na wale wanaopata ajira ni madereva wa kigeni ambao hulipwa mshahara mdogo.

Msemaji wa Wizara ya Kazi nchini humo, Makhosonke Buthelezi wiki iliyopita alisema waajiri wanapenda kuwa na mdereva wa kigeni maana wanafanya kazi saa nyingi kwa kiwango kidogo cha mshahara kwa hiyo ni kama wanawadhulumu.

Juni mwaka huu Waziri wa Usafiri, Fikile Mbalula alisema tatizo lililopo nchini kwa sasa limesababishwa na kuajiriwa kwa madereva wengi wakigeni ambao wengine hawajasajiliwa au kuwa na vibali halali vya kufanyia kazi. **DW**



Wanafunzi wa vyuo vikuu na shule za sekondari mjini Hong Kong, wakiwa wamegoma kuingia madarasani wakijiandaa kwa maandamano. **PICHA: REUTERS**

# Vuta ni kuvute wabunge, waziri mkuu Uingereza

**LONDON,** Uingereza

MJADALA mkali unatarajia kutokea kwenye Bunge la Uingereza kati ya Waziri Mkuu, Boris Johnson anayeshikilia mpango wa kujiondoa kutoka Umoja wa Ulaya (EU) bila ya mkataba, chama kikuu cha upinzani kinachozuia mpango huo.

Vyama vya upinzani vimesimama kidete kuupinga mpango wa Boris wa kutaka kuiondoa Uingereza kutoka EU bila ya mkataba, ifikapo Oktoba 31.

Vyama vya upinzani jana viliwasilisha bungeni ajenda ya kuuzuia mpango wa Boris ambaye amewataka wabunge wa chama chake cha Conservative wasiunge mkono ajenda ya wapinzani ya kuizuia Uingereza kuondoka EU bila ya mkataba. Katika tamko alilolitoa, Boris aliwataka wabunge wa chama chake waunge mkono mpango wa serikali yake.

Waziri Kuu Boris alitoa kauli hiyo huku akizomewa na wapinzani wa Brexit pia alisema kuwa hataki uchaguzi mkuu wa mapema.

Lakini pia alieleza wazi kwamba ikiwa serikali yake itashindwa itawasilisha muswada leo, juu ya kuidhinisha uchaguzi. Lakini alisisitiza kwamba hataki uchaguzi na kwamba ni lazima kusonga mbele na ajenda ya umma.

Kiongozi wa chama cha upinzani, Jeremy Corbyn, aliwataka wabunge wake wapige kura kuunga mkono kufanyika uchaguzi Oktoba 14 na kuambatanisha na hatua ya kuomba EU kutoa muda zaidi kwa Uingereza.

Corbyn alifanya juhudi kwa kushirikiana na baadhi ya wabunge waasi wa chama cha Conservative ili Uingereza iweze kuchelewesha kuondoka EU, kwa muda wa miezi mitatu.

Kiongozi huyo wa chama cha upinzani alisema ikiwa serikali itashindwa ataitisha uchaguzi.

Waziri Mkuu Boris anataka kulitumia suala la Uingereza kujiondoa bila ya mkataba kama njia ya kuushinikiza EU ukubaliane na matakwa yake.

Hata hivyo EU ilisema hakuna uwezekeno wa kuanzisha mazungumzo mapya juu ya mkataba ambao tayari umeshafikiwa. Mkataba huo ulifikiwa na Waziri Mkuu wa zamani, Theresa May lakini Boris alisema mkataba huo haukubaliki. **DW**

# Shule Lindi kukaguliwa changamoto za ufaulu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI inakusudia kufanya ukaguzi maalum katika shule za Mkoa wa Lindi ili kubaini changamoto zinazosababisha kuwa na kiwango kidogo cha ufaulu.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, alisema bungeni jana alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa kuteuliwa, Salma Kikwete.

Mbunge Salma, akiuliza swali bungeni alisema hali ya ufaulu mkoani humo ni mbaya inayosababisha kuwa wa mwisho.

Alihoji serikali ina mkakati gani kuhakikisha inadhibiti au kupunguza changamoto hiyo ili wanafunzi wafanye vizuri kwenye masomo yao.

Akijibu swali hilo, Prof. Ndalichako alisema wizara ambayo kazi yake ni kusimamia na kudhibiti masuala ya elimu, itahakikisha inafanya ukaguzi maalum katika mkoa huo ili kuinua ufaulu.

"Tutafanya ukaguzi maalum katika shule za mkoa wa Lindi ili tuweze kubaini changamoto na tuweze kuchukua hatua mahusisi kuhakikisha kwamba unainuka katika ufaulu kwa wanafunzi ambao wanasoma katika shule za sekondari na msingi," alisema.

Awali, akijibu swali hilo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, alisema ni kweli mkoa huo umekuwa haufanyi vizuri na kipindi cha katikati ofisi hiyo ilipoona changamoto hiyo alimwagiza Naibu Waziri wake Mwita Waitara, kwenda mkoani humo kutembelea shule mbalimbali pamoja na mambo mengine.

"Lengo ni kuboresha shule hizi ili mazingira yawe rafiki zaidi na kwamba ndio maana maombi ambayo Mama Salma aliyaomba yalienda kuangaliwa, na mimi mwenyewe nitafanya ziara maalum mkoani Lindi kwa ajili ya kuhakikisha jinsi gani tunafanya mkoa huu sasa uinuke kielimu na ndio maana hata katika mgao wa walimu wapya kipaumbele chetu ni kwamba jinsi gani hata kule tupeleke wa kutosha," alisema.

Alieleza kuwa hata uhamisho wa walimu mkoani Lindi kwa sasa umesitishwa kwa lengo kubwa ambalo mkoa huo unatakiwa uwe katika hali nzuri.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Halima Bulembo, alitaka kujua sababu ya mikopo ya wanafunzi wa chuo kikuu kutolewa kwa ubaguzi.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Wizara ya Elimu, William Ole Nasha, alisema hakuna ubaguzi wowote katika utoaji mikopo na imekuwa ikitolewa kwa Watanzania wote wenye uhitaji na waliiomba mikopo hiyo kwa kuzingatia sheria, taratibu na vigezo vilivyowekwa.

Alisema ni vyema waombaji wakazingatia maelekezo yanayotolewa na bodi wakati wa uombaji wa mikopo ikiwa ni pamoja na kujaza taarifa zao kwa usahihi na kuambatanisha nyaraka zote muhimu.



Mkuu wa Bidhaa na Huduma kutoka Tigo, David Umoh, akikabidhi 'Home Internet Router' kwa Mtangazaji wa Clouds Fm, Abdallah Kamelo, katika uzinduzi wa huduma ya kwanza na ya kipekee ya Home Internet kutoka Tigo, jijini Dar es Salaam jana. Katikati ni Ofisa Mkuu wa Biashara wa kampuni hiyo, Tarik Boudiaf. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Mnufaika asimulia alivyokombolewa na Tasaf

**Na Elizabeth Zaya,** SINGIDA

MNUFAIKA wa mpango wa kunusuru kaya maskini unaosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) katika Kijiji cha Mtipa Halmashauri ya Singida, Maria Majengo, amesimulia namna alivyosaidiwa na mfuko huo baada ya kufukuzwa yeye pamoja na watoto wake saba kwa sababu za ndugu wa mume wake kugombania mali

Akisimulia hayo mbele ya waandishi wa habari waliomtembelea kijijini hapo, Maria alisema baada ya mume wake kufariki mwaka 2002, alifukuzwa na ndugu hao pamoja na watoto wake saba ili wagawane mali.

"Mwaka 2002 mume wangu alifariki na kuniachia watoto saba, tulikuwa na mali ambazo zingenisaidia kuwalea watoto wangu, lakini cha kushangaza ndugu waliingiwa na tamaa na mali hizo wakaanza kugombania, mgogoro ulifikia hatua mbaya mpaka wakanifukuza na watoto wangu," alisimulia Maria.

Aliongeza: "Baada ya kufukuzwa, nilirudi nyumbani kwa wazazi wangu pamoja na watoto wangu, lakini maisha yalianza kuwa magumu kwa sababu nao walikuwa hawana uwezo wa kutuhudumia, walikuwa wamezeeka."

"Ilibidi nianze kuhangaika kutafuta vibarua nafanya ndio tunapata chakula, na wakati mwingine nisipopata tulikuwa tunalala na njaa na nilikuwa nalazimika kuomba kwa majirani ili angalau watoto wapate hata kama kidogo cha kuchangamsha tumboni."

"Watoto wangu ambao walikuwa wameanza shule waliacha kwenda kwa sababu nilishindwa kuwanunulia mahitaji yoyote ikiwamo nguo, nilihangaika na nilikuwa naumia sana nikimkumbuka mume wangu, wanakijiji nao ilifika kipindi wakawa wananionea huruma na kunisaidia chochote wanachopata," alisema.

Alisema mwaka 2007 wanakijiji walimpendekeza aingizwe katika mpango wa Tasaf wa kunusuru kaya maskini.

"Niliingizwa Tasaf mwaka 2007, baada ya kupendekezwa katika mkutano wa kijiji, wote tuliokuwa tumependekezwa tuliandikishwa na tukaja kuangaliwa tunakoishi, na baada ya miezi miwili nilipewa Sh. 40,000, sikuamini kushika hiyo hela katika mikono yangu," aliongeza.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA
(S.M.M. 1984 NYONGEZA)
YA 5 KANUNI YA 2

Katika Mahakama ya Mwanzo: TEMEKE

Usimamizi wa Mirathi No. 320/2016

Ombi la **FARSY ADINANI MSUYA** kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya Marehemu **ADINANI MANGACHI MSUYA/KATERA MSHANGA MANGACHI**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 16/09/2019.

kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 16/09/2019.

115402702

KUPOTEA KWA KADI YA GARI

VEDASTO EDGAR NGOMBALE ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI T 997 BAS AINA YA FUSO. CHASSIS NO. FK417J740596. ENGINE NO. 1257556.

YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI.

TAARIFA YA POLISI: KLM\RB\2138\2019.

115401702

## Waelezwa utaratibu wa kuwalalamikia mahakimu

**Na Amri Lugungulo,** KISARAWE

KATIBU Tawala Wilaya ya Kisarawe, Mkoa wa Pwani, Mtella Mwampamba, amewahimiza wananchi wenye malalamiko dhidi ya mahakimu wa mahakama za mwanzo wilayani humo, ikiwamo kukosa haki zao mahakamani watoe taarifa kwa mkuu wa wilaya ili wazipate.

Mwampamba alitoa wito huo mwishoni mwa wiki wakati wa mkutano wa kawaida wa Baraza la Madiwani wa halmashauri ya wilaya hiyo mjini Kisarawe.

"Mwananchi yeyote anapoona hatendewi haki na hakimu wa mahakama ya mwanzo. afike ofisi ya mkuu wa wilaya ambako kuna tume ya kuyajadili malalamiko ya wananchi dhidi ya mahakimu hao wa mahakama za mwanzo ili kupata suluhu," alisema.

Alisema kuwa ofisi ya DC ina uwezo wa kujadili malalamiko ya mwananchi yeyote dhidi ya hakimu wa mahakama za mwanzo tu ili kupata suluhu.

"Malalamiko dhidi ya mahakimu wa mahakama za juu yanajadiliwa na mamlaka za juu ikiwamo ofisi ya mkuu wa mkoa," alisema.

Aliongeza kuwa ofisi hiyo imekuwa ikiona kuwa hakimu anayelalamikiwa kuwa anafanyakazi kinyume cha sheria atajadiliwa kupata suluhu.

Alisema ofisi hiyo imekuwa ikishindwa kujadili malalamikio kutokana na wananchi kushindwa kupeleka malalamiko yao kwa DC.

"Natoa wito kwa wananchi watoe taarifa za malalamiko kwa DC ili waweze kupata haki zao," alisema.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA KAZI

Anahitajika - Mhasibu na sales Lady
Sifa – Awe Mwanamke
Elimu – Diploma


Ofisi yetu ipo Posta – Dar es Salaam
Kwa Mawasiliano :- 0715 – 885 533


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA Tutumie
E-mail: advertise@guardian.co.tz,
au piga simu: 0767 223311


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAMBO YA NDANI**
**IDARA YA UHAMIAJI**


### MAOMBI YA URAIA



**MR. DHAVAL JAGDISHCHANDRA RANA** mwenye picha hapo juu anaomba uraia wa Tanzania kwa Mh. Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Utaifa wake wa sasa ni Mhindi. Nchi atokayo ni India. Kwa sasa anaishi Kahama Shinyanga. Kwa yeyote mwenye taarifa/sababu za kwanini mwombaji asipewe Uraia wa Tanzania, atume taarifa ya maandishi kwa Kamishna Jenerali wa Uhamiaji S.L.P 512, Dar es salaam.

115402502

### KUPOTELEWA NA RESULT SLIP



**SENGELEMA JOHN SENGELEMA** anatangaza kupotelewa na Result Slip ya kidato cha cha nne yenye index namba **S.5168/0079** iliyotolewa na MOUNT MORIE SEKONDARI mwaka 2018. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Control No. **991089413913..**

115402102

### VYETI VIMEPOTEA



**MOH'D AHMED HIMID** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1298-0157** kilichotolewa na KIEMBESAMAKI SEKONDARI mwaka 2007. Cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P.1085-0052** kilichotolewa na LAUREATE INSTITUTE CENTRE mwaka 2008. Cheti cha Shahada ya kwanza ya Ualimu chenye namba **BAED 013484** kilichotolewa na Chuo Kikuu cha Dar es salaam mwaka 2013. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MAZ/L.F 117/2019.**

115402302

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**JOVENARY JOSEPH NDUKA,** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA, yenye Namba T224DFW, chasis No: NCP58003003I, Model Na UA-NCP58G, Engine Na. 1NZB137653. Kadi iliungua kwa moto, na aliripoti kituo cha polisi cha Muleba tarehe 20/08/2019 na kupewa.

No: KAG/MUL/RB/264260/2019.

Kwa yeyote atakayeiona haipeleke kituo cha polisi kilichoko karibu naye, au awasiliane naye kwa namba 0754-887810.

115401501

### KADI YA GARI IMEPOTEA

V.I.P SAFARI CLUB LTD. ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI T 415 ACS. CHASSIS NO 4325696. ENGINE NO 4090571.

YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI.

TAARIFA YA POLISI: ARU/ARU/RB/266553/2019.

115401602

### KADI YA GARI IMEPOTEA

**ELISHAFRA SHARTIEL KILAVO** Anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T 966 DKE**. Aina Yake **TOYOTA HARRIER 240.** Yenye chassis namba **ACU30-0027081** na Engine namba **2AZ-FE2362.** Yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa kituo cha polisi, Taarifa ya Polisi: **MOR/MOR/RB/261092/2019.**

115403301

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo**
**CHAMWINO MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi**

**Ombi la RAMADHANI KONDO Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu MWAJABU SAIDI MGOMBELWA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 18/09/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 03/09/2019.

115403202

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;165/2019**

**Ombi la ROSE ATHUMANI RAMADHANI Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu THOMAS BERIAS MASINDE**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 17/09/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 03/09/2019

115403002

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
03/09/2019

### TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Alhamisi tarehe **05/09/2019** kampuni ya **Builders & Limeworks Co. Ltd** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **SAME kuelekea ARUSHA,** gari hilo lenye namba za usajili **T170BAP/ T515 ALG**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| **Urefu** | ……………….. | **17.0m** |
| **Upana** | ………………… | **3.5m** |
| **Kimo** | ………………… | **4.55m** |

3. Njia itakayotumika: **SAME hadi ARUSHA Kupitia KIA,** gari litasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

115403102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA**
**KAGERA LILILOPO BUKOBA**
**RUFAA NA: 18/2019**
**LONGINO EDWARD ……………MKATAFURAA**
**DHIDI YA**
**CHRISTINA JOSEPH ……………MJIBURUFAA**

**KWA: CHRISTINA JOSEPH**
**(POPOTE PALE MLIPO)**

Mnaarifiwa/ unaarifiwa kuwa ***Rufaa Na. 18/2019*** yamepangwa kutajwa tarehe **16.09.2019** mbele ya mwenyekiti wa baraza , ***R. Mtei*** saa 2:00 asubuhi.
Hivyo, unaamuriwa kuhudhuria wewe mwenyewe/ mwakilishi wako mbele ya baraza siku hiyo bila kukosa. Usipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yako na hukumu kutolewa.
AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na **MUHURI** wa baraza hili leo tarehe **07.08.2019**

115402602

### KUPOTEA KWA KADI

**Blandina Francis Billy** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili wa namba T773 CNC aina ya TOYOTA IST,yenye chasis namba NCP600066094.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa: DAR/IST/RB/244339/2019

215400802

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.70 OF 2019**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE JUDITH MGAZA KUMWENDA**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF PROBATE AND**
**ADMINISTRATION OF ESTATE BY PETER SENKONDO ANDREW.**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate(or letters of administration) is made to the above named Petitioner. Objections to the grant should be filled on or before 23rd Day of September 2019.

The will of the said deceased is deposited and open for inspection at the court.

Dated at 2 this day of September 2019.

215401202

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**TAWAQAL AND COMPANY** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TRACTOR VOLVO YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 482 BBJ.** CHASSIS NAMBA **YU2J4CFC93A569624** ENGINE NAMBA **0000182176.**YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI **MB/TR/RB/649/2018.**

115402202

### KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**TANZANIA CHINA TRADE AND TOITIN** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili T 679 CUX FEKON – FK 125 – B. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **MBE/MBE/RB/224472/2019.**

115401002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

Katika Mahakama ya Mwanzo DODOMA MJINI
Usimamizi wa mirathi 56/2019
Ombi la HASSAN SAID kuteuliwa

Msimamizi wa mirathi Marehemu SAID SALEHE MSUNGWA

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnano tarehe 23/9/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa

Tarehe 29/8/2019

115401102


**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# ERIKSEN HAJUTII KUTANGAZA KUONDOKA TOTTENHAM



**LONDON,** England

CHRISTIAN Eriksen hajutii kuhusu kutangaza kwake hadharani mpango wa kutaka kuondoka Tottenham, lakini ameelezea kukatishwa tamaa baada ya mchakato huo wa kuhama kushindikana.

Eriksen alibainisha Juni mwaka huu kwamba anataka kupata changamoto mpya kwa kucheza kwenye klabu mpya baada ya kucheza miaka sita akiwa Spurs.

Licha ya klabu kadhaa kubwa kuonyesha nia ya kutaka kumsajili kama vile Real Madrid, Juventus na Paris Saint-Germain, lakini zilishindwa kukamilisha uhamisho wake kwa wakati.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 raia wa Denmark amesema: “Hapana, haikuwa kosa, lakini huu ni mchezo wa soka na huwezi kujua nini kitatokea na kuna vitu vinakuja kwenye njia iliyo sawa.

“Ningependa kufanya maamuzi kwenye soka, lakini bahati mbaya mambo hayakuweza kutokea na sikuwa na uwezo wa kulazimisha jambo litokee.”

Mkataba wa sasa wa Eriksen unamalizika kipindi kijacho cha majira ya joto na atakuwa mchezaji huru kuanza mazungumzo ya kusaini mkataba mpya na klabu nyingine, Januari mwakani.

# Emery atupiwa lawama Arsenal

**LONDON,** England

NYOTA wa zamani wa Arsenal, Paul Merson, amemtupia lawama kocha wa Arsenal, Unai Emery kwa kushindwa kuleta jipya lolote tangu alipoichukua klabu hiyo mwaka 2017.

Emery aliiongoza Arsenal kumaliza nafasi ya tano kwenye msimamo na kucheza fainali ya kombe la Europa msimu uliopita, na sasa ipo kwenye nafasi ile ile baada ya mechi nne za Ligi Kuu ya England, huku ikitoka sare ya kufungana mabao 2-2 na Tottenham kwenye mchezo wake wa mwisho.

Merson, ambaye alitumikia miaka 12 katika kikosi cha kwanza cha Arsenal, bado hashawishiki kama klabu hiyo inapiga hatua yoyote chini ya kocha huyo raia wa Hispania.

Merson aliiambia Sky Sports: “Mchezo wa ‘dabi’ ya London ulikuwa mzuri na Arsenal waliweza kupata sare baada ya kuwa nyuma kwa mabao mawili. Lakini kuna chochote kimebadilika Arsenal? Sidhani.

“Arsenal ilicheza vile vile kama ambavyo ilifungwa na Liverpool wiki iliyopita, hakuna kilichobadilika. Ni kama vile Unai Wenger anaendesha timu kwa sasa.

“Kila wakati Tottenham waliipita kirahisi beki ya Arsenal na ilionekana kama wanakwenda kufunga. Arsenal walijiachia na walikuwa wazi. Safu ya kiungo ilipwaya kabisa.

“Unakuwa na mtu kama Granit Xhaka ambaye anaenda kuwafanyia faulo wachezaji na mara zote anapewa adhabu.

“Ndio, Matteo Guendouzi alitengeneza pasi nzuri kwa bao la kusawazisha, lakini huwezi kumuachia yeye peke yake achezea mpira na kutafuta mabao.”



# Skrtel ajiunga Instanbul




**INSTANBUL,** Uturuki

BEKI Martin Skrtel amejiunga na klabu ya Instanbul Basaksehir baada ya ‘kwabwatukizana’ na benchi la ufundi la Atalanta ya Italia ambayo alivunja nao mkataba siku 24 baada ya kuusaini.

Mlinzi huyo wa zamani wa Liverpool alijiunga na miamba hao wa Serie A Agosti mwaka huu na kumaliza miaka mitatu ya kucheza pale Fenerbahce, lakini akaondoka bila kucheza mchezo wowote.

Skrtel mwenye umri wa miaka 34, akaamua kurudi tena Uturuki, huku kuondoka kwake kukitokana na kulamu kushindwa kuzoea mbinu mpya za uchezaji.

“Alisema kwamba katika umri wake, alikuwa na wakati mgumu wa kucheza mfumo wa walinzi watatu ambao haueleweki,” amenukuliwa kocha Gian Piero Gasperini akisema.

“Aliwasili baada ya kuanza mazoezi, na alikuwa na wakati mgumu.

“Ilikuwa ngumu kwake kuzoea mfumo na staili yetu ya uchezaji, ambayo inaeleweka.”

Skrtel awali alitumia misimu tisa kucheza pale Liverpool, akicheza mechi 320 katika mashindano yote.

HABARI MICHEZO

# Mkhitaryan ajiunga Roma kwa mkopo

**ROME,** Italia

KIUNGO wa Arsenal, Henrikh Mkhitaryan, amejiunga na AS Roma kwa mkataba wa mkopo wa muda mrefu, klabu hiyo imetangaza.

Dili hilo pia lina kipengele cha kumnunua kwa ada ya pauni milioni 3 mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 raia wa Armenia.

"Ni nafasi nzuri kwangu kuanza ukurasa mpya na klabu kubwa," amesema Mkhitaryan.

"Naijua klabu hii kwa namna ilivyo, na nina uhakika tunaweza kupata mafanikio makubwa kwa pamoja."


Akiwa amesajiliwa kutoka Manchester United kwa uhamisho uliomhusisha Alexis Sanchez Januari 2018, Mkhitaryan alishindwa kuwa na wakati mzuri pale kwenye dimba la Emirates chini ya kocha Arsene Wenger pamoja na mrithi wake, Unai Emery.

"Henrikh atafiti kwenye malengo na mbinu zetu na kuongezwa kwenye kikosi cha wachezaji wetu," amesema Mkurugenzi wa soka wa Roma, Gianluca Petrachi.

Mkhitaryan pia alitokea benchi kwenye mchezo wa jumapili wa sare ya kufungana mabao 2-2 na Tottenham kwenye uwanja wa Emirates, na unaonekana kama ndio ulikuwa mchezo wake wa mwisho kucheza akiwa na jezi ya Arsenal.

Emery alimuambia wazi mchezaji huyo wa zamani wa Borussia Dortmund kwamba hakuwa kwenye mipango yake msimu huu na Mkhitaryan amemfuata mchezaji mwenzake pale Old Trafford, Chris Smalling ambaye ametua kwa mkopo hapo Roma.



# GREENWOOD KUMWAGA WINO MKATABA MPYA UTD

**MANCHESTE,** England

'DOGO' Mason Greenwood anaelekea kusaini mkataba mpya katika klabu ya Manchester United baada ya kocha, Ole Gunnar Solskjaer kuonekana kuvutiwa na kinda huyo, kwa mujibu wa Daily Mail.

United walimpa mkataba Greenwood Oktoba mwaka jana, lakini sasa wanaonekana wanataka kumuongeza tena mwingine baada ya kuimarika kiwango chake cha uchezaji.

Taarifa zaidi inasema kwamba, sasa mchezaji huyo atalipwa mshahara wa pauni 25,000 kwa wiki pamoja na bonsai, ikitegemea na kukua zaidi kwa kiwango chake.

Greenwood amepewa nafasi kwenye benchi katika mechi zote nne za ligi Kuu msimu huu.

Amecheza jumla ya dakika 47 baada ya kufunga mara mbili kwenye mechi za mandalizi ya msimu huu.

Pia kuna matarajio kwamba Greenwood anaweza kuanza kwenye mechi za kombe la Carabao pamoja na ligi ya Europa.

Solskjaer ameonekana kuvutiwa na kiwango cha mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 17 na alimpa nafasi ya kuanza kwenye mchezo dhidi ya Cardiff msimu uliopita.

Julai, aliweka wazi kwamba anamchukulia mshambuliaji huyo kama mmoja wa wachezaji ambao watakuja kutamba zaidi siku za usoni na hivi karibuni aliitwa katika kikosi cha timu ya taifa ya England chini ya umri wa miaka 21.

# *Sanchez: Sijutii kuhama United*

**MILAN,** Italia

ALEXIS Sanchez amesema kuwa hajutii uamuzi wake wa kujiunga na Manchester United mwaka jana.

Mchezaji huyo raia wa kimataifa wa Chile alisajiliwa Inter Milan kwa mkopo wa muda mrefu baada ya miezi 18 pale Old Trafford ambako alifunga mabao matano katika mechi 45 alizocheza.

Mshambuliaji huyo amejiunga na Romelu Lukaku hapo Inter baada ya mchezaji wa kimataifa wa Ubelgiji kujiunga na Nerazzurri hao kipindi cha majira ya joto.

"Nina furaha kubwa nilienda Manchester United," alisema akiiambia BBC Sport. "Ni klabu ambayo imeshinda zaidi nchini England.

"Wakati nilikuwa Arsenal ilinivutia zaidi, nilikuwa na furaha pale lakini United ilikuwa inakua kwa wakati ule, walikuwa wananunua wachezaji wa kushinda kitu fulani.

"Nilitaka kujiunga nao na kushinda kila kitu. Sijutii kwenda pale."

Kocha wa United, Ole Gunnar Solskjaer amesema Sanchez anaweza kuwa na nafasi kwenye klabu hiyo baada ya kipindi cha mkopo kule Serie A, lakini mshambuliaji huyo amebainisha kwamba anahitaji muda zaidi wa kucheza uwanjani ili ajisikie furaha. "Nafikiri ninakuwa na furaha wakati nikiwa naichezea timu ya taifa," aliongeza. "Nilikuwa na furaha pia kuwa pale Manchester United, lakini mara zote nimewaambia marafiki kwamba nataka kucheza.

"Kama wangenipa nafasi ya kucheza nilifanya vizuri zaidi. Wakati mwingine ningepanda kucheza dakika 60, lakini sikupata nafasi hiyo na sikujua kwanini."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ICARDI: KUTUA PSG NI HATUA KUBWA

Ninamjua Cavani, nilikutana na Neymar Jr, ninajisikia fahari kuwa mchezaji mwenzao...

**PARIS,** Ujerumani

MAURO Icardi amesema kutua kwake kwa miamba ya Ligue 1, Paris Saint-Germain ni "hatua kubwa katika kazi yake" baada ya kuhitimisha ndoto zake pale Inter Milan.

**Icardi ameachana na miamba ya Serie A, Inter na kujiunga na PSG kwa mkataba wa mkopo wa muda mrefu kabla ya dirisha la usajili la majira ya joto kufungwa juzi, Jumatatu saa sita usiku.**

Kunyang'anywa kitambaa cha unahodha Inter msimu uliopita na kutokukubalika na kocha Antonio Conte msimu huu, Icardi alitia saini mkataba wa mwaka mmoja zaidi katika klabu hiyo ya 'Nerazzurri' kabla ya kwenda kujiunga na PSG dakika za mwisho.

Akiangazia kutua kwake PSG, ambayo imeripotiwa kuwa na nafasi ya kumnunu mshambuliaji huyo kwa euro milioni 70, Icardi aliiambia PSG TV: "Ni mwenye furaha sana, kufurahi.

"Ni hatua kubwa katika kazi yangu, na nafasi nzuri kujiunga na klabu kubwa kama Paris Saint-Germain. Ninatumai kuacha mambo mazuri hapa.

"Kuwa tayari kucheza sambamba na wachezaji wenye vipaji hapa inashangaza. Uamuzi ulikuwa rahisi kufanya, nimekuja Paris kwa sababu nilitaka kuichezea.

"Ninajua Waargentina wazi, na ninamjua [Edinson] Cavani. Na nilikutana na Neymar Jr. Ninajisikia fahari kuwa mchezaji mwenzao.

"Mimi ni straika, ninapenda kufunga mabao. Itakuwa vizuri kucheza mbele na washambuliaji wa kushangaza katika kikosi hiki.

"Mara zote ni jambo la kipekee kucheza dhidi ya wapinzani. Hili ndilo linalolifanya soka kuwa zuri. Nilicheza dhidi ya Juve, Milan, hizi ni mechi kubwa. Sasa ninatazama mbele kucheza mechi hizi hapa Ufaransa.

"Sijhawahi kucheza hapa Parc des Princes, itakuwa mara ya kwanza kwangu. Kisha nitakuwa tayari kueleza nini ninachokipenda!"

Icardi, ambaye alitua Inter akitokea Sampdoria mwaka 2013, amefunga mabao 111 kwenye Serie A na mabao 124 kwenye mashindano yote ambayo yanamfanya kuwa mfungaji bora wa nane wa wakati wote.

## ZISIKUPITE

### NEVILLE AWINDWA MAREKANI

KOCHA wa timu ya Taifa ya England, Phil Neville ndiye anayeongoza katika orodha ya makocha wanaopewa nafasi ya kurithi mikoba ya kocha aliyeibebesha Marekani Kombe la Dunia kwa wanawake, Jill Ellis. ***(Mail)***

### ILITAKA REKODI KWA NEYMAR

RAIS wa PSG, Nasser Al-Khelaifi, angeweza kumwacha Neymar tu aondoke kama ofa ya rekodi ya dunia ya pauni milioni 272 ingewekwa mezani. ***(Le Parisien, via Sport)***

### SANCHO AIFUNGULIA UNITED

MSHAMBULIAJI wa Borussia Dortmund, Muingereza Jadon Sancho, 19, ameacha milango wazi ya kujiunga na Manchester United kwa kusema "hakujali" kurudi nchini mwake. ***(Mirror)***

### LUIS, DIAS WATAZAMWA UNITED

MANCHESTER United imetuma mashushu kutazama mechi kati ya Benfica na Braga Jumapili ili kumtazama beki Mreno Ruben Dias, 22, na kiungo Florentino Luis, 20. ***(Mirror)***

### KALINIC KWA MKOPO ROMA

MSHAMBULIAJI wa Atletico Madrid, Nikola Kalinic, amejiunga na AS Roma kwa mkopo wa muda mrefu, na miamba hiyo ya Serie A ikimtoa mshambuliaji wa kimataifa wa Czech, Patrik Schick, 23, kwa mkopo RB Leipzig. ***(Gazzetta dello Sport - in Italian)***

### REBIC, SILVA WAPISHANA RASMI

STRAIKA Mcroatia Ante Rebic, 25, ameondoka Eintracht Frankfurt na kujiunga kwa mkopo wa miaka miwili AC Milan, huku Mreno Andre Silva, 23, akielekea upande wa pili. ***(Gazzetta dello Sport - in Italian)***

### ATAKIWA KUMNUNUA MBAPPE

MTANDAO wa shabiki wa Liverpool umeishauri klabu hiyo kumuuza Mohamed Salah, kupata fedha za kumnunua mshambuliaji Kylian Mbappe, 20, kutoka Paris St-Germain, straika wa Borussia Dortmund, Jadon Sancho, 19, ama Kai Havertz, 20, wa Bayer Leverkusen. ***(Mirror)***

### ALCANTARA MKOPO CELTA VIGO

KIUNGO Mbrazil Rafinha Alcantara, 26, ameongeza mkataba na Barcelona kabla ya kujiunga na mahasimu wao Celta Vigo kwa mkopo wa muda mrefu. ***(Marca)***

### KJAER MBADALA WA SKRTEL

ATALANTA imeziba pengo la Martin Skrtel, 34, ambaye alivunja mkataba na klabu hiyo siku 24 tu baada ya kutia saini, kwa kumsajili beki wa kati Mdenmark Simon Kjaer, 30, kutoka Sevilla. ***(Goal)***

### WINGA SPURS ATUA VITORIA

WINGA wa Tottenham, Muingereza Marcus Edwards, 20, anayedaiwa kuwa "Messi mdogo" - ameondoka hapo kaskazini mwa London na kwenda kujiunga jumla na klabu ya Vitoria ya Ureno. ***(Sun)***

### NEYMAR AWEKWA KIPORO

BARCELONA imeshindwa kuipata saini ya mshambuliaji wake wa zamani, Mbrazil Neymar, 27, kutoka Paris St-Germain, lakini haijakata tamaa kwani itarudia tena mpango huo majira ya joto yajayo. ***(ESPN)***

## HABARI MICHEZO

### MSIMAMO LIGI KUU BARA




| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Lipuli | 1 | 1 | 0 | 0 | 3 | 1 | 3 |
| 2. Simba | 1 | 1 | 0 | 0 | 3 | 1 | 3 |
| 3. Kagera Sugar | 1 | 1 | 0 | 0 | 2 | 0 | 3 |
| 4. Namungo | 1 | 1 | 0 | 0 | 2 | 1 | 3 |
| 5. Azam | 1 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 3 |
| 6. Ruvu Shooting | 1 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 3 |
| 7. Polisi Tanzania | 1 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 3 |
| 8. Mwadui | 1 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 3 |
| 9. Mbao | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 | 1 | 1 |
| 10. Alliance | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 | 1 | 1 |
| 11. Mbeya City | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| 12. TZ Prisons | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| 13. Ndanda | 1 | 0 | 0 | 1 | 1 | 2 | 0 |
| 14. Yanga | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 |
| 15. Coastal Union | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 |
| 16. Singida United | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 |
| 17.Kinondoni MC | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 |
| 18.Mtibwa Sugar | 1 | 0 | 0 | 1 | 1 | 3 | 0 |
| 19.JKT Tanzania | 1 | 0 | 0 | 1 | 1 | 3 | 0 |
| 20. Biashara United | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 |

# NDAYIRAGIJE AITUMIA BURUNDI SALAMU

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, ikielekea Burundi jana tayari kwa mechi yao ya leo dhidi ya wenyeji hao, Kaimu Kocha Mkuu wa kikosi hicho, Mrundi Etienne Ndayiragije, amesema yupo kazini na kuwataka Warundi wenzake wasitarajie kutakuwapo na huruma yoyote kutoka kwake.

**Kauli hiyo ni faraja kwa mashabiki wa soka nchini ambao wamekuwa na wasiwasi kuwa Ndayiragije anaweza kupanga kikosi dhahifu ili kulibeba taifa lake katika mechi hiyo ya leo.**



Hata hivyo, Ndayiragije ambaye aliiongoza Taifa Stars kuitoa timu ya Taifa ya Kenya, 'Harambee Stars' kwenye mechi ya kuwania kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), amesema yupo kikazi zaidi na kwamba lengo lake ni kuona Tanzania inashinda na kutinga hatua ya makundi ya kuwania kufuzu fainali za Kombe la Dunia 2022 zitakazofanyika nchini Qatar.

"Waajiri wangu kwa sasa ni Watanzania na wote kwa pamoja tuna malengo ya kuhakikisha Tanzania inafuzu Kombe la Dunia, Burundi pia wana ndoto hizo hivyo wanatakiwa kupambana kwa ajili ya hilo," alisema kocha huyo.

Baada ya mechi hiyo, itakayopigwa Uwanja wa Prince Louis Rwagasore jijini Bujumbura, timu hizo zitarudiana Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam Jumapili Septemba 8, mwaka huu na mshindi wa jumla atatinga hatua ya makundi.




Wachezaji wa Taifa Stars wakielekea kukwea pia Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam jana, tayari kwa safari ya kwenda kuivaa Burundi kwenye mechi ya kuwania kutinga hatua ya makundi kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia Qatar 2022. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Azam yaboresha benchi la ufundi

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Azam FC umeliongezea nguvu benchi la ufundi la timu hiyo kufuatia kumwajiri kocha mpya wa viungo, Mrundi Bahati Vivian.

Vivian sasa ataungana na Mrundi mwenzie, Etienne Ndayiragije ambaye ni kocha mkuu wa timu hiyo, kuhakikisha Azam inafanya vizuri kwenye mechi za Ligi Kuu ya Vodacom na Kombe la Shirikisho Afrika.

Mbali na kukabiliwa na mechi za msimu mpya wa Ligi Kuu ya Vodacom, Azam pia ina kibarua kigumu kuhakikisha inaitoa Triangle FC ya Zimbabwe kwenye mechi ya raundi ya kwanza ya Kombe la Shirikisho Afrika ili kuweza kucheza mechi za mchujo kusaka nafasi ya kutinga hatua ya makundi ya michuano hiyo inayoshika nafasi ya pili kwa utajiri barani Afrika kwa ngazi ya klabu baada ya ile ya Ligi ya Mabingwa.

Akizungumza na Nipashe jana, msemaji wa timu hiyo, Jafari Idd alisema kocha huyo atakuwa maalumu kwa ajili ya kuwapa mazoezi ya viungo na kuiongoza timu hiyo kupasha mwili joto kabla ya mechi.

"Tumeongeza nguvu kwenye benchi letu la ufundi, tumepata kocha maalumu wa viungo kutoka Burundi ambaye kocha wetu mkuu amempendekeza kuwa naye," alisema Jafari.

Alisema wameshukuru kumpata kocha huyo ambaye wanaamini ataleta mafanikio katika klabu hiyo.

Aidha, alisema kesho wanatarajia kucheza mchezo wa kirafiki dhidi ya Friends Rangers ya Ligi Daraja la Kwanza, mchezo ambao utachezwa saa moja usiku kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi.

"Alhamisi tutakuwa na mchezo wa kirafiki dhidi ya Friends Rangers kwa ajili ya kujiandaa na mechi yetu dhidi ya Triangle FC," alisema.

# *Ngao ya Jamii Zanzibar yalamba waamuzi wawili*

**Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KAMATI ya waamuzi ya soka visiwani Zanzibar imewaondoa waamuzi wawili waliochezesha mechi ya Ngao ya Jamii kati ya KMKM na Malindi katika orodha ya marefa watakaochezesha mechi zote za ligi zinazosimamiwa na Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF) kutokana na kuvurunda katika mchezo huo uliopigwa Jumapili iliyopita katika Uwanja wa Amaan.

Waamuzi waliokutana na rungu hilo ni Rashid Farhani ambaye alikuwa mwamuzi wa kati na msaidizi wake laini namba moja, Mussa Hemed.


Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na kamati hiyo na kutiwa saini na Katibu wa Kamati ya Waamuzi, Muhusini Ali Rajabu, ameeleza katika mchezo huo mwamuzi na msaidizi wake walishindwa kuchukua maamuzi ya kisheria dhidi ya mlinda mlango wa KMKM, Alex Venance kwa kuwachezea vibaya wachezaji wawili wa Malindi kwa nyakati tofauti, Msati Kassim na Mohmed Ahmed wakiwa ndani ya 18.

Taarifa hiyo iliendelea kueleza kuwa, kamati ya waamuzi imekutana na iliwaita waamuzi wote wanne waliochezesha mechi hiyo na wote walikubali kuwa kweli lilikuwa kosa lililostahili kutolewa penalti na kipa wa KMKM alipaswa kuonyeshwa kadi ya njano, lakini hawakufanya hivyo.

Aidha, iliendelea kueleza kuwa kamati ya waamuzi kulingana na kifungu cha kanuni namba 22 cha kuendesha mashindano ya ZFF kimechukua hatua ya kuwaondoa katika orodha hiyo ya waamuzi na kuwapiga faini ya Sh. 200,000 kwa kila mmoja ambayo hadi ifikapo Oktoba 3, mwaka huu inatakiwa iwe imelipwa.

Adhabu hiyo, imepata baraka zote kutoka ZFF, hivyo wanapaswa kuitumikia kama ilivyoagizwa.

Michezo
Jumatano Septemba 4, 2019
Nipashe




Icardi: Kutua PSG ni hatua kubwa

UKURASA 30



Mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba kesho watarejea tena mazoezini baada ya mapumziko ya siku mbili.

# Zahera agoma kuivaa Mbao, TFF yamfungia

## ●●● Pia yeye na Masau Bwire walimwa faini, mwamuzi aliyekataa bao la Ruvu Shooting naye afungiwa...

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI Kocha Mkuu wa Klabu ya Yanga, Mwinyi Zahera, akigoma kabisa kucheza mechi za kirafiki na timu za Ligi Kuu, katika kambi yao ya Mwanza kujiandaa na mchezo wao wa raundi ya kwanza wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Zesco United ya Zambia, pia amekutana na rungu la Kamati ya Bodi ya Ligi Kuu ya Uendeshaji na Usimamizi wa Ligi, ambayo imemfungia mechi tatu na kumpiga faini.

**Yanga ilipanga kucheza mechi kadhaa ikiwa kambini Mwanza, mojawapo ikiwa dhidi ya Mbao FC, lakini Zahera amegomea mechi hizo kwa kuhofia wachezaji wake kuumizwa na kudai hilo lilitokea pia wakati walipocheza mechi ya kirafiki dhidi ya Polisi Tanzania kuelekea mechi yao dhidi ya Township Rollers ya Botswana.**

Akizungumza na Nipashe jana, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Mashindano ya Klabu ya Yanga, Saady Khimji, alisema Zahera ameweka wazi kwamba hawezi kukubali timu yake icheze na timu kubwa mkoani humo, kwa kile anachodai huwa zinawakamia bila kuelewa wanakwenda kucheza mchezo wa kimataifa.

Makamu huyo alisema awali walipanga kukutana na Mbao FC lakini kocha amesema anahofia wanaweza kuumiza wachezaji wao kama ilivyokuwa wakati walipocheza dhidi ya Polisi Tanzania.

"Zahera amekaa na kamati ya mashindano akatupa hoja zake tukakubaliana kwa pamoja kwa sababu anasema tulipocheza na Polisi Tanzania Kilimanjaro walitukamia sana mpaka kuumiza vibaya wachezaji wetu wawili. "Kocha amesema bora acheze na timu za Ligi Daraja la Kwanza ambazo zitacheza nao zikiwa zinajiandaa kupanda Ligi Kuu na sisi tutacheza kwa tahadhari kubwa," alisema Saady.

Wakati huo huo, Kamati ya Bodi ya Ligi Kuu ya Uendeshaji na Usimamizi wa Ligi katika kikao chake cha Septemba 2, mwaka huu ilipitia matukio mbalimbali ya Ligi Kuu ya Vodacom (VPL) msimu wa 2019/2020 iliyoanza rasmi Agosti 24, 2019 na kufanya maamuzi mbalimbali.

Katika mechi namba tisa- ambayo Yanga ilikubali kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Ruvu Shooting, Mwamuzi Msaidizi, Janeth Balama amefungiwa miezi mitatu kwa kushindwa kutafsiri sheria, hivyo kusababisha akatae bao halali lililofungwa na Ruvu Shooting katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Uhuru Agosti 28, mwaka huu, adhabu hiyo ikitolewa kwa kuzingatia Kanuni ya 39(1) ya Ligi Kuu kuhusu Udhibiti kwa Waamuzi.

Kocha wa Yanga, Zahera ametozwa faini ya Sh. 500,000 (laki tano) kwa kuvaa mavazi yasiyo nadhifu na ya heshima katika mechi hiyo, kinyume cha Kanuni ya 14(2m) ya Ligi Kuu kuhusu Taratibu za Mchezo. Adhabu dhidi yake imetolewa kwa kuzingatia Kanuni ya 41(13) ya Ligi Kuu kuhusu Udhibiti kwa Makocha. Kadhalika, Zahera amefungiwa kuiongoza timu yake katika mechi tatu za Ligi Kuu ya Vodacom kwa kutoa shutuma na kejeli kwa Bodi ya Ligi katika mkutano na waandishi wa habari baada ya mechi dhidi ya Ruvu Shooting. Adhabu hiyo imetolewa kwa kuzingatia Kanuni ya 41

Huku Klabu ya Yanga ikipewa onyo kali kwa kushindwa kuhakikisha Zahera anaongoza benchi la ufundi la timu yake akiwa katika mavazi nadhifu na ya heshima. Adhabu dhidi ya klabu hiyo ni kwa mujibu wa Kanuni ya 14(3) ya Ligi Kuu kuhusu Taratibu za Mchezo.

Naye Mkurugenzi wa Ruvu Shooting, Masau Bwire ametozwa faini ya Sh. 200,000 (laki mbili), kwa kuingia ndani ya uwanja (eneo la kuchezea) baada ya filimbi ya mwisho, kinyume cha Kanuni ya 14(10) ya Ligi Kuu kuhusu Taratibu za Mchezo. Adhabu dhidi yake imetolewa kwa kuzingatia Kanuni ya 14(49) ya Ligi Kuu kuhusu Taratibu za Mchezo.

# Mo Dewji moto, hataki kupoa Simba

**Na Mwandishi Wetu**

HUKU mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba wakirejea mazoezini kesho kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu ya Vodacom dhidi ya Mtibwa Sugar itakayopigwa Uwanja wa Uhuru Septemba 17, mwaka huu, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya klabu hiyo, Mohamed "Mo" Dewiji ameendelea kuwasha moto wa kurejesha morali kwa wachezaji na mashabiki wa timu hiyo.

Mashabiki wa Simba wamekatishwa tamaa na klabu yao baada ya kutolewa raundi ya awali ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa faida ya bao la ugenini na UD Songo ya Msumbiji kufuatia kutoka suluhu ugenini kabla ya kulazimishwa sare ya bao 1-1 Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Na mwishoni mwa wiki Mo aliwataka Wanasimba kumsamehe kwa kuwa mkimya na maumivu ya matokeo waliyoyapata, ambapo aliwataka kutovunjika moyo wala kukata tamaa.

Lakini jana Mo alifunguka tena akiwaamsha mashabiki na wachezaji wa klabu hiyo kwa kueleza: "Ujumbe huu ni kwa wachezaji wa @Simba SC Tanzania na mashabiki, mabingwa hawaelezwi kwa ushindi wao bali namna wanavyoanza baada ya kuanguka."

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >